

SALA YA SAA MAKUBWA

YA KUZALIWA KRISTU

YA EPIFANIA YA BWANA YESU KRISTU

YA MUKAZI TANO KUBWA YA JUMA TAKATIFU

CENTRE DE LA MISSION ORTHODOKSE

KOLWEZI KONGO

1999

SAA MAKUBWA YA KUZALIWA KRISTU

SAA WA KWANZA

Padri: Abarikiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

Msomaji: Amina. Mungu Mtakatifu, Mweza Mtakatifu, Musiye kufa Mtakatifu, utuhurumie. (*mara tatu*). Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasana siku zote, hata milele na milele. Amina.

Utatu Mtakatifu Kamili utuhurumie, Bwana utusamehe zambi zetu, Rabi utuondolee makosa yetu, mtakatifu utukaribie na uponye magonjwa yetu. Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama mbinguni, utupe sisi leo chakula chetu cha kila siku, utusamehe ndeni zetu kama sisi vilevile tunawasamehe walio na ndeni zetu, tena usitutie katika majaribu, lakini utuokoe na yule mwovu

Padri: Kwa kuwa Ufalme, na uwezo, na utukufu ni kwako, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

Msomaji: Amina. Bwana hurumia (*mara kumi na mbili*).

Njoooni tumwinamie na tumsujudu Mungu na Mfalme wetu.

Njoooni tumwinamie na tumsujudu Kristu Mfalme wetu.

Njoooni tumwinamie na tumsujudu Yeye Kristu aliye Mfalme wetu.

Zaburi 5(6)

Sikiliza maneno yangu, Ee Bwana, Ungalie mafikili yangu. Usikie sauti ya kilio changu, Mufalme wangu, na Mungu wangu: Kwa maana ninaomba kwako. Ee Bwana, asubui utasikia sauti yangu; ásubui nitatengeneza maombi yangu kwako, na kuangalia sana. Kwa maana wewe si Mungu anayependezwa na uovu; mwovu hatakaa kwako. Wenye majivuno hawatasimama mbele ya macho yako; unachukia watenda wote wa uovu. Utaharibu wale wanaosema uwongo; Bwana anachukia mwuaji na mwenye hila. Lakini mimi, kwa wingi wa wema wako nitaingia nyumbani mwako; katika kukuogopa wewe nitaabudu kwa upande wa hekalu lako takatifu. Uniongoze, ee Bwana, kwa haki yako kwa sababu ya adui zangu; unifanyie njia yako wazi mbele ya uso wangu. Kwa maana hapana uaminifu kinywani mwao; mtima wao ni shimo tupu; koo lao ni kaburi wazi; Wanabembeleza na ulimi wao. Uwahesabie zambi zao, ee Mungu; Waanguke kwa mashauri yao wenyewe; uwatoe inje katika wingi wa makosa yao, kwa maana wamekuasi

wewe. Lakini wote wanaokuwekea tumaini lao wafurahi, wapige kelele daima kwa furaha kwa sababu unawasimamia; wao vilevile wanaopenda jina lako wafurahi ndani yako. Kwa maana utabariki mwenye haki; ee Bwana, utamuzungusha na mapendeleo kama ngabo.

Zaburi 44 (45).

Moyo wangu umefurika kwa neno jema: Ninasema maneno niliyofanyizia mufalme; Ulimi wangu ni kalamu ya mwandishi tayari. Wewe ni muzuri sana kuliko wana wa watu; neema imemwangwa midomoni mwako; kwa hivi Mungu amekubariki hata milele.

Ujifungie upanga wako pajani, ee wewe mwenye uwezo, utukufu wako na enzi yako.

Katika enzi yako panda na kuchukiliwa na baraka, kwa sababu ya kweli na upole na haki; na mukono wako wa kuume utakufundisha maneno ya kuogopesha. Mishale yako ni mikali, watu wanaanguka chini yako, wao ni moyoni mwa adui za mufalme. Kiti chako cha ufalme, ee Mungu, ni cha milele na milele; fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya haki. Umependa haki na kuchukia uovu; kwa hivi Mungu, Mungu wako, amekupakaa na mafuta ya furaha kupita wenzako. Mavazi yako yote yananuka manemane, na uudi na mdalasani; Toka majumba ya pembe vinubi vimekufurahisha. Binti za wafalme ni kati ya wanawake wako wenye heshima; kwa mukono wako wa kuume anasimama malkia amevaa zahabu ya Ofiri. Sikiliza, ee binti, na fikili, na tega sikio lako; sahau vilevile watu wako mwenyewe, na nyumba ya baba yako; hivi mufalme atatumaini uzuri wako; maana yeye ndiye Bwana yako, nawe umwabudu. Na binti ya Tiro atakuwa pale na zawadi; hata matajiri kati ya watu watajipendekeza kwako, Binti ya mufalme aliye ndani ni mwenye utukufu; mavazi yake ni ya nyuzi za zahabu. Atapelekwa kwa mufalme akivaa mavazi yaliyofumwa kwa uzuri; Mabikira, wenzake wanaomufuata watapelekwa kwako. Wataongozwa kwa furaha na shangwe; Na kuingia katika nyumba ya mufalme. Kwa pahali pa baba zako watakuwa watoto wako, utakaowafanya kuwa wakubwa katika inchi zote. Nitafanya jina lako kuwa ukumbusho katika vizazi vyote, kwa hivi mataifa watakushukuru milele na milele.

Zaburi 45(46)

Mungu ni kimbilio letu na nguvu yetu, Musaidia aliye karibu sana wakati wa mateso.

Kwa hivi hatutaogopa, hata inchi ikibadilika, na hata milima ikihamishwa moyoni mwa bahari; hata maji yao yakinguruma na kuchafuka, hata milima ikitikisika kwa kiburi chake. Kuna muto, vijito vyake vinafurahisha muji wa Mungu, pahali patakatifu pa makao yake aliye juu. Mungu ni katikati yake; hautatikiswa; Mungu atausaidia, asubui mapema. Matalia waligazibika, falme zilitikisika; akatoa sauti yake, inchi ikayeyuka. Bwana ya majeshi ni pamoja nasi, Mungu wa Yakobo ni kimbilio letu. Kujeni, mutazame kazi za Bwana, namna alivyofanya ukiwa katika inchi. Anakomesha vita hata mwisho wa dunia; anavunja upinde, na kukata mukuki, anachoma magari kwa moto. Munyamaze, mujue ya kuwa mimi ni Mungu; nitatukuzwa kati ya mataifa, nitatukuzwa katika inchi. Bwana ya majeshi ni pamoja nasi; Mungu wa Yakobo ni kimbilio letu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Allilulia, allilulia, allilulia, utukufu kwako, ee Mungu. (*mara tatu*), Bwana hurumia (*mara tatu*).

Kisha tunasoma hii mwimbo:

Utukufu kwa Baba. . .

Zamani Maria mwenye kuchukua tunda isiyopandwa akajiandikisha kule Bethlehemu pamoja na mtukufu Yosefu wa kizazi cha Daudi. Wakati wa kuzaa ilitimia na hakukuwa fasi katika nyumba ya wageni; lakini kwa Malkia pango ikawa nyumba safi: Kristu anakuja duniani kuinua sura yake iliyoanguka.

Sasa na siku zote. . . Theotokion.

Namuna gani tutakuita ewe Mujaliwa neema? Kwa sababu ulileta duniani jua ya haki. Paradizo? Kwa sababu uliotesha ua isiyo harabika. Kwa sababu ulibaki Bikira bila uharibifu. Mama kamili? Kwa sababu ulichukua katika kifua chako takatifu Mtoto, aliye Mungu wawote. Umuombe yeye aokoe mioyo yetu.

Kisha tunaimba hii wimbo na muziki ya kuachana (Idiomela).

Sauti ya mnane.

Ee Bethlehemu, ujitayarisha, sanduku ya kulishia nyama iwe tayari kwa kusaidia na pango kwa kumupokea Bwana? Tazama ukweli safi imekuja, kivuli cha sheria imeondolewa: Anapozaliwa kwa Bikira, Mungu ameonekana kwa Wanadamu, amechukua hali yetu na kuigeuza. Adamu mupya na Eva wanapaza sauti: Wema wa Mungu imeonekana duniani sababu ya kuokoa wanadamu.

Tunaimba hii mara wa mbili, bila shairi.

Shairi: Mungu alikuja toka Temani, na Mutakatifu toka mulima Parani.

Sauti wa tatu.

Sasa itatimizika kwa siri unabii yenye kusema: «Na wewe Bethlehemu, katika inchi ya Yudea, wewe si mudogo kati ya watawala wa Yuda, wewe mwenye kutayarisha pango; kwa maana kwako atatota mtawala wa mataifa, atazaliwa kwa Bikira, Kristu Mungu wetu, atakayewachunga watu wangu, Israeli mupya. Sisi wote pamoja tutukuzeni utukufu wake kubwa.

Shairi: Ee Bwana nimesikia sauti yako, nimejaa na woga.

(Na tunaimba mara ingine hii wimbo.)

Utukufu kwa Baba. . . Sauti wa mnane.

Ni hivi Yosefu anamwambia Bikira Maria: Hili ni tendo gani ninaona kwako? Sijui, ni lenye kufichwa, tazama nashangaa. Upesi, kwa siri ondoka mbali yangu. Maria, hili ni tendo gani ninaona kwako? Ni haya kwangu pa hali pa heshima, ni sikitiko pahali pa furaha, pahalipasifa umenipati ahaya. Sivumilie kemeo la watu, maana nimekupokea kama bikira mtakatifu kwa makuhani wenye kutumia katika Hekalu la Bwana, tazama hii ninaona sasa.

Sasa na siku zote. . . Tunaimba mara ingine hii wimbo.

Kisha: Prokimenon ya Unabii. Sauti ya ine.

Bwana aliniambia: Wewe ni mwana wangu; lao nimekuzaa.

Shairi:Uniombe, na nitakupa mataifa kuwa uriti wako.

Zaburi Mikea

Sasa utajikusanya kwa majeshi, ee binti ya majeshi; ametuzunguka kwa vita; kwa fimbo watapiga shavu la mwamuzi wa Israeli. Lakini wewe, Betelehemu-Efurata, ulio mudogo katika elfu za Yuda, katika wewe atanitokea mumoja, atakayekuwa mutawala katika Israeli; matokeo yake ni tangu zamani, tangu milele. Kwa sababu hii atawatoa, hata wakati wa kuzaa kwake aliye na uchungu, kisha mabaki ya ndugu zake yatarudi kwa wana wa Israeli, 4 Naye atasimama na atakulisha kundi lake kwa nguvu za Bwana kwa enzi jina la Bwana Mungu wake, na watakaa, kwa maana sasa atakuwa mukubwa hata miisho ya dunia.

Matendo ya Mitume

Barua ya Mtume Paulo kwa Waebrania tutasoma. (1, 1-12).

Mungu, aliyesema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, 2 katika siku hizi za mwisho amesema nasi katika Mwana, aliyemuweka kuwa muriti wa vitu vyote, kwa yeye aliyefanya ulimwengu. 3 Yeye akiwa kungaa kwa utukufu wake, na chapa ya nafsi yake mwenyewe, akichukua vitu vyote kwa Neno la uwezo wake, akikwisha kufanya katika yeye utakaso wa zambi zetu, aliketi mukono wa kuume wa Mwenye Ukuu; 4 amepata kuwa muzuri kupita malaika, kwa sababu ameriti jina lenye utukufu kuliko lao. 5 Kwa maana Mungu alimwambia malaika gani wakati wo wote: Wewe ndiwe Mwana wangu, Mimi leo nimekuzaa? Na tena mimi nitakuwa kwake Baba, na yeye atakuwa kwangu Mwana? Na tena, wakati alipoleta muzaliwa wa kwanza katika duniua, anasema: Na malaika zote za Mungu wamwabudu. 7 Na juu ya malaika anasema: Anayefanya malaika zake kuwa pepo, Na watumishi wake ndimi za moto. 8 Lakini juu ya Mwana anasema: Kiti chako cha ufalme, Mungu, ni cha milele na milele, na fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya haki. 9 Umependa haki, umechukua uovu; Kwa sababu ile Mungu, Mungu wako, amekutia mafuta, Mafuta ya furaha kupita wenzako. 10 Na tena: Wewe Bwana, katika mwanzo umeweka misingi ya inchi, na mbingu ni kazi za mikono yako. 11 Hizi zitaharibika, lakini wewe unabaki; Na hizi zote zitachakaa kama nguo, 12 Na kama mavazi utazikunja, Nazo zitabadilika; Lakini wewe ni sawasawa saa zote, na miaka yako haitakoma.

EVANGELIO

Hekima; Inukeni tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.

Msomaji: Na kwa roho yako.

Somo ya Evangelio Takatifu ilionandikwa na Mwevangelizaji Matayo, tusikilize.

Msomaji: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

Padri: Kuzaliwa kwa Yesu Kristu kulikuwa hivi: Maria mama yake alipoposwa na Yosefu, mbele ya kukaribiana, alionekana ana mimba kwa Roho Mutakatifu. Na Yosefu mume wake, akiwa mutu wa haki, wala hakutaka kumupa haya wazi, alikusudi kumwacha kwa siri. Lakini wakati alipokuwa akifikili maneno haya, tazama, malaika ya Bwana alimutokea katika ndoto, akisema: Yusefu, mwana wa Daudi, usiogope kuchukua Maria muke wako, maana mimba yake ni kwa uwezo wa Roho Mutakatifu. Naye atazaa mwana; nawe utamwita jina lake Yesu, kwa sababu ndiye atakayeokoa watu wake toka zambi zao. Maneno haya yote yamekuwa ili litimie neno lililosemwa na Bwana kwa nabii, akisema: Tazama, Bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana, nao watamwita jina lake Emanueli; maana yake Mungu pamoja nasi. Na wakati Yosefu alipoamka toka usingizi, alifanya kama malaika ya Bwana alivyomwagiza; akachukua muke wake; lakini hakumujua hata alipozaa mwana wake; aliita jina lake Yesu. (Matayo 1, 18-24).

Kisha Msomaji atasoma: Ongoza mwendo wangu katika neno lako: Wala uovu wowote usinitawale.

Unikomboe na maneno ya mutu: Hivi nitachunga mafundisho yako yote.

Uangazie Mutumishi wako na uso wako; na unifundishe amri yako.

Kinyuwa changu kinajazwa na sifa yako Bwana, kama ninavyotukuza ziku zote uzuri wako.

Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

Kisha tunasoma Kontakion:

Leo Bikira anajitayarisha kwa kuzaa katika pango Neno wa mbele ya nyakati. Ewe dunia yote kwa hii habari imba na kucheza, tukuza pamoja na Malaika na Wachungaji huyu alitaka kuwa mwana mchanga, yeye aliye Mungu wa mbele ya nyakati.

Kisha tunasema: Bwana hurumia, (*mara makumi ine*) na hii sala:

Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa, na kutukuzwa wakati wote na katika kila saa mbinguni na duniani, uliye mwadilifu, mrahimu tele, mfazili sana unayependa wenye haki, tena kuwahurumia wenye zambi; unayewaita wote kuona wokovu, ukiwaahidi vitu vema vilivyokuja; wewe, ee Bwana, hata katika saa hii uyapokee maombi yetu, na kuyashurtisha maisha yetu njiani pa amri, uuzitakase roho zetu, uyasafishe miili yetu, uyatengeneze mafikira zetu, uzinyoshe nia zetu; ukatuokoe na kila shida, ubaya, na teso, utulindie kwa Malaika wako, ili sisi tukiwa na utunzi na uongozi wao, tufike katika umoja wa imani na kuujulisha utukufu wako usiofikika. Kwa kuwa unahimidiwa milele na milele. Amina.

Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia. Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . . Uliye wadamani. . . Kwa jina la Bwana barikia, ee padri:

Mungu atufazili na kutubariki, atuangazie uso wake na kutuhurumia.

Padri anasoma hii sala:

Kristu, nuru ya kweli, aliyeangaza na kutakasa kila mutu, anayekuja duniani, na imeonekana kwetu nuru ya uso wako, ulituonyesha nuru ya uso wako isio zimika na

ongoza mwendo wetu katika kazi ya amri yako. Kwa maombi ya Mama wako Mtakatifu na ya watakatifu wote. Amina.

SAA WA TATU

Msomaji mara moja anasoma:

Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . . Bwana hurumia (*mara kumi na mbili*).

Njooi tumwinamia. . .

Kisha anasoma:

Zaburi 66(67)

Mungu aturehemu na atubariki, atuangazie uso wake. Njia yako ijulikane duniani, wakovu wako katika mataifa yote. Watu wakusifu, ee Mungu; watu wote wakusifu. Mataifa washangilie na waimbe kwa furaha, maana utahukumu watu kwa haki, na kutawala mataifa duniani. Watu wakusifu, ee Mungu; watu wote wakusifu. Inchi imetoa mazao yake; Mungu, hata Mungu wetu; atatubariki. Mungu atatubariki. Miisho yote ya dunia itamwagopa.

Zaburi 86 (87).

Musingi wake nikatika milima mitakatifu. Bwana anapenda malango ya Sayuni kuliko makao yote ya Yakobo. . Maneno ya utukufuyanasemwa juu yako, Ee muji wa Mungu. Nitataja Rahaba na Babeli kama katikati yao wanaonijua; Tazama Filistia na Tiro, pamoja na Etiopia; Huyu alizaliwa pale. Ndiyo, itasemwa juu ya Sayuni: Huyu na huyu alizaliwa ndani yake; Naye aliye juu atausimamisha. Wana atahesabu wakati anapoandika watu, Huyu alizaliwa pale. Wao wanaoimba nao wanaocheza vilevile watasema: Visima vyangu vyote ni ndani yako.

Kisha Zaburi 50(51):

Unirehemu, ee Mungu, sawasawa na wema wako, sawasawa na wingi wa rehema zako uzime makosa yangu. Unioshe kabisa na uovu wangu, na kunisafisha na zambi yangu. Maana ninajua makosa yangu, na zambi yangu ni mbele yangu daima. Nimekukosea wewe peke yako, na kufanya yaliyo mabaya machoni mwako, ili ujulikane kuwa mwenye haki wakati unaposema, na kuwa safi wakati unapotoa hukumu. Tazama, niliumbwa katika hali ya uovu, na katika makosa mama yangu alinichukua mimba. Tazama, wewe unataka kweli moyoni, na kwa siri utanijulisha hekima. Unisafishe kwa hisopo na nitakuwa safi, unioshe, na nitakuwa mweupe kupita theluji. Unifanye kusikia furaha na shangwe, ili mifupa uliyovunja ifurahi. Ufiche uso wako usitazame zambi zangu, na uzima maovu yangu yote. Umba moyo safi ndani yangu, ee Mungu, na ufanye upya roho nzuri ndani yangu. Usinitenge na uso wako, wala usiondolee Roho yako mutakatifu. Unirudishie furaha ya wokovu wako, unitegemeze kwa roho ya tayari. Halafu nitafundisha wenye makosa njia zako, na wenye zambi watarudi kwako. Uniponyeshe na damu ya watu, ee Mungu, wewe Mungu wa wokovu wangu, ulimi wangu utaimba na

sauti haki yako. Ee Bwana, ufungue midomo yangu, na kinywa changu kitaonyesha sifa zako. Maana hupendezwi na zabihu, ao ningeitoa, hufurahi kwa sadaka ya kuteketezwa. Zabihu za Mungu ni roho ya kuvunjika, moyo uliovunjika na wa toba hutauzarau, ee Mungu. Utendee Sayuni mema kwa mapenzi yako, ujenge kuta za Yerusalema. Halafu utafurahi kwa zabihu za haki, kwa sadaka ya kuteketezwa, na sadaka nzima ya kuteketezwa, halafu watatoa ngombe ndume juu ya mazabahu yako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Allilua, allilua, allilua, utukufu kwako, ee Mungu. (*mara tatu*), Bwana hurumia (*mara tatu*).

Kisha tunasoma hii mwimbo:

Utukufu kwa Baba. . .

Zamani Maria mwenye kuchukua tunda isiyopandwa akajiandikisha kule Bethlehemu pamoja na mtukufu Yosefu wa kizazi cha Daudi. Wakati wa kuzaa ilitimia na hakukuwa fasi katika nyumba ya wageni; lakini kwa Malkia pango ikawa nyumba safi: Kristu anakuja duniani kuinua sura yake iliyoanguka.

Sasa na siku zote. . . Theotokion.

Ee Mzazi-Mungu, ndiwe mzabibu wa kweli wenyi kuzidisha tunda la uzima. Tunakuomba: Utuombee, ee Malkia, pamoja na Mitume na Watakatifu wote, ili roho zetu zipate rehema.

Kisha tunaimba hii wimbo (Idiomela):

Sauti ya sita

Ni Yeye Mungu wetu, mutu hata mumoja hawezi kufanana naye, ni Yeye Bikira alizaa na mwenyi kuishi kati ya wanadamu; Mwana wa pekee amelala katika sanduku la kulishia nyama kama mtoto, tazama, Bwana wa utukufu amefunikwa vitambaa, nyota inaalika wenye akili kwa kumuabudu; naa sisi wenyewe tunaimba: Okoa roho zetu, ee Utatu Mtakatifu.

Tunaimba hii wimbo mara ingine bila shairi.

Shairi: Mungu alikuja toka Temani, na Mutakatifu toka mulima wa kivuli.

Sauti ya mnane.

Mbele ya kuzaliwa kwako, ee Bwana, walipoona hii fumbo wakatetemeka, majeshi ya mbinguni walishangaa; kwa sababu kwa kutaka kwako ulijifanya kuwa mtoto, wewe uliyepamba mbingu kwa nyota na kuweka nyama katika zizi, wewe mwenye kushika mipaka ya dunia mikononi mwako; kwa tendo lako la wokovu, ee Bwana, inaonekana rehema yako kubwa na mapendo ya roho yako. Utukufu kwako.

Shairi: Ee Bwana nimesikia sauti yako, nimejaa na woga.

Tunaimba hii wimbo mara ingine.

Utukufu kwa Baba. . . Sauti wa tatu.

Ee Yosefu, utuambie, namna gani Bikira uliyepokea kwa mlango ya Hekalu takatifu unamupeleka mwenyi kuwa na mimba kule Bethlehemu? Yeye anajibu: Mimi kisha kuangalia unabii na kisha Malaika kuniambia nasadiki kweli ya kwamba Maria atazaa

Mungu kwa namna isiyoweza kufasiriwa; na wenye akili watatoka mashariki kuja kumwabudu, watumutukuza na ibada ya umungu, watumutolea zawadi ya heshima kubwa. Wewe mwenye kutwa mwili kwa ajili yetu, ee Bwana, utukufu kwako.

Sasa na siku zote. . . Mara ingine hii wimbo.

Prokimenon ya Unabii. Sauti ya ine.

Maana kwa ajili yetu mutoto amezaliwa, tumepewa mutoto mwanamume.

Shairi: Na utawala utakuwa juu ya bega lake.

Unabii ya Nabi Yeremia tutasoma:

Unabii Yeremia. Kitabu ya Baruka (3, 36-4, 4)

Yey ndiye Mungu wetu, wala hakuna mwingine wa kufanana naye. Amevumbua njia zote za Hekima, akampatia Yakobo, mtumishi wake, na Israeli, mpendwa wake: nayo Hekima ikaonekana duniani, ikakaa kati ya watu. Hekima, ndicho kitabu cha amri za Mungu, na sheria inayodumu milele. Wote wenye kuishika watapewa uzima, lakini wenye kuiacha watakufa Rudi, ee Yakobo, ukaishike sheria, katika ungaro wake uuendee mwangaza: Usimpe mwingine utukufu wako, wala taifa la kigeni mafaa yako. Tuna heri sisi, ee Israeli: maana tumefumbuliwa mambo yanayompendeza Mungu.

Matendo ya Mitume.

Barua ya Mtume Paulo kwa wa Galatia tutasoma.

Lakini mbele ya kuja kwa imani, tulichungwa chini ya sheria, tumefungwa kwa imani itakayofunuliwa nyuma. Hivyo torati ilikuwa mwalimu wa kutuleta kwa Kristu, tupewe haki kwa imani. Lakini sasa imani imekwisha kuja, hatuko tena chini ya mwalimu; maana ninyi wote ni wana wa Mungu, kwa imani, katika Yesu Kristu. Maana ninyi wote ni wana wa Mungu, kwa imani, katika Yesu Kristu. Maana ninyi wote muliobatizwa na kuingizwa katika Kristu, mumevaa Kristu. Hapana Muyuda, wala Muyunani, hapana mutumwa wala huru, hapana mwanamume wala mwanamuke. Maana ninyi wote ni mumoja katika Yesu Kristu. Na kama mwanamuke. Maana ninyi wote ni mumoja katika Yesu Kristu. Na kama ninyi ni wa Kristu, basi, mumekuwa uzao wa Abrahamu na wariti kwa ahadi.

EVANGELIO

Hekima; Inukeni tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.

Msomaji: Na kwa roho yako.

Somo ya Evangelio Takatifu ilionandikwa na Mwevangelizaji Luka, tusikilize.

Msomaji: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

Padri:

Katika siku zile amri ilitoka kwa Kaisari Augusto ili majina ya watu wote katika dunia yaandikwe. Maandiko haya yalifanywa kwanza wakati Kurenio alipokuwa mutawala wa Suria. Na watu wote walikwenda kuandikwa, kila mutu kwa muji wake. Na Yosefu vilevile aliondoka Galilaya toka muji wa Nazareti, akapanda kwenda Yuda hata muji wa

Daudi ulioitwa Betlehemu, kwa sababu alikuwa wa jamaa ya Daudi, aandikwe pamoja na Maria aliyepatana kuwa muke wake naye ana mimba. Walipokuwa pale, siku zake za kuzaa zilitimia. Akazaa mwanamume wake wa kwanza akamufunga nguo za kitoto, akamulalisha katika sanduku ya kulisha nyama, kwa sababu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni.

Kisha Msomaji anasoma:

Ahimidiwe Bwana wetu, ahimidiwe Bwana siku kwa siku. Mungu huyu anatumitea wokovu. Mungu wetu ni Mungu mwenye kuokoa.

Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

Kisha tunasoma Kontakion:

Leo Bikira anajitayarisha kwa kuzaa katika pango Neno wa mbele ya nyakati. Ewe dunia yote kwa hii habari imba na kucheza, tukuza pamoja na Malaika na Wachungaji huyu alitaka kuwa mwana mchanga, yeye aliye Mungu wa mbele ya nyakati.

Kisha tunasema: Bwana hurumia, (*mara makumi ine*) na hii sala: Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa. . . (Ona ndani ya hii kitabu, ukurasa 5).

Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia. Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . . Uliye wadamani. . . Kwa jina la Bwana barikia, ee padri:

Mungu atufazili na kutubariki, atuangazie uso wake na kutuhurumia.

Padri anasoma hii sala:

Mungu, Rabi, Baba Mwenyezi; Mwokozi, Mwana wa pekee, Yesu Kristu na Roho Mtakatifu, umungu moja, nguvu moja, unihurumie; wakati wa mwisho uniokoe mimi mukoosifu wako, kwani unabarikiwa milele na milele. Amina.

SAA WA SITA

Musomaji anasoma mara moja:

Njooi tumwinamie na tumsujudu Mungu na Mfalme wetu.

Njooi tumwinamie na tumsujudu Kristu Mfalme wetu.

Njooi tumwinamie na tumsujudu Yeye Kristu aliye Mfalme wetu.

Zaburi 71(72)

Umupe mufalme hukumu zako, Ee Mungu, Na mwana wa mufalme haki yako. Atahukumu watu wako kwa haki, Na masikini zako kwa hukumu. Milima italetea watu salama, Na vilima, katika haki. Atahukumu masikini za watu, Ataokoa wana wa wenye hitaji, Na atavunja mutesaji vipande vipande. Watakuogopa wakati wote wa kudumu kwa jua, Na wakati wa mwezi, kizazi kwa kizazi. Atashuka kama mvua juu ya majani yaliyokatwa; Kama manyunu yanayonyweshwa inchi. Katika siku zake mwenye haki

atasitawi; Na wingi wa salama, hata mwezi utakapokoma. Naye atatawala vilevile toka bahari hata bahari, Na toka Muto hata miisho ya dunia. Wao wanaokaa jangwani watainama mbele yake, Na adui zake wataramba mavumbi. Wafalme wa Tarsisi na wa visanga wataleta kodi; Wafalme wa Sheba na Seba watatoa zawadi. Ndiyo, wafalme wote wataanguka mbele yake, Mataifa yote watamutumikia. Kwa maana ataponyesha mwenye hitaji wakati anapolia, Na masikini, asiye na musaidia. Atahurumia masikini na mwenye hita. ii, Na nafsi za wenye hitaji ataziokoa. Atakomboa nafsi yao na jeuri na ukali; Na damu yao itakuwa ya damani machoni mwake; Nao wataishi; naye atapewa ya zahabu ya Sheba; Na watu watamwombea daima. Watamubariki muchana kutwa. Na nafaka zitakuwa nyingi juu ya kichwa cha milima; Matunda yake yatatetemeka kama Lebanoni; Na watu wa muji watasitawi kama majani juu ya inchi. Jina lake litadumu milele; Jina lake litakuwa na wazao kwa wakati wote wa jua; Watu wote watabarikiwa ndani yake; Mataifa yote watamwita heri. . Heri ni Bwana Mungu, Mungu wa Israell, anayetenda maneno ya ajabu sana: Na Iibarikiwe jina lake lenye ut. ukufu kwa mllele; Dunia yote ijae na utukufu wake. Amina na Amina. Maombi ya Daudi, mwana wa Yese, yamekwisha.

Zaburi 131 (132)

Bwana, ukumbukie Daudi, Taabu zake zote; Namna alivyoapia Bwana, na kuweka nazirì kwa Mwenye Uwezo wa Yakobo; Hakika sitaingia hemani mwa nyumba yangu, Wala sitapanda kwa kitanda changu; Sitaacha macho yangu kupata usingizi, Wala kope zangu kusinzia; Hata nitakapopatia Bwana pahali, Makao kwa Mwenye Uwezo wa Yakobo. Tazama, tulisikia habari zake katika Efurata, Tuliiona katika shamba la Yeanmu. Tutaingia katika makao yake; Tutaabudu kwa kiti cha miguu yake. Simama, Bwana, uende katika pahali pako pa raha, Wewe na sanduku ya nguvu yako. Makuhani yako wavikwe haki; Na watakatifu wako wapige kelele kwa furaha. Kwa ajili ya mutumishi wako Daudi. Usigeuze uso wako mbali na mupakaliwa mafuta wako.

Bana aliapia Daudi katika kweli; Hatageuka mbali nayo. Wa wazao wa mwili wako Nitaweka juu ya kiti chako cha ufalme. Kama wana wako wakishika agano langu Na ushuhuda wangu nitakaowafundisha, Wana wao vilevile watakaa juu ya kiti chako cha ufalme mllele. Kwa kuwa Bwana amechagua Sayuni; Ameitamani kwa kao lake. Hapa ni pahali pangu pa raha mijele; Nitakaa hapa: maana nimepatamani. Hakika nitabariki vyakula vyake: Na nitashibisha masikini zake chakula. Nitavika makuhani yake wokovu vilevile: Na watakatifu wake watapiga kelele kwa furaha. Pale nitachipushia pembe ya Daudi: Nimetengeneza taa kwa mupakaliwa mafuta wangu. Nitavika adui zake haya: Lakini juu yake mwenyewe taji yake itasitawi.

Zaburi 90 (91)

Yeye anayekaa kwa pahali pa maficho yake aliye juu atakaa chini ya kivuli cha Mwenyezi. Nitasema juu ya Bwana, yeye ni pahali pangu pa kukimbilia na boma la nguvu langu, Mungu wangu ninayemwamini. Kwa maana atakuokoa toka mutego wa muwindaji ndege, na kwa tauni ya uharibifu. Na manyoya yake atakufunika. Na chini ya mabawa yake utakimbilia, kweli yake ni ngabo na kigabo. Hutaogopa kwa woga wa usiku, wala kwa mushale unaoruka muchana; kwa tauni inayotembea katika giza, wala kwa kuharibu kunakoharibu azuhuri, elfu moja wataanguka kando yako, na elfu kumi kwa mukono

wako wa kuume; lakini hakutafika karibu nawe. Na macho yako tu utatazama, na kuona zawabu ya waovu. Maana wewe, ee Bwana, ni pahali pangu pa kukimbilia! Umejanya aliye juu kao lako; Mabaya hayatakupata wewe wala tauni haitafika na hema yako. Maana ataagiza malaika yake juu yako, wakuchunge katika njia zako zote. Watakuchukua juu mikononi mwao, usivunje muguu wako kwa jiwe. Utakanyaga simba na nyoka mudogo mwenye sumu, utakanyaga mwana-simba na joka. Kwa sababu ametia mapendo yake juu yangu, kwa hivi nitamuponyesha. Nitamuweka juu kwa sababu amejua jina langu. Ataniita na nitamujibu; nitakuwa pamoja naye katika taabu; nitamuponyesha na kumuheshimu. Kwa maisha ndefu nitamushibisha, na kumwonyesha wokovu wangu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Allilulia, allilulia, allilulia, utukufu kwako, ee Mungu. (*mara tatu*), Bwana hurumia (*mara tatu*).

Kisha tunasoma hii mwimbo:

Utukufu kwa Baba. . .

Zamani Maria mwenye kuchukua tunda isiyopandwa akajiandikisha kule Bethlehemu pamoja na mtukufu Yosefu wa kizazi cha Daudi. Wakati wa kuzaa ilitimia na hakukuwa fasi katika nyumba ya wageni; lakini kwa Malkia pango ikawa nyumba safi: Kristu anakuja duniani kuinua sura yake iliyoanguka.

Sasa na siku zote. . . Theotokion.

Kwani hatuna matumaini hata moja sababu ya zambi zetu nyingi, umwombe huyu aliyezaliwa kwako, ee Bikira Mzazi-Mungu. Maana ni la nguvu, ombi la Mama kwa kupata neema ya Rabi. Usizarau maombi ya wenye zambi, ewe Mtukufu kamili, kwa kuwa yeye ni mwenye rehema na Mweza kwa kuokoa, huyu aliyekubali kuteswa mwilini kwa ajili yetu.

Kisha tunaimba hii wimbo: (idiomela)

Sauti wa kwanza.

Kujeni, enyi waaminifu, tuinue roho zetu kwa Mungu na tuona tangu mbinguni kushuka kwake akija kwetu sababu ya kuonekana katika mji wa Bethlehemu; kwa uzima wetu tutolee fazila zetu pahali pa manemane, tutayarische na imani hii siku kuu ya Noeli yenye kutufungulia hazina zake za roho; na tuimbeni: Utukufu kwa Mungu katika Utatu Mtakatifu juu mbinguni, amani imeonekana duniani kwa wanadamu, kwani kwa mapendo yake kwa wanadamu amewaokoa toka laana ya wababu.

Mara ingine tunaimba hii, bila shairi.

Shairi: Mungu alikuja toka Temani, na Mutakatifu toka mulima wa kivuli.

Sauti wa ine.

Ee mbingu, sikia sauti yangu, ee inchi, tega sikio, misingi yako yatikisike, gehena iogope, maana Mungu Muumba amevaa mwili, na huyu mkono wa uwezo iliumba ameonekana katika kifua cha Muumba wako. Hii ni fumbo kubwa ya hekima na ya maarifa ya Mungu. Haki zake ni isiyoweza kufasiriwa.

Shairi: Ee Bwana nimesikia sauti yako, nimejaa na woga.

Tunaimba hii wimbo mara ingine.

Utukufu kwa Baba. . . Sauti ya tano.

Kujeni, enyi wakristu, tuone maajabu ya kushangaa; tuiimbie na imani, tusujudu na heshima. Leo Bikira amefika kule Bethlehemu sababu ya kuzaa Bwana anachukua tumboni mwake, Malaika wanamutangulia na nyimbo. Kwa kuona hivi, Yosefu mchumba wake anauliza: Ee Bikira, ni fumbo gani hii ya kushangaa ninaona kwako, namna gani Mwana-kondoo jike asiyeolewa anajitayarisha kwa kuzaa?

Sasa na siku zote. . . *Mara ingine hii wimbo.*

Prokimenon ya Unabii:

Kwa uzuri wa utakatifu, toka tumbo la asubui, wewe una umande wa ujana wako.

Shairi: Bwana anamwambia Bwana yangu: Uketi kwa mukono wangu wa kuume.

Somo ya Unabii ya Nabii Isaya, tutasoma.

Na Bwana akasema na Ahazi tena, akisema: Ujionbee alama kwake Bwana Mungu wako; omba kwayo katika pahali pa chini, ao katika pahali pa juu. Na Ahazi akasema: Sitaomba; na sitajaribu Bwana. Na akasema: Sikieni basi, nyumba ya Daudi: ni neno dogo kwenu kuchokesha watu, hata munachokesha Mungu wangu vilevile? Kwa sababu hii Bwana mwenyewe atawapa ninyi alama: Tazama, bikira atapata mimba naye atazaa mutoto mwanamume, na ataita jina lake EmanueJi. Atakula siagi na asali, ajue kukataa maovu, na kuchagua mema. Kwa maana mbele mutoto hajajua bado kukataa mabaya na kachagua mema, inchi ile itaachwa, nao wafalme wake wawili unaowachukia. Bwana ataleta juu yako, na juu ya watu wako, na juu ya nyumba ya baba yako, siku zisizokuja bado tangu siku ile Efuraimu aliyoo-ndoka toka Yuda hata mufalme wa Asuria. Mungu yuko pamoja nasi; yueni, ee ninyi mataifa, na kushindwa. Tegeni masikio, ninyi yote, mulio mpaka mwisho wa inchi. Mulio na nguvu sana mutashindwa. Mukipata nguvu tena, mutashindwa tena. Mukifanya shauri pamoja, litabatilika. Mukisema neno, halitasimama kwenu. Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Matendo ya Mitume.

Barua ya Mtume Paulo kwa wa Ebrania, tutasoma.

Na tena: Wewe Bwana, katika mwanzo umeweka misingi ya inchi, na mbingu ni kazi za mikono yako. Hizi zitaharibika, lakini wewe unabaki; na hizi zote zitachakaa kama nguo, na kama mavazi utazikunja, nazo zitabadilika; lakini wewe ni sawasawa saa zote, na miaka yako haitakoma. Lakini kwa malaika gani amekwsiha kusema hata mara moja: Uketi kwa mukono wangu wa kuume hata nitakapoweka adui zako chini ya miguu yako? hawa wote si roho za kutumikia, waliotumwa kutumikia wale watakaoriti wokovu? Kwa sababu ile imetupasa kuangalia zaidi maneno tuliyoyasikia tusije tukayaacha kuponyoka. Kwa maana ikiwa lile neno lililosemwa na malaika lilisimama na nguvu, na kila kosa na uasi ulipata azabu ya haki; basi sisi tutapona namna gani tusipochunga wokovu mukubwa

namna hii? Uliokuwa kwanza kusemwa na Bwana, kisha ukasibitika kwetu na wale waliomusikia;

EVANGELIO

Hekima; Inukeni tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.

Msomaji: Na kwa roho yako.

Somo ya Evangelio Takatifu ilionandikwa na Mwevangelizaji Matayo, tusikilize.

Msomaji: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

Padri:

Wakati Yesu alipozaliwa katika Betelehemu ya Yudea siku za mufalme Herode, tazama, waakili wa mashariki walifika Yerusalema, wakisema: Yuko wapi yeye aliyezaliwa Mufalme wa Wayuda? Kwa sababu tuliona nyota yake katika mashariki, nasi tumekuja kumwabudu. Wakati mufalme Herode aliposikia maneno haya, alifazaika na Yerusalema pia pamoja naye. Alikusanya wakubwa wa makuhani wote na waandishi wa watu, akawauliza pahali Kristu atakapozaliwa. Nao wakamwambia: Katika Betelehemu ya Yudea; kwa maana ndivyo ilivyoandikwa na nabii: Nawe Betelehemu, inchi ya Yuda, wewe si mudogo sana katikati ya wakubwa wa Yuda: Kwa sababu kwako atatoka mutawala, atakayechunga watu wangu Israeli.

Kisha Msomaji anasoma:

Huruma yako itufikie upesi, kwani tumetaabika sana. Utusaidie, ee Mungu Mwokozi wetu, kwa ajili ya utukufu wa jina lako. Utuokoe, utusamehe zambi zetu kwa ajili ya jina lako.

Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

Kisha tunasoma Kontakion:

Leo Bikira anajitayarisha kwa kuzaa katika pango Neno wa mbele ya nyakati. Ewe dunia yote kwa hii habari imba na kucheza, tukuza pamoja na Malaika na Wachungaji huyu alitaka kuwa mwana mchanga, yeye aliye Mungu wa mbele ya nyakati.

Kisha tunasema: Bwana hurumia, (mara makumi ine) na hii sala: Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa. . . (Ona ukurasa 5).

Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia. Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . . Uliye wadamani. . . Kwa jina la Bwana barikia, ee padri:

Mungu atufazili na kutubariki, atuangazie uso wake na kutuhurumia.

Padri atasoma hii sala ya Mtakatifu Basile Mukubwa.

Ee Mungu na Bwana wa majeshi, fundi wa kiumbe yote, kwa mapendo ya rehema yako isiyoweza kufananishwa, ulimtuma Mwana wako wa pekee, Bwana wetu Yesu Kristu, kwa ajili ya wokovu wa wanadamu. Ulizima ile barua ya deni zetu, kwa msalaba wake tukufu na ulishinda, katika hii, ufalme na nguvu za giza. Wewe mwenyewe, ee Rabi, mpenda-wanadamu, utupokee sisi wenye zambi; pokea shukrani zetu na maombi yetu. Utuopoe ku kosa yote yenye kuzuru na ya giza na kwa wale wote wenyi kutafuta

kutuzuru, maadui wenye kuonekana na wasioonekana. Toboa mwili wetu na woga wako, usiinamishe mioyo yetu ku maneno wala ku mawazo mabaya, lakini umiza mioyo yetu ku mapendo yako ili wakati wote macho yenye kukaza kwako, na tukiongozwa na nuru isiyokaribika na ya milele, na kukutolea utukufu na shukrani, Baba wasipo mwanzo, pamoja na Mwana wako wa pekee na Roho wako Mtakatifu kamili, mwema na mletaji uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SAA WA TISA

Msomaji mara moja anasoma:

Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . . Bwana hurumia (*mara kumi na mbili*), Njooi tumwinamia. . .

Kisha anasoma hii ma zaburi:

Zaburi 109 (110)

Bwana anamwambia Bwana yangu: Uketi kwa mukono wangu wa kuume, hata kifanye adui zako kuwa kiti cha miguu yako. Bwana atanyosha fimbo ya nguvu yako toka Sayuni: Wewe tawala katikati ya adui zako. Watu wako wanajitoa kwa moyo siku ya uwezo wako: Kwa uzuri wa utakatifu, toka tumbo la asubui, wewe una umande wa ujana wako. Bwana ameapa naye hatageuka, wewe ni kuhani milele kwa namna ya Melkizedeki. Bwana kwa mukono wako wa kuume Atapiga wafalme kwa siku ya gazabu yake. Atahukumu katikati ya mataifa, atajaza inchi na maiti; atapiga kichwa katika inchi nyingi. Atakunywa maji ya muto njiani: Kwa hivi atanyanyua kichwa chake.

Zaburi 110 (111)

Musifu Bwana. Nitashukuru Bwana kwa moyo wangu wote, katika baraza ya wenye haki, na katika makutano. Kazi za Bwana ni kubwa zinatafutiwa sana nao wanaozifurahia. Kazi yake ni heshima na enzi: Na haki yake inakaa milele. Amefanya ukumbusho wa kazi zake za ajabu: Bwana ni mwenye neema, anajaa rehema. Amewapa chakula wale wanaomwogopa: Atakumbuka agano lake milele. Ameonyesha watu wake uwezo wa kazi zake kwa kuwapa uriti wa mataifa. Kazi za mikono yake ni kweli na hukumu; Maagizo yake yote ni hakika. Yamesimamishwa milele na milele Y amefanywa katika kweli na haki. Ametumia watu wake wokovu. Ameamuru agano lake liwe kwa milele: Jina lake ni takatifu na la kustahili heshima. Woga wa Bwana ni mwanzo wa akili: Na wote wanaofanya hivi wana akili njema: Sifa yake inakaa milele.

Zaburi 85 (86)

Uiname sikio lako, Ee Bwana, unijibu; Maana mimi ni masikini na mwenye hitaji. Chunga nafsi yangu maana mimi ni mwema; ee wewe Mungu wangu, ponyesha mutumishi wako anayekutumainia. Unirehemu, ee Bwana; Maana kwako ninalia muchana kutwa. Furahisha nafsi ya mutumishi wako; maana kwako, ee Bwana,

ninanyanyua nafsi yangu. Kwani wewe, Bwana, ni mwema, na tayari kusamehe, Ukijaa rehema kwa wote wanaokuomba. Sikia, ee Bwana, maombi yangu; na sikiliza sauti ya kuomba kwangu. Kwa siku ya taabu yangu nitaomba kwako, Kwani utanijibu: Hakuna mwingine katika miungu kama wewe, ee Bwana, wala hakuna kazi kama kazi zako. Mataifa yote uliyofanya watakuja na kuabudu mbele yako, ee Bwana; na watatukuza jina lako. Kwa kuwa wewe ni mukubwa, na unafanya maajabu; wewe pekee ni Mungu. Unifundishe njia yako, Ee Bwana; nitatembea katika kweli yako; ufunganishe moyo wangu kuogopa jina lako. Nitakusifu, ee Bwana Mungu wangu, na moyo wangu wote, na nitatukuza jina lako kwa milele. Maana rehema yako ni kubwa kwangu, na umeponyesha nafsi yangu toka Hadeze ya chini kabisa. Ee Mungu, wenye majivuno wamesimama juu yangu, Na makutano ya wenye jeuri wametafuta nafsi yangu, wala hawakukuweka wewe mbele yao. Lakini wewe, ee Bwana, ni Mungu anayejaa huruma na neema, Muvumilivu, mwenye rehema na kweli nyingi. Ugeuke kwangu na kunirehemu; umupe mutumishi wako nguvu yako, na kuponyesha mwana wa kijakazi chako. Unionyeshe alama kwa wema; Hata wao wanaonichukia wapate kuiona na kuhayarishwa, kwa kuwa wewe, Bwana, umenisaidia, na kunifariji.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Allilulia, allilulia, allilulia, utukufu kwako, ee Mungu. (*mara tatu*), Bwana hurumia (*mara tatu*).

Kisha tunasoma hii mwimbo:

Utukufu kwa Baba. . .

Zamani Maria mwenye kuchukua tunda isiyopandwa akajiandikisha kule Bethlehemu pamoja na mtukufu Yosefu wa kizazi cha Daudi. Wakati wa kuzaa ilitimia na hakukuwa fasi katika nyumba ya wageni; lakini kwa Malkia pango ikawa nyumba safi: Kristu anakuja duniani kuinua sura yake iliyoanguka.

Sasa na siku zote. . . Theotokion.

Wewe uliyezaliwa kwa Bikira kwa ajili yetu, na uliyevumilia usulubisho, ee Mwema, uliyenyaganya mauti kwa lufu, na uliyeonyesha usimamao sawasawa na Mungu, usikengue walioubwa kwa mukono wako; onyesha mapendo yako kwa wanadamu, murehemu; pokea Mzazi-Mungu aliyekuzaa, aliyepatanisha juu yetu, na okoa, ee Mwokozi wetu, taifa isiyotumainia.

Kisha tunaimba hii wimbo:

Sauti ya saba.

Herodi alishangaa wakati aliona Wenye akili na imani yao; aliposirika, wakamujulisha tarehe na wingi wa miaka; Wamama walilia watoto wao maana waliuawa, maziwa yao yalikauka. Ilikuwa ni mateso kubwa. Kwa hivi, sisi waaminifu tunapokusanyika na ibada, tusujudie Kuzaliwa kwa Kristu.

Mara ingine hii, bila shairi.

Shairi: Mungu alikuja toka Temani, na Mutakatifu toka mulima wa kivuli.

Sauti wa mbili.

Ee Bikira wakati Yusefu aliposikitika sana wakati mulipopanda kwenda Yerusalema, ukamwambia: Sababu gani umesikitika na kushituka wakati unaona mimba yangu sawa haujui kabisa fumbo ya ajabu inafanyika kwa mimi? Usishangae sasa usiogope, maana Mungu atashuka duniani kwa kutaka kwake, sasa ametwaa mwili tumboni mwangu; kisha kuzaliwa kwake utamuona kama alivyotaka, na kwa furaha utasujudu mbele ya Muumba wako, huyu Malaika wanaimbia na kutukuza daima pamoja na Baba na Roho Mtakatifu.

Shairi: Ee Bwana nimesikia sauti yako, nimejaa na woga.

Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Sauti ya sita

Hii wimbo musomaji ataisoma kati ya Kanisa na kisha kundi ya waimbaji wataimba pamoja mu fasi yao.

Leo amezaliwa kwa Bikira huyu mwenye kushika viumbe vyote mkononi mwake;(mara tatu).

Duniani amefunikwa vitambaa huyu Mungu msiyetikilika;

Huyu aliyesabitisha mbingu kwa mwanzo wa nyakati amelala katika sanduku la kulishia nyama;

Yeye aliyewapa watu wake jangwani mkate toka mbingu amelishwa kwa maziwa; Amewaita Wenye akili, yeye Mchumba wa Eklezija;

Anapokea zawadi zao, yeye Mwana wa Bikira.

Ee Kristu, tunasujudia kuzaliwa Kwako. (mara tatu).

Utunyesheshe kufunuliwa kwako kimungu.

Prokimenon ya Unabii *Sauti ya ine*

Ndiyo, itasemwa juu ya Sayuni: Huyu na huyu alizaliwa ndani yake.

Shairi: Musingi wake ni katika milima mitakatifu. .

Unabii ya Nabii Isaya tutasoma. (9, 6-7).

Maana kwa ajili yetu mutoto amezaliwa, tumepewa mutoto utakuwa juu ya bega lake: Na jina lake litaitwa Mwenye ajabu, Mwenye shauri, Mungu Mwenye uwezo, Baba ya milele, mukubwa wa salama. Kuongezwa kwa utawala wake na salama hakutakuwa na mwisho, juu ya kiti cha ufalme cha Daudi, na juu ya ufalme wake, kuusimamisha, na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele. Wivu wa Bwana wa majeshi utafanya maneno haya.

Matendo ya Mitume.

Barua ya Mtume Paulo kwa wa Ebrania, tutasoma.

Wa Ndugu, maana mwenye kutakasa, nao wenye kutakaswa wote pia wanataka kwa mumoja. Kwa sababu hii haoni haya kuwaita ndugu zake, akisema: Nitahubiri jina lako kwa ndugu zangu; katikati ya kanisa nitakuambia sifa. Na tena: Nitaweka imani yangu ndani yake. Na tena: Tazama, mimi pamoja na watoto niliopewa na Mungu. Basi, kwa sababu watoto wameshiriki damu na mwili, yeye mwenyewe vivyo hivyo alishiriki kama

wao, hata kwa njia ya kufa apate kuharibu yeye aliyekuwa na nguvu za kufa, ndiye Shetani, na kuwafungua wale wote waliokuwa maisha yao yote katika hali ya utumwa, kwa woga wa mauti. Maana ni hakika, hatwai asili ya malaika, lakini anatwaa asili ya mazao ya Abrahamu. Kwa hivyo ilimupasa kufananishwa na ndugu zake katika maneno yote, apate kuwa kuhani mukubwa mwenye rehema na mwaminifu katika mambo ya Mungu kusudi afanye upatanisho kwa zambi za watu. Na kwa kuwa yeye mwenyewe aliteswa wakati alipojaribiwa, anaweza kusaidia wale wanaojaribiwa.

EVANGELIO

Hekima; Inukeni tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.

Msomaji: Na kwa roho yako.

Somo ya Evangelio Takatifu ilionandikwa na Mwevangelizaji Matayo, tusikilize.

Msomaji: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

Padri:

Na wakati walipokwisha kwenda zao, tazama, malaika ya Bwana alitokea Yusefu katika ndoto, akisema: Ondoka, uchukue mutoto na mama yake, ukimbilie Misri, ukae kule hata nitakapokuambia; sababu Herode atatafuta mutoto amuharibishe. Akaamka, akachukua mutoto na mama yake usiku, akakwenda zake hata Misri; akakaa kule hata alipokufa Herode: Ili litimie neno lililosemwa na Bwana kwa nabii, akisema: Toka Misri niliita mwana wangu. Halafu Herode, akiona na kuwa alizihakiwa na waakili, alikasirika sana, akatuma watu, akaua watoto wanaume wote waliokuwa Betelehemu na mipaka yake yote, toka miaka miwili na kidogo kupita, kama wakati aliohakikishwa na waakili. Halafu neno lilitimia lililosemwa na nabii Yeria, akisema: Sauti ilisikiwa katika Rama, kilio na maombolezo mengi, Rakeli akililia watoto wake, asitake kufarijiwa, kwa sababu hawako.

Kisha msomaji anasoma:

Usituache mpaka mwisho, sababu ya jina lako takatifu, usiharibu agano lako, na usitenge kwa sisi rehema yako, sababu ya Abrahamu mpendwa wako, na Isaaka mtumishi wako na Israeli mtakatifu wako.

Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

Kisha tunasoma Kontakion:

Leo Bikira anajitayarisha kwa kuzaa katika pango Neno wa mbele ya nyakati. Ewe dunia yote kwa hii habari imba na kucheza, tukuza pamoja na Malaika na Wachungaji huyu alitaka kuwa mwana mchanga, yeye aliye Mungu wa mbele ya nyakati.

Kisha tunasema: Bwana hurumia, (mara makumi ine) na hii sala: Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa. . . (Ona ukurasa 5).

Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia. Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . . Uliye wadamani. . . Kwa jina la Bwana barikia, ee padri:

Padri: Mungu atufazili na kutubariki, atuangazie uso wake na kutuhurumia.

Padri atasoma hii sala ya Mtakatifu Basile Mukubwa.

Ee Rabi na Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, mpole kwa kukasirika juu ya makosa yetu, unatufikisha mpaka hii wakati ambako ulipotundikwa juu ya msalaba wenyi kuleta uzima, ukamufungulia munyanganyi mlango ya paradizo na ukavunja mauti kwa lufu. Utuhurumie pia na sisi watumishi wako wasiostahili tena waovu; maana tulitenda zambi na hatustahili kunyanyua macho kwa kutazama mbinguni. Ndiyo, tuliacha njia ya haki, tulitembea kama ilivyopenda roho yetu. Lakini tunaomba wema wako: Utusamehe, ee Bwana, kadiri ya rehema yako kubwa na utuokoe kwa ajili ya jina lako takatifu, kwani tulijivuna katika maisha yetu. Utuondoe toka mkono ya adui, zima zambi zetu, regeza mawazo yetu ya mwili; hivi, tukiondoa mutu wa zamani, tutavaa mutu mupya, na tutaishi juu Yako wewe Rabi na Muombezi wetu; halafu, kwa kanuni zako, tutafika kwa mapumziko ya milele, kwa makao ya wenye heri wote. Kwani ni Wewe heri ya kweli tena furaha ya wale wenye kukupenda, ee Kristu Mungu wetu, na tunakutolea utukufu, pamoja na Baba yako asiye na mwanzo, na Roho wako Mtakatifu kamili, mwema na mletaji-uzima, daima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Kisha tunasoma **TIPIKA:**

Umsifu Bwana, ee roho yangu, na yote yaliyo ndani yangu yasifu jina lake Takatifu. Umsifu Bwana, ee roho yangu, wala usisahau mema yake yote! Yeye anasamehe zambi zako zote, anaponyesha magonjwa yako yote. Yeye anakomboa uzima wako katika kaburi, anayekutia taji ya huruma na rehema. Yeye anashibisha mema maisha yako, na ujana wako unarudishwa upya kama wa tai. Bwana anatenda wa huruma, anawahukumu sawa wote wanaoteswa. Alimujilisha Musa njia zake, wana wa Israeli mapenzi yake. Bwana na mwenye huruma na mpole, mvumilivu, mwenye mema mingi. Haendelei daima kukaripia, wala hatavhunga hasira yake milele. Hakututendia kadiri ya zambi zetu, wala hakutulipa sawasawa na makosa yetu. Kama vile mbingu ziinuka juu ya inchi, hivyo Bwana alizidisha kwa wenye wakumwogopa. Kama mashariki ilivyo mbali na magari, hivyo na zambi zetu ameziweka mbali nasi. Kama vile baba anavyowahurumia watoto wake, hivyo Bwana anawahurumkia watu wanamwogopa, maana anajua tumeumbwa kwa kitu gani, anakumbuka ya kama sisi ni mavumbi. Siku za mutu ni sawa na majani, anachanua kama ua la shamba. Upepo ukiisha pita juu yake, hayupo, wala pahali pake hapaonekani tena. Lakini huruma ya Bwana inadumu tangu milele hata milele kwa wenye kumwogopa. Na haki yake kwa wana wa wana wao, kwa wale wanaoshika agano lake, wanaokumbuka amri zake wazitimize. Bwana amesimika kiti chake mbinguni, na ufalme wake unatawala vitu vyote. Msifuni Bwana, enyi Malaika wake wote, mlio na nguvu nyingi, mnaotimiza neno laki, mnaposikia sauti ya neno lake. Msifuni Bwana, enyi majeshi yake yote, watumishi wake mnaotimiza mapenzi yake.

Msifuni Bwana, enyi matendo yake yote, pahali pote pa ufalme wake. Umsifu Bwana, ee roho yangu!

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mutakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina. Umsifu, Bwana, ee roho yangu, na yote yaliyo ndani yangu yasifu jina lake takatifu. Muhimidiwe, ee Bwana.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu.

Umsifu Bwana, ee roho yangu, nitamusifu Bwana maisha yangu yote, nitamwambia Mungu wangu zaburi mimi ningali mzima. Msiwatumainie wakubwa wa dunia, wala mwanadamu asiyeweza kuokoa. Atatoa roho yake, anarudia udongo wake. Siku ile

mafikili yake yote yanapotea. Heri mtu anayesaidiwa na Mungu wa Yakobo, anayemtumainia Bwana, Mungu wake. Aliyeumba mbingu na dunia, bahari na vyote vilivyomo. Anayeshika kweli wake hata milele. Anawarudishia haki waliozulumiwa, anawapa wenye njaa chakula. Bwana anawafungwa wafungwa, Bwana anafungua macho ya vipofu. Bwana anawanyanyua walioinama. Bwana anawapenda wenye haki, Bwana anachunga wageni. Anawatunza yatima na mjane, anapindua njia ya waovu. Bwana atatawala milele, Mungu wako, ee Sayuni, kizazi hata kizazi.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Uliye Mwana wa pekee tena Neno wa Mungu, ukiwa msiyekufa ukakubali kwa ajili ya wokovu wetu kupata mwili kwa Maria Mzazi-Mungu, tena Bikira daima, ukawa mtu bila kujigeuza; hata kusulubiwa, ewe Kristu Mungu, na kukikanyanga kifo kwa kifo; ukiwa mumoja na Utatu Mtakatifu, na kutukuzwa pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, utuokoe.

HERI

Katika ufalme wako, utukumbuke, ee Bwana, utakapokuja katika ufalme wako. Heri walio masikini wa roho, maana Ufalme wa mbinguni ni wao.

Heri wenye huzuni: maana wao watafarijiwa.

Heri wenye upole: maana wao watariti inchi.

Heri wenye njaa na kiu haki: maana wao watashibishwa.

Heri wenye rehema: maana wao watapata rehema.

Heri wenye moyo safi: maana wao wataona MUngu.

Heri wenye kufanya salama: maana wataitwa wana wa Mungu.

Heri walioteswa kwa sababu ya haki: maana ufalme wa mbinguni ni wao.

Heri ninyi, wakati wanapowatukana ninyi na kuwatesa ninyi nakuwasemea ninyi kila neno baya kwa uwongo, kwa sababu yangu.

Furahini, shangilieni; kwa sababu zawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyotesa manabii waliokuwa mbele yenu.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mutakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Utukumbuke, ee Bwana, wakati utakapokuja katika ufalme wako.

Utukumbuke, ee Rabi, wakati utakapokuja katika ufalme wako.

Utukumbuke, ee Mtakatifu, wakati utakapokuja katika ufalme wako.

Kundi la waimbaji wa mbinguni wanakuimbia na wanasema: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Savaothi, mbingu na dunia zimejaa na utukufu wako.

Njongeni kwake, na mutaangaziwa na uso wetu usipate haya.

Kundi la waimbaji wa mbinguni wanakuimbia na wanasema: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Savaothi, mbingu na dunia zimejaa na utukufu wako.

Utukufu kwa Baba. . .

Kundi la malaika na malaika Wakuu, pamoja na majeshi ya mbinguni wanakuambia na waanasema: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Savaothi, mbingu na dunia zimejaa utukufu wako.

Sasa na siku zote. . .

Tunasoma Simvolo ya Imani: Nasadiki Mungu moja. . .

Kisha tunasoma:

Zima, ashilia, hurumia, ee Mungu, makosa yetu ya kutaka na yisiyokutaka, iliyofanyika kwa matendo na maneno, ya kujuwa na ya kutokujuwa ya usiku ao ya mchana, ndani ya akili na ya ufahamu; yote utuhurumie, sawa mwema na mpenda wanadamu.

Baba yetu uliye mbinguni. . .

Kontakion:

Leo Bikira anajitayarisha kwa kuzaa katika pango Neno wa mbele ya nyakati. Ewe dunia yote kwa hii habari imba na kucheza, tukuza pamoja na Malaika na Wachungaji huyu alitaka kuwa mwana mchanga, yeye aliye Mungu wa mbele ya nyakati.

Kisha tunasema: Bwana hurumia, (mara kumi na mbili).

Jina la Bwana lihimidiwe tangu sasa, na mupaka milele (*mara tatu*). Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Tunasoma zaburi hii:

Zaburi 34 (35)

Nitabariki Bwana wakati wote; sifa yake itakuwa kinywani mwangu daima. Nafsi yangu itajisifu katika Bwana; Wapole watasikia na watafurahi. Musifu Bwana pamoja nami, na tutukuze jina lake pamoja. Nilitafuta Bwana, naye alinijibu, na kuniponyesha toka woga zangu zote. Wakamutazama, na walitiwa nuru; Na nyuso zao hazitaona haya milele. Masikini huyu akalia, Bwana akamusikia, akamwokoza toka taabu zake zote. Malaika ya Bwana anapiga kambi kuzunguka wale wanaomwogopa, na anawaokoza. Onjeni mwone ya kuwa Bwana ni Mwema; Heri mutu anayemuwekea tumaini lake. Ogopeni Bwana, ninyi watakatifu wake; Kwa sababu wale wanaomwogopa hawahitaji kitu. Wana-simba wanahitaji, wanaona njaa; Lakini wao wanaotafuta Bwana hawatakosa kitu cho chote kilicho chema. Njooi, ninyi watoto, munisikilize; nitawafundisha ninyi woga wa Bwana. Ni nani mutu yule anayetaka uzima, na anayependa siku nyingi ili apate kuona mema? Uzuize ulimi wako na ubaya, na midomo yako na kusema hila. Uache mabaya ukatende mema; Tafuta salama, na kuifuata. Macho ya Bwana yanatazama wenye haki, na masikio yake ni wazi kwa kusikia kilio chao. Uso wa Bwana ni juu yao wanaotenda mabaya, aondoshe ukumbusho wao duniani. Wenye haki walilia, na Bwana alisikia, na kuwaponyesha toka taabu zao zote. Bwana ni karibu na wenye moyo wa kuvunjika, na anaokoza wenye roho ya toba. Mateso ya mwenye haki ni mengi; Lakini Bwana anamuponyesha nayo yote. Anachunga mifupa yake yote; haukuvunjika hata mumoja. Uovu utawa mwovu; nao wanaochukia wenye haki watahukumiwa. Bwana anakomboa nafsi ya watumishi wake; wala hawatahukumiwa wote wanaomuwekea yeye kimbilio lao.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Bwana hurumia (*mara tatu*), Rabi mtakatifu barikia.

Padri:

Kristu Mungu wetu ukweli, kwa maombezi ya Mama wake Mtakatifu asiye na doa wala si lawama kamili; ya Mitume Watakatifu watukufu, wasifiwa kamili na ya watakatifu wote, atuhurumie na atuokoe, kwani ni Mwema na mupenda-wanadamu.

Kwa maombezi ya wapadri watakatifu wetu, ee Bwana Yesu kristu, Mungu wetu, utuhurumie. Amina.

SALA YA SAA MAKUBWA YA EPIFANIA YA BWANA YESU KRISTU

SAA WA KWANZA

Padri: Abarikiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote hata milele na milele.

Msomaji: Amina. Mungu Mtakatifu, Mweza Mtakatifu, Musiye kufa Mtakatifu, utuhurumie. (*mara tatu*). Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasana siku zote, hata milele na milele. Amina.

Utatu Mtakatifu Kamili utuhurumie, Bwana utusamehe zambi zetu, Rabi utuondolee makosa yetu, mtakatifu utukaribie na uponye magonjwa yetu. Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama mbinguni, utupe sisi leo chakula chetu cha kila siku, utusamehe ndeni zetu kama sisi vilevile tunawasamehe walio na ndeni zetu, tena usitutie katika majaribu, lakini utuokoe na yule Mwovu

Padri: Kwa kuwa Ufalme, na uwezo, na utukufu ni kwako, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hasa milele na milele.

Msomaji: Amina. Bwana hurumia (*mara kumi na mbili*).

Njooi tumwinamie na tumsujudu Mungu na Mfalme wetu.

Njooi tumwinamie na tumsujudu Kristu Mfalme wetu.

Njooi tumwinamie na tumsujudu Yeye Kristu aliye Mfalme wetu.

Zaburi 5(6)

Sikiliza maneno yangu, ee Bwana, Uangalie mafikili yangu. Usikie sauti ya kilio changu, Mufalme wangu, na Mungu wangu: Kwa maana ninaomba kwako. Ee Bwana, asubui utasikia sauti yangu; asubui nitatengeneza maombi yangu kwako, na kuangalia sana. Kwa maana wewe si Mungu anayependezwa na uovu; mwovu hatakaa kwako. Wenye majivuno hawatasimama mbele ya macho yako; unachukia watenda wote wa uovu. Utaharibu wale wanaosema uwongo; Bwana anachukia mwuaji na mwenye hila. Lakini mimi, kwa wingi wa wema wako nitaingia nyumbani mwako; katika kukuogopa wewe nitaabudu kwa upande wa hekalu lako takatifu. Uniongoze, ee Bwana, kwa haki yako kwa sababu ya adui zangu; unifanyie njia yako wazi mbele ya uso wangu. Kwa maana hapana uaminifu kinywani mwao; mutima wao ni shimo tupu; koo lao ni kaburi wazi; wanabembeleza na ulimi wao. Uwahasabie zambi zao, ee Mungu; Waanguke kwa

mashauri yao wenyewe; uwatoe inje katika wingi wa makosa yao, kwa maana wamekuasi wewe. Lakini wote wanaokuwekea tumaini lao wafurahi, wapige kelele daima kwa furaha kwa sababu unawasimamia; wao vilevile wanaopenda jina lako wafurahi ndani yako. Kwa maana utabariki mwenye haki; ee Bwana, utamuzungusha na mapendeleo kama ngabo.

Zaburi 22 (23).

Bwana ni mchungaji wangu; sitapungukiwa na kitu. Ananilisha katika malisho ya majani mabichi; ananiongoza kando ya maji matulivu. Anarudisha nafsi yangu; ananiongoza katika njia za haki kwa ajili ya jina lake. Ndiyo, hata nikipita kati ya bonde la kivuli cha mauti, sitaogopa mabaya; kwa maana wewe ni pamoja nami; Gongo lako na fimbo yako zinanifariji. Unanitengenezea meza mbele ya adui zangu; umenipakalia mafuta kichwani; kikombe changu kinafurika. Hakika wema na rehema zitanifuata siku zote za maisha yangu; na nitakaa nyumbani mwa Bwana milele.

Zaburi 26 (27).

Bwana ni nuru yangu na wokovu wangu; Nitaogopa nani? Bwana ni nguvu ya uzima wangu, Nitakuwa na woga kwa sababu ya nani? Wakati watenda mabaya walipofika karibu nami kwa kula nyama yangu, hata watesi wangu na adui zangu walikwaa na walianguka. Kama jeshi likipanga juu yangu, moyo wangu hautaogopa. kama vita ikitokea juu yangu, hata hivi nitakaa na imani. Kitu kimoja niliomba na Bwana, ndicho nitakachotafuta, nikae nyumbani mwa Bwana siku zote za maisha yangu, Nitazame uzuri wa Bwana, nikauliza kwa hekalu lake. Kwani kwa siku ya taabu atanificha kwa kibanda chake, atanificha kwa maficho ya hema yake, atanipandisha juu mwambani. Na leo kichwa changu kitapandishwa juu kuliko adui zangu wanaonizunguka, na nitatoa zabihu za furaha hemani mwake, nitaimba, ndiyo, nitaimba zaburi kwa Bwana! Usikie, Bwana; na sauti yangu ninalia, unirehemu ukanijibu. Wakati uliposema: Tafuteni uso wangu, moyo wangu ukakuambia: Uso wako, Ee Bwana, nitautafuta. Usinifichie uso wako, Usiondoe mutumwa wako na kasirani. Umekuwa musaidia wangu, usinitupe wala kuniacha, ee Mungu wa wokovu wangu. Maana baba yangu na mama yangu waliniacha, Lakini Bwana atanikaribisha. Unifundishe njia yako, Bwana, Uniongoze kwa mapito sawa kwa sababu ya adui zangu. Usinitoe kwa mapenzi ya adui zangu, kwa sababu washuhuda wa uwongo wamesimama juu yangu, Na wenye kutoa ukali. Kama singeamini ya kuwa wema wa Bwana, kwa inchi ya wahai! Ungojee Bwana, uwe hodari, moyo wako upate nguvu. Ndiyo, ungojee Bwana.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Allilulia, allilulia, allilulia, utukufu kwako, ee Mungu. (*mara tatu*), Bwana hurumia (*mara tatu*).

Kisha tunasoma hii mwimbo:

Utukufu kwa Baba. . .

Zamani Yordani ilirudi nyuma, wakati Eliseo alipigapo nguo yako, na maji yaligawanyika kisha kutwaliwa kwa Elia mbinguni; mawimbi yakawa kwake njia kavu kwa mfano wa

Ubatizo tunakovuka mtoni wa hii uzima yenyi kututikisa. . Kristu anaonekana katika Yordani sababu ya kutakasa maji.

Sasa na siku zote. . . Theotokion.

Namuna gani tutakuita ewe Mujaliwa neema? Kwa sababu ulileta duniani jua ya haki. Paradizo? Kwa sababu uliotesha ua isiyo harabika. Kwa sababu ulibaki Bikira bila uharibifu. Mama kamili? Kwa sababu ulichukua katika kifua chako takatifu Mtoto, aliye Mungu wawote. Umuombe yeye aokoe mioyo yetu.

Kisha tunaimba hii wimbo na muziki ya kuachana (Idiomela).

Sauti ya mnane.

Leo hali ya maji inatakaswa; maji ya Yordani yanasimama na inasimamisha mawimbi yake mbele ya Rabi anaingiamo.

Mara ingine hii, bila shairi.

Shairi: Nitakumbuka wewe toka inchi ya Yordani na ya Hermoni.

Sauti ya mnane.

Unashuka katika mtoni, ee Kristu mfalme wetu, na unajiharikisha kupokea kwa ubinadamu wako ubatizo wa watumishi kwa mkono wa Mtangulizi sababu ya zambi zetu, ee mpenda-wanadamu tena Mungu wa wema.

Shairi: Maji yalikuona, ee Mungu; maji yakakuona, yakaogopa; vilindi vilevile vikatetemeka. (*Mara ingine tunaimba hii ya yulu*)

Utukufu kwa Baba. . . Sauti ya mnane

Kwa sauti inalia jangwani: Tengenezeni njia ya Bwana, ulikuja, ee Kristu, kama mtumishi, kuomba ubatizo, wewe peke yako usiye na zambi. Maji yalikuona na yakaogopa; Mtangulizi alipoogopa, akapaza sauti: Ni kwa kinara kuangaza Nuru? Ni kwa mtumwa kuwekea Bwana mkono? Unitakase mimi pamoja na maji, ee Mwokozi mwenye kuzima zambi ya dunia.

Sasa na siku zote. . . (Mara ingine hii).

Prokimenon ya Unabii

Mungu wa utukufu anapiga radi, Bwana ni juu ya maji mengi.

Shairi: Nitakupenda, ee Bwana katika nguvu yangu.

Unabii ya Nabii Isaya tutasoma. (35, 1-10)

Jangwa na inchi kavu zitafurahi; na jangwa litashangilia na kutoa maua kama waridi. Litatoa maua mengi, litashangilia hata na furaha na kuimba; litapewa utukufu wa Lebanoni, uzuri wa Karmeli na Saroni; wataona utukufu wa Bwana, enzi ya Mungu wetu. Mutie nguvu mikono iliyo zaifu, musimamisha magoti yaliyolegea. Muwaa- mbie walio na moyo wa woga: Mukae na nguvu, musiogope; tazama, Mungu wenu atakuja na kisasi, na malipo ya Mungu. Atakuja yeye mwenyewe na kuwaokoa ninyi. Ndipo macho ya vipofu yatafunguliwa, na masikio ya viziwi yatafunguliwa. Ndipo kiwete atarukaruka kama ayala, na ulimi wa bubu utaimba; maana katika jangwa maji yatabubujika; na mito jangwani. Na

muchanga unaongaa mufano wa maji utakuwa ziwa la maji, na inchi yenye kiu itakuwa chemchemi za maji; katika makao ya mbweha, pahali walipolala, patakuwa na majani, pamoja na matete na manyasi. Na njia kubwa itakuwa kule, na njia, nayo itaitwa njia ya utakatifu; wachafu hawatapita katikati yake; lakini itakuwa kwa ajili ya wale: wasafiri, hata wapumbavu, hawatapotea katika njia ile. Simba haitakuwa kule, wala nyama mukali hatapanda juu yake; hawataonekana kule; lakini waliokombolewa watatembea kule. Na wale waliokombolewa na Bwana watarudi na watafika Sayuni kwa kuimba; na furaha ya milele itakuwa juu ya vichwa vyao; watapata kucheka na furaha, na huzuni na kuugua zitakimbia.

Matendo ya Mitume tutasoma. (13, 25-32)

Naye Yoane, wakati alipomaliza mwendo wake alisema: Munazani mimi ni nani? Mimi siye. Lakini, tazameni, anakuja mumoja nyuma yangu nami sistahili kufungua viatu vya miguu yake. Wanaume, ndugu zangu, wa'na wa uzao wa Abrahamu, nanyi munaogopa Mungu, kwetu sisi neno la wokovu huu limetumwa. Lakini kwa sababu wale wanaokaa Yerusalema na wakubwa wao, hawakumuJua yeye, wala maneno ya manabii yanayosomwa kila sabato, wameyatimiza kwa kumuhukumu. Na hata hawakukuta neno lililofaa, kufa ndani yake, waliomba Pilato auawe. Nao wakati walipokwisha kutimiza yote yaliyoandikwa Juu yake, wakamushusha toka muti, wakamuweka kaburini. Lakini Mungu alimufufua toka wafu; akaonekana siku nyingi nao waliopanda pamoja naye toka Galilaya hata Yerusalema, walio sasa washuhuda wake mbele ya watu, Nasi tunawahubiri ninyi Habari Njema ya ahadi Ile waliyopewa baba zetu, ya kwamba.

EVANGELIO

Hekima; Inukeni tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.

Msomaji: Na kwa roho yako.

Somo ya Evangelio Takatifu ilionandikwa na Mwevangelizaji Matayo, tusikilize.

Msomaji: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

Padri:

Wakati ule Yesu akatoka Galilaya hata kufika Yorodani kwa Yoane abatizwe naye. Lakini Yoane alitaka kumuzuia, akisema: Mimi ninahitaji kubatizwa nawe, nawe unakuja kwangu? Yesu akajibu akamwambia: Kubali hivi sasa; sababu hivi imetupasa kutimiza haki yote. Basi akamukubali. Wakati Yesu alipobatizwa mara moja alitoka katika maji; na tazama, mbingu zikamufunguliwa, akaona Roho ya Mungu akishuka kama hua, akikuja juu yake; na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema: Huyu ni Mwana wangu, mupendwa wangu, ninapendezwa naye.

Kisha Msomaji atasoma: Ongoza mwendo wangu katika neno lako: Wala uovu wowote usinitawale.

Unikomoe na maneno ya mutu: Hivi nitachunga mafundisho yako yote.

Uangazie Mutumishi wako na uso wako; na unifundishe amri yako.

Kinyuwa changu kinajazwa na sifa yako Bwana, kama ninavyotukuza ziku zote uzuri wako.

Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

Kisha tunasoma Kontakion:

Sauti ya ine.

Aliposhuka leo katika maji ya Yordani Bwana akamwambia Yoane: Usiogope kunibatiza; nimekuja kuokoa Adamu Baba wa kwanza.

Kisha tunasema: Bwana hurumia, (mara makumi ine) na hii sala: Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa. . .(Ona ukurasa 5).

Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia. Utukufu kwa Baba. . .

Sasa na siku. . . Uliye wadamani. . . Kwa jina la Bwana barikia, ee padri:

Padri: Mungu atufazili na kutubariki, atuangazie uso wake na kutuhurumia.

Padri anasoma hii sala:

Kristu, nuru ya kweli, aliyeangaza na kutakasa kila mutu, anayekuja duniani, na imeonekana kwetu nuru ya uso wako, ulituonyesha nuru ya uso wako isio zimika na ongoza mwendo wetu katika kazi ya amri yako. Kwa maombi ya Mama wako Mtakatifu na ya watakatifu wote. Amina.

SAA WA TATU.

Msomaji mara moja anasoma: Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utukufu. . . Sasa. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . . Bwana hurumia (mara kumi na mbili), Njoooni tumwinamia. . .

Kisha tunasoma zaburi: 28 (29)

Mumupe Bwana ninyi wana wa wenye amri, Mumupe Bwana utukufu na nguvu; Mumupe Bwana utukufu wa kufaa jina lake, abuduni Bwana kwa uzuri mutakatifu. Sauti ya Bwana ni juu ya maji; Mungu wa utukufu anapiga radi, Bwana ni juu ya maji mcngi. Sauti ya Bwana ni yenye nguvu; Sauti ya Bwana inajaa ukubwa. Sauti ya Bwana inavunja micrezi, ndiyo Bwana anavunja rierezi ya Lebanoni. Anaifanyiza kurukaruka kama mwana-ngombe, Lebanoni na Sirioni, kama mwana-mbogo. Sauti ya Bwana inapasua ndimi za moto. Sauti ya Bwana inatetemeshwa jangwa, Bwana anatemeshwa jangwa la Kadesi. Sauti ya Bwana inazalisha paa Na inafunua mwitu; Na ndani ya hekalu lake kila kitu kinasema: Utukufu, Bwana anakaa juu ya garika, ndiyo, Bwana anakaa mufalme kwa milele. Bwana atawapa watu wake nguvu; Bwana atabariki watu wake kwa salama.

Zaburi 41 (42).

Kama ayala anavyotaka sana mito ya maji, vivyo hivyo nafsi yangu inakutaka wewe sana, ee Mungu. Nafsi yangu ina kiu kwa Mungu, kwa Mungu aliye hai; wakati gani nitakuja na kutokea mbele ya Mungu? Machozi yangu yamekuwa chakula changu muchana na usiku, wakati wanaponiambia muchana kutwa: Mungu wako ni wapi'? Maneno haya ninakumbuka, na kumwanga nafsi yangu ndani yangu, namna nilivyokwenda pamoja na makutano, na kuwaongoza kwa nyumba ya Mungu, na sauti ya furaha na sifa, makutano wakifanya siku kubwa. Kwa nini unainama, ee nafsi yangu? Na kwa nini unafazaika ndani yangu? Utumainie Mungu; kwa maana nitakuja kumusifu, kwa kusaidia kwa uso wake. Ee Mungu wangu, nafsi yangu imeinama ndani yangu; kwa hivi ninakukumbuka toka inchi ya Yorodani, na Mahermoni, toka kilima Misari. Kilindi kinaita kilindi kwa sauti ya nguzo zako za maji, Garika zako zote na mawimbi yako yote yamepita juu yangu. Muchana Bwana ataagiza wema wake, na usiku wimbo wake utakuwa pamoja nami, maombi kwa Mungu wa uzima wangu. Nitamwambia Mungu mwamba wangu: Kwa nini umenisahau? Kwa nini ninakwenda nikihuzunika kwa ajili ya mateso ya adui? Kama na upanga mifupani mwangu watesi wangu wanabilaumu; wakati wanaponiambia muchana kutwa: Mungu wako ni wapi? Kwa nini unainama, ee nafsi yangu? Na kwa nini unafazaika ndani yangu? Utumainie Mungu; kwa maana nitakuja kumusifu, kusaidia kwa uso wangu, na Mungu wangu.

Kisha Zaburi 50 (51):

Unirehemu, ee Mungu, sawasawa na wema wako, sawasawa na wingi wa rehema zako uzime makosa yangu. Unioshe kabisa na uovu wangu, na kunisafisha na zambi yangu. Maana ninajua makosa yangu, na zambi yangu ni mbele yangu daima. Nimekukosea wewe peke yako, na kufanya yaliyo mabaya machoni mwako, ili ujulikane kuwa mwenye haki wakati unaposema, na kuwa safi wakati unapotoa hukumu. Tazama, niliumbwa katika hali ya uovu, na katika makosa mama yangu alinichukua mimba. Tazama, wewe unataka kweli moyoni, na kwa siri utanijulisha hekima. Unisafishe kwa hisopo na nitakuwa safi, unioshe, na nitakuwa mweupe kupita theluji. Unifanye kusikia furaha na shangwe, ili mifupa uliyovunja ifurahi. Ufiche uso wako usitazame zambi zangu, na uzima maovu yangu yote. Umba moyo safi ndani yangu, ee Mungu, na ufanye upya roho nzuri ndani yangu. Usinitenge na uso wako, wala usiondolee Roho yako mutakatifu. Unirudishie furaha ya wokovu wako, unitegemeze kwa roho ya tayari. Halafu nitafundisha wenye makosa njia zako, na wenye zambi watarudi kwako. Uniponyeshe na damu ya watu, ee Mungu, wewe Mungu wa wokovu wangu, ulimi wangu utaimba na sauti haki yako. Ee Bwana, ufungue midomo yangu, na kinywa changu kitaonyesha sifa zako. Maana hupendezwi na zabihu, ao ningeitoa, hufurahi kwa sadaka ya kuteketezwa. Zabihu za Mungu ni roho ya kuvunjika, moyo uliovunjika na wa toba hutauzarau, ee Mungu. Utendee Sayuni mema kwa mapenzi yako, ujenge kuta za Yerusalema. Halafu utafurahi kwa zabihu za haki, kwa sadaka ya kuteketezwa, na sadaka nzima ya kuteketezwa, halafu watatoa ngombe ndume juu ya mazabahu yako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Allilulia, allilulia, allilulia, utukufu kwako, ee Mungu. (*mara tatu*), Bwana hurumia (*mara tatu*).

Kisha tunasoma hii mwimbo:

Utukufu kwa Baba. . .

Zamani Yordani ilirudi nyuma, wakati Eliseo alipigapo nguo yako, na maji yaligawanyika kisha kutwaliwa kwa Elia mbinguni; mawimbi yakawa kwake njia kavu kwa mfano wa Ubatizo tunakovuka mtoni wa hii uzima yenyi kututikisa. . Kristu anaonekana katika Yordani sababu ya kutakasa maji.

Sasa na siku zote. . . Theotokion.

Ee Mzazi-Mungu, ndiwe mzabibu wa kweli wenyi kuzidisha tunda la uzima. Tunakuomba: Utuombe, ee Malkia, pamoja na Mitume na Watakatifu wote, ili roho zetu zipate rehema.

Kisha tunaimba hii wimbo (Idiomela):

Sauti ya mnane.

Mkono ya Mbatizaji na Mtangulizi, ya Nabii mtukufu kupita Manabii wote wa zamani ilitetemeka wakati alikuona Wewe Mwana kondoo wa Mungu anayeondoa zambi ya dunia; akapaza sauti na sikitiko: Sitasubutu kukugusa, ee Neno; ni Wewe Bwana mwenye rehema unaweza kunitakasa, kuniangaza; wewe ni uzima, nuru na amani ya dunia.

Mara ingine hii, bila shairi.

Shairi: Nitakumbuka wewe toka inchi ya Yordani na ya Hermoni.

Sauti ya Ine.

Leo Mungu wetu Utatu usiyogawanyika anafunuliwa kwetu: Baba anashuhudia Mwana wake; toka mbingu Roho Mtakatifu anashuka kama njiwa; Mwana anainamisha kichwa chako takatifu kwa Mtangulizi, na kisha kubatizwa mpenda-wanadamu anakomboa wanadamu toka utumwa.

Shairi: Maji yalikuona, ee Mungu; maji yakakuona, yakaogopa; vilindi vilevile vikatetemeka. (*Mara ingine tunaimba hii ya yulu*).

Utukufu kwa Baba. . . Sauti ya tano.

Ee Bwana, ulipokuja mwilini kubatizwa katika Yordani sababu ya kuangazia roho zetu zenye kupotea pakutuokoa toka mitego na werevu wa nyoka, ukawa chombo cha ushuhuda wa Baba, na Roho Mtakatifu akashuka juu yako kama njiwa. Tokea sasa ikaa katika roho zetu, ee mpenda-wanadamu tena Bwana mwenye rehema.

Sasa na siku zote. . . *Mara ingine hii.*

Prokimenon Sauti ya ine.

Maji yalikuona, ee Mungu; maji yakakuona, yakaogopa; vilindi vilevile vikatetemeka.

Shairi: Sauti ya Bwana pa maji.

Unabii ya Nabii Isaya tutasoma. (1, 16-20).

Mujioshe, mujitakase; mwondoshe uovu wa matendo yenu toka mbele ya macho yangu; mwache kufanya uovu; mujifundishe kufanya mema; mutafute hukumu za haki, musaidie huyu aliyeonewa, hukumieni yatima, mwombe mujane. Haya, kujeni na tufanye shauri pamoja, Bwana anasema, hata zambi zenu ni nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kabisa kama theluji: Hata ni nyekundu kama nyekundu ya damu zitakuwa

kama manyoya ya kondoo. Lakini kama mukikataa na kuasi, mutakuliwa na upanga: Kwa maana kinywa cha Bwana kimesema maneno haya.

Matendo ya Mitume (19, 1-8)

Ikakukwa wakati Apolo alipokuwa katika Korinto, Paulo akikwisha kupita kati ya inchi za juu, akafika Efeso, akaona wanafunzi wengine, akawauliza: Mulipokea Roho Mutakatifu wakati mulipoamini? Wakajibu: Hapana, hatukusikia ya kama Roho Mutakatifu yuko. Akawauliza: Basi, mulibatizwa kwa ubatizo gani? Wakasema: Kwa ubatizo wa Yoane. Paulo alisema: Yoane alibatiza kwa ubatizo wa toba, akiwaambia watu wamwamini yeye atakayekuja nyuma yake, ndiye Kristu Yesu. Waliposikia maneno haya wakabatizwa katika jina la Bwana Yesu. Na wakati Paulo alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mutakatifu alikuja juu yao, wakaanza kusema kwa jugha na kutabiri. Na jumla yao walikuwa kama wanaume kumi na wawili. Akaingia ndani ya sunagogi, akasema kwa uhodari, akabishana na watu kwa miezi mitatu, na kuwavuta waamini maneno ya ufalme ya Mungu. .

EVANGELIO

Hekima; Inukeni tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.

Msomaji: Na kwa roho yako.

Somo ya Evangelio Takatifu ilionandikwa na Mwevangelizaji Marko, tusikilize.

Msomaji: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

Padri:

Mwanzo wa Habari Njema ya Yesu Kristu, Mwana wa Mungu. Kama maneno yaliyoandikwa katika kitabu cha nabii Isaya: Tazama, ninatuma mujumbe wangu mbele ya uso wako atengeneze njia yako; sauti ya mutu akilia jangwani, tengenezeni njia ya Bwana, nyosheni mapito yake. Yoane alikuja akibatiza katika jangwa, akahubiri ubatizo wa toba kwa kusamehewa zambi. Wayuda wote na watu wote wa Yerusalema walikwenda kwake, wakabatizwa naye katika mtoni wa Yorodani, wakikiri zambi zao. Yoane alivaa singa za ngamia na mukaba wa ngozi kwa kiuno chake; Alikula nzige na asali ya poli. Alihubiri akisema: Mutu atakuja nyuma yangu; yeye mwenye uhodari kuliko mimi, sistahili kuinama na kufungua kamba ya viatu vyake. Mimi nimewabatiza ninyi kwa maji, lakini yeye atawabatiza ninyi kwa Roho Mutakatifu.

Kisha Msomaji anasoma:

Ahimidiwe Bwana wetu, ahimidiwe Bwana siku kwa siku. Mungu huyu anatuletea wokovu. Mungu wetu ni Mungu mwenye kuokoa.

Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utukufu. . . sasa. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

Kisha tunasoma Kontakion:

Aliposhuka leo katika maji ya Yordani Bwana akamwambia Yoane: Usiogope kunibatiza; nimekuja kuokoa Adamu Baba wa kwanza.

Kisha tunasema: Bwana hurumia, (mara makumi ine) na hii sala: Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa. . (Ona ukurasa 5).

Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia. Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . . Uliye wathamani. . . Kwa jina la Bwana barikia, ee padri:

Mungu atufazili na kutubariki, atuangazie uso wake na kutuhurumia.

Padri anasoma hii sala:

Mungu, Rabi, Baba Mwenyezi; Mwokozi, Mwana wa pekee, Yesu Kristu na Roho Mtakatifu, umungu moja, nguvu moja, unihurumie; wakati wa mwisho uniokoe mimi mukoosifu wako, kwani unabarikiwa milele na milele. Amina.

SAA WA SITA

Musomaji anasoma mara moja:

Njooi tumwinamie na tumsujudu Mungu na Mfalme wetu.

Njooi tumwinamie na tumsujudu Kristu Mfalme wetu.

Njooi tumwinamie na tumsujudu Yeye Kristu aliye Mfalme wetu.

Zaburi 73 (74).

Ee Mungu, kwa nini umetutupa milele? Kwa nini hasira yako inatoa moshi juu ya kondoo za malisho yako? Kumbuka makutano yako, uliyonunua zamani, uliyokomboa kuwa kabila la uriti wako; Na mulima Sayuni, pahali ulipokaa. Nyanyua miguu yako kwa maangamizi kwa milele, Mabaya yote adui aliyofanya katika pahali patakatifu. Adui zako wamenguruma katikati ya kusanyiko lako. Wamesimamisha bendera zao kuwa alama. Wameonekana kwa watu walionyanyua Mashoka juu ya kichaka cha miti. Na sasa kazi yake yote iliyochorwa, Wanaiyunja kwa mashoka na nyundu. Wamewasha pahali patakatifu pako kwa moto; Wamechafua kao la jina lako hata chini. Walisema moyoni mwao: Tuwaangamize kabisa; Wameteketeza masunagogi ya Mungu yote katika inchi. Hatuoni alama zetu, Wala sasa hakuna nabii, Wala hakuna mumoja katikati yetu anayejua hata wakati gani. Hata wakati gani, ee Mungu, adui atalaumu? Adui atakufuru jina lako milele? Kwa nini unarudisha mukono wako, hata mukono wako wa kuume? Uutoe kifua ni mwako na kuwaharibu kabisa. Lakini Mungu ni Mfalme wangu tangu zamani, Akifanya kazi ya wokovu katikati ya inchi. Umetenga bahari kwa nguvu yako; umevunja vichwa vya majoka katika maji. Umevunja vichwa vya lewiatani vipande vipande, umemutoa kuwa chakula kwa watu wanaokaa jangwani. umepasua chemchemi na garika, umekausha mito yenye maji siku zote. Muchana ni wako, usiku vilevile ni wako: Umetengenezä nuru na jua. Umeweka mipaka yote ya inchi, umefanya wakati wa jua kali na wakati wa baridi. Kumbuka neno hili ya kuwa adui amelaumu, ee Bwana, na watu wapumbafu wamekufuru jina lako. Usimupe nyama mukali nafsi ya hua yako: Usisahau uzima wa masikini zako milele. Angalia agano: Maana pahali pa giza pa inchi pamejaa makao ya ukali. Mwenye kuteswa asirudi amekwisha kuhayarishwa: Masikini

na wenye hitaji wasifu jina lako. Simama, ee Mungu, ujitetee mwenyewe: Kumbuka namna mupumbafu anavyokulaumu muchana kutwa. Usisahau sauti ya adui zako: Kelele lao wanaosimama juu yako linapanda daima.

Zaburi 76 (77).

Nitapazia Mungu sauti yangu; hata Mungu sauti yangu, naye atanisikia. Kwa siku ya taabu yangu nilitafuta Bwana. Mukono wangu ulinyoshwa usiku wala haukulegea; Nafsi yangu Ilikataa kufarijiwa. Ninakumbuka Mungu, na ninafazaika; ninanungunika, na roho yangu inashindwa. Unashika macho yangu ukitazama; nimefazaishwa hata siwezi kuserna. Nimefikili siku za zamani Miaka ya nyakati za kale: Ninakumbuka wimbo wangu katika usiku; Ninawaza moyoni; roho yangu imetafutatafuta. Bwana atatupa milele? Wala hatapendelea tena kabisa? Rehema zake zimekoma milele? Ahadi yake inakosa kizazi na kizazi? Mungu amesahau kuonyesha neema? Kwa kasirani amefunga rehema zake? Nikasema: Huu ni uzaifu wangu; lakini nitakumbuka miaka ya mukono wa kuume wake aliye juu. Nitataja matendo ya Bwana. Kwani nitakumbuka rnaajabu yako ya zamani. Nitafikili vilevile juu ya kazi yako yote, na kuwaza juu ya matendo yako. Njia yako, ee Mungu, ni katika pahali patakatifu; nani aliye mungu mukubwa kama Mungu? Wewe ni Mungu anayefanya maajabu; umejulisha watu nguvu yako. Na mukono wako umeokoa watu wako, wana wa Yakobo na Yosefu. Maji yalikuona, Ee Mungu; maji yakakuona, yakaogopa; vilindi vilevile vikatetemeka. Mawingo yalimwanga maji; Mbingu zilitoa sauti. Mishale yako ikakwenda mbali vilevile. Sauti ya radi yako ilikuwa katika tufani, lalo zikaangaza ulimwengu; Inchi ikatetemeka, ikatikisika. Njia yako ilikuwa katika bahari, na mapito yako katika maji makubwa, Wala hatua zako hazikujulikana. Uliongoza watu wako kama kondoo, kwa mukono wa Musa na Haruni.

Zaburi 90 (91).

Yeye anayekaa kwa pahali pa maficho yake aliye juu atakaa chini ya kivuli cha Mwenyezi. Nitasema juu ya Bwana, yeye ni pahali pangu pa kukimbilia na boma la nguvu langu, Mungu wangu ninayemwamini. Kwa maana atakuokoa toka mutego wa muwindaji ndege, na kwa tauni ya uharibifu. Na manyoya yake atakufunika. Na chini ya mabawa yake utakimbilia, kweli yake ni ngabo na kigabo. Hutaogopa kwa woga wa usiku, wala kwa mushale unaoruka muchana; kwa tauni inayotembea katika giza, wala kwa kuharibu kunakoharibu azuhuri, elfu moja wataanguka kando yako, na elfu kumi kwa mukono wako wa kuume; lakini hakutafika karibu nawe. Na macho yako tu utatazama, na kuona zawabu ya waovu. Maana wewe, ee Bwana, ni pahali pangu pa kukimbilia! Umejanya aliye juu kao lako; mabaya hayatakupata wewe wala tauni haitafika na hema yako. Maana ataagiza malaika yake juu yako, wakuchunge katika njia zako zote. Watakuchukua juu mikononi mwao, usivunje muguu wako kwa jiwe. Utakanyaga simba na nyoka mudogo mwenye sumu, utakanyaga mwana-simba na joka. Kwa sababu ametia mapendo yake juu yangu, kwa hivi nitamuponyesha. Nitamuweka juu kwa sababu amejua jina langu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Allilulia, allilulia, allilulia, utukufu kwako, ee Mungu. (*mara tatu*), Bwana hurumia (*mara tatu*).

Kisha tunasoma hii mwimbo:

Utukufu kwa Baba. . .

Zamani Yordani ilirudi nyuma, wakati Eliseo alipigapo nguo yako, na maji yaligawanyika kisha kutwaliwa kwa Elia mbinguni; mawimbi yakawa kwake njia kavu kwa mfano wa Ubatizo tunakovuka mtoni wa hii uzima yenyi kututikisa. . Kristu anaonekana katika Yordani sababu ya kutakasa maji.

Sasa na siku zote. . . Theotokion.

Kwani hatuna matumaini hata moja sababu ya zambi zetu nyingi, umwombe huyu aliyezaliwa kwako, ee Bikira Mzazi-Mungu. Maana ni la nguvu, ombi la Mama kwa kupata neema ya Rabi. Usizarau maombi ya wenye zambi, ewe Mtukufu kamili, kwa kuwa yeye ni mwenye rehema na Mweza kwa kuokoa, huyu aliyekubali kuteswa mwilini kwa ajili yetu.

Kisha tunaimba hii wimbo, (idiomela):

Sauti wa mnane.

Ni hivi Bwana anamwambia Mtakatifu Yoane: Kubali tu, ee Nabii, unibatize japo mimi ni Muumba wako na mwenye kuangazia na kutakasa ulimwengu kwa neema; gusa kichwa changu takatifu, bila kusitasita, ee Nabii, timiza sasa, mimekuja kutimiza haki yote, usisitesite, kwani nakuja kuharibu adui mfalme wa giza mwenye kujificha katika maji, sababu ya kuokoa dunia na kwa mapendo kuipatia uzima wa milele.

Mara ingine hii, bila shairi.

Shairi: Nitakumbuka wewe toka inchi ya Yordani na ya Hermoni.

Sauti ya sita.

Leo unabii na zaburi imetimizika, kwa maana imesema: Bahari iliona na ilikimbia, maji ya Yordani yamerudi nyuma mbele ya Bwana Mungu wa Yakobo anayekuja kubatizwa na mtumishi kusudi zikitakaswa kwa uchafu wa miungu ya uongo, roho zetu ziweze kuangazwa.

Shairi: Maji yalikuona, ee Mungu; maji yakakuona, yakaogopa; vilindi vilevile vikatetemeka. (*Mara ingine tunaimba hii ya yulu*)

Utukufu kwa Baba. . . Sauti ya tano.

Sababu gani unarudisha mawimbi yako, ee Yordani? Sababu gani unayakataza kutiririka pahali pa kuendelea kutelemuka kama desturi? Ikajibu: Siwezi kuvumilia moto mkali; natetemeka mbele ya mapendo kubwa iliyokataziwa; hii iliyo safi sizoe kuiocha; hata mara moja sikufundishwa kutakasa Mtakatifu kamili, nitasafisha paka vyombo vyenye kuchafuka; tazama ananifundisha kuteketeza miiba ya zambi, Kristu anayekuja kwangu alipaza sauti na kusema: Tazama Mwana-kondoo wa Mungu anayeondoa zambi ya dunia.

Enyi Waaminifu, tupazeni sauti na tumwambieni: Ewe Mungu mwenye kujifunua kwa ajili ya wokovu wetu, ee Bwana, utukufu kwako.

Sasa na siku zote. . . *Mara ingine hii.*

Prokimenon Sauti ya ine.

Sauti ya Bwana pa maji.

Shairi: Ee abuduni Bwana kwa uzuri wa utakatifu; tetemekeneni mbele yake, inchi yote.

Unabii ya Nabii Isaya tutasoma.

Basi, kwa furaha mutateka maji katika visima vya wokovu. Na katika siku ile mutasema: Mushukuru Bwana, mwitie jina lake; mutangaze matendo yake katikati ya mataifa, mufanye ukumbusho ya kwamba jina lake limetukuka. Mwimbie Bwana; kwa maana amefanya matendo makubwa; maneno haya yajulikane katika dunia yote. Paza sauti, piga kelele, wewe unayekaa Sayuni; kwani Mutakatifu wa Israeli ni mukubwa katikati yenu.

Matendo ya Mitume tutasoma.

Barua ya Mtume Paulo kwa wa Roma tutasoma. (6, 3-11).

Wa ndugu, ao hamufahamu, sisi sote tuliobatizwa katika Yesu Kristu, tulibatizwa katika kufa kwake? Hivi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika kufa: Hata kama Kristu alivyofufuka toka wafu kwa njia ya utukufu wa baba, vivyo hivyo tutembe katika upya wa uzima vilevile. Kwa maana kama tulivyoungwa pamoja naye katika mufano wa kufa kwake, tutakuwa katika mufano wa ufufuko wake vilevile. Tukijua neno hili, ya kama mutu wetu wa zamani alisulibishwa pamoja naye, mwili wa zambi uharibiwe, tusitumikie zambi tena: kwa sababu yeye aliyekufa amekwisha kuhesabiwa haki toka zambi. Lakini kama tulikufa pamoja na Kristu, tunaamini ya kuwa tutaishi pamoja naye vilevile; tukijua ya kuwa Kristu akikwisha kufufuka toka wafu, hakufi tena; wala kufa hakumutawali tena. Kwa kule kufa kwake, alikufa zambi mara moja: Lakini kwa kule kuishi kwake, anaishi kwa Mungu. Hivyo ninyi mujihesabu wenyewe kuwa wafu kwa zambi, lakini walio hai Mungu katika Kristu Yesu.

EVANGELIO

Hekima; Inukeni tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.

Msomaji: Na kwa roho yako.

Somo ya Evangelio Takatifu ilionandikwa na Mwevangelizaji Marko, tusikilize.

Msomaji: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

Padri:

Siku zile Yesu alitoka Nazareti ya Galilaya, akabatizwa na Yoane katika Yorodani. Mara moja akitoka kwa maji aliona mbingu zinapasuka na Roho akishuka juu yake kama hua; na sauti ikatoka mbinguni: Wewe ndiwe Mwana wangu, mupendwa wangu, ninapendezwa nawe. Mara moja Roho alimusukuma jangwani. Alikuwa katika jangwa siku makumi ine na alijaribiwa na Shetani; alikuwa pamoja na nyama; na malaika walilutumikia.

Waimbaji: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

Kisha Msomaji anasoma:

Huruma yako itufikie upesi, kwani tumetaabika sana. Utusaidie, ee Mungu Mwokozi wetu, kwa ajili ya utukufu wa jina lako. Utuokoe, utusamehe zambi zetu kwa ajili ya jina lako.

Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

Kisha tunasoma Kontakion:

Aliposhuka leo katika maji ya Yordani Bwana akamwambia Yoane: Usiogope kunibatiza; nimekuja kuokoa Adamu Baba wa kwanza.

Kisha tunasema: Bwana hurumia, (mara makumi ine) na hii sala: Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa. . . (Ona ukurasa 5).

Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia. Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . . Uliye wadamani. . . Kwa jina la Bwana barikia, ee padri:

Mungu atufazili na kutubariki, atuangazie uso wake na kutuhurumia.

Padri atasoma hii sala ya Mtakatifu Basile Mukubwa.

Ee Mungu na Bwana wa majeshi, fundi wa kiumbe yote, kwa mapendo ya rehema yako isiyoweza kufananishwa, ulimtuma Mwana wako wa pekee, Bwana wetu Yesu Kristu, kwa ajili ya wokovu wa wanadamu. Ulizima ile barua ya deni zetu, kwa msalaba wake tukufu na ulishinda, katika hii, ufalme na nguvu za giza. Wewe mwenyewe, ee Rabi, mpenda-wanadamu, utupokee sisi wenye zambi; pokea shukrani zetu na maombi yetu. Utuopoe ku kosa yote yenye kuzuru na ya giza na kwa wale wote wenye kutafuta kutuzuru, maadui wenye kuonekana na wasioonekana. Toboa mwili wetu na woga wako, usiinamishe mioyo yetu ku maneno wala ku mawazo mabaya, lakini umiza mioyo yetu ku mapendo yako ili wakati wote macho yenye kukaza kwako, na tukiongozwa na nuru isiyokaribika na ya milele, na kukutolea utukufu na shukrani, Baba wasipo mwanzo, pamoja na Mwana wako wa pekee na Roho wako Mtakatifu kamili, mwema na mletaji uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SAA WA TISA

Msomaji mara moja anasoma:

Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utukufu. . . Sasa na siku. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . . Bwana hurumia (*mara kumi na mbili*).

Njooi tumwinamia. . .

Kisha tunasoma:

Zaburi 92 (93).

Bwana anatawala; amevikwa utukufu; Bwana amevikwa, amejifungia nguvu: Ulimwengu umesimamishwa usiweze kuhamishwa. Kiti chako cha ufalme kimesimamishwa tangu zamani: Wewe ni tangu milele. Garika zimepaza, ee Bwana, garika zimepaza sauti yao; garika zimepaza kunguruma kwao. Kupita sauti za maji mengi, mawimbi makubwa ya bahari, Bwana aliye juu ni mwenye uwezo. Shuhuda zako ni imara: Utakatifu unafaa nyumba yako, ee Bwana, kwa milele.

Zaburi 113 (114), 114 (115).

Wakati Israeli walipotoka Misri, Nyumba ya Yakobo toka watu wa lugha ya kigeni; Yuda ilikuwa pahali pake patakatifu, Israeli miliki yake. Bahari iliona, ikakimbia; Yorodani ikarudishwa nyuma. Milima ikaruka kama kondoo ndume, Vilima vidogo kama wana-kondoo. Una nini, ee wewe bahari, hata unakimbia? Wewe Yorodani, hata unarudi nyuma? Ninyi milima munaoruka kama kondoo ndume; Ninyi vilima vidogo, kama wana-kondoo? Tetemeka, Ee inchi, mbele ya uso wa Bwana, mbele ya uso wa Mungu wa Yakobo: Aliyegeuza mwamba kuwa ziwa la maji, Jiwe gumu kuwa chemchemi si kwetu, ee Bwana, si kwetu, lakini jina lako ulitukuze, kwa ajili ya rehema yako, na kwa ajili ya kweli yako. Kwa nini mataifa watasema: Mungu wao ni wapi? Lakini mungu wetu ni mbinguni; Amefanya neno lo lote alilotaka. Sanamu zao ni feza na zahabu, Kazi ya mikono ya watu. Zina vinywa, lakini hazisemi, zina macho, lakini hazioni; zina masikio, lakini hazisikii; zina pua, lakini hazinusi; zina mikono, lakini hazigusi; zina miguu, lakini hazitembei; wala hazitoi sauti kwa koo yao. Wao wanaozifanya watakuwa sawasawa nao; Ndiyo, kila mutu anayezitumainia. Ee Israeli, utumainie Bwana: Yeye ni musaidia wao na ngabo yao. Ee nyumba ya Haruni, mutumainie Bwana: Yeye ni musaidia wao na ngabo yao. Ninyi munaogopa Bwana, mutumainie Bwana: Yeye ni musaidia wao na ngabo yao. Bwana ametufikili, atatubariki: Atabariki nyumba ya Israeli; Atabariki nyumba ya Haruni. Atawabariki wanaogopa Bwana, Wadogo na wakubwa. Bwana awaongeze ninyi kupita na kupita, Ninyi na wana wenu. Mubarikiwe ninyi na Bwana, aliyefanya mbingu na dunia. Mbingu ni mbingu za Bwana; lakini amewapa wana wa watu inchi. Wafu hawasifu Bwana, wala wo wote wanaoshuka kimya; lakini sisi tutabariki Bwana tangu sasa hata milele. Musifu Bwana.

Zaburi 85 (86).

Uiname sikio lako, ee Bwana, unijibu; maana mimi ni masikini na mwenye hitaji. Chunga nafsi yangu maana mimi ni mwema; ee wewe Mungu wangu, ponyesha mutumishi wako anayekutumainia. Unirehemu, ee Bwana; maana kwako ninalia muchana kutwa. Furahisha nafsi ya mutumishi wako; maana kwako, ee Bwana, ninanyanyua nafsi yangu. Kwani wewe, Bwana, ni mwema, na tayari kusamehe, ukijaa rehema kwa wote wanaokuomba. Sikia, ee Bwana, maombi yangu; na sikiliza sauti ya kuomba kwangu. Kwa siku ya taabu yangu nitaomba kwako, kwani utanjibu: Hakuna mwingine katika miungu kama wewe, ee Bwana, wala hakuna kazi kama kazi zako. Mataifa yote uliyofanya watakuja na kuabudu mbele yako, ee Bwana; na watatukuza jina lako. Kwa kuwa wewe ni mukubwa, na unafanya maajabu; wewe pekee ni Mungu. Unifundishe njia yako, ee Bwana; nitatembea katika kweli yako; ufunganishe moyo

wangu kuogopa jina lako. Nitakusifu, ee Bwana Mungu wangu, na moyo wangu wote, na nitatukuza jina lako kwa milele. Maana rehema yako ni kubwa kwangu, na umeponyesha nafsi yangu toka Hadeze ya chini kabisa. Ee Mungu, wenye majivuno wamesimama juu yangu, na makutano ya wenye jeuri wametafuta nafsi yangu, wala hawakukuweka wewe mbele yao. Lakini wewe, ee Bwana, ni Mungu anayejaa huruma na neema, Muvumilivu, mwenye rehema na kweli nyingi. Ugeuke kwangu na kunirehemu; Umupe mutumishi wako nguvu yako, na kuponyesha mwana wa kijakazi chako. Unionyeshe alama kwa wema; hata wao wanaonichukia wapate kuiona na kuhayarishwa, kwa kuwa wewe, Bwana, umenisaidia, na kunifariji.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Allilulia, allilulia, allilulia, utukufu kwako, ee Mungu. (*mara tatu*), Bwana hurumia (*mara tatu*).

Kisha tunasoma hii mwimbo:

Utukufu kwa Baba. . .

Zamani Yordani ilirudi nyuma, wakati Eliseo alipigapo nguo yako, na maji yaligawanyika kisha kutwaliwa kwa Elia mbinguni; mawimbi yakawa kwake njia kavu kwa mfano wa Ubatizo tunakovuka mtoni wa hii uzima yenyi kututikisa. . Kristu anaonekana katika Yordani sababu ya kutakasa maji.

Sasa na siku zote. . . Theotokion.

Wewe uliyezaliwa kwa Bikira kwa ajili yetu, na uliyevumilia usulubisho, ee Mwema, uliyenyaganya mauti kwa lufu, na uliyeonyesha usimamao sawasawa na Mungu, usikengue walioubwa kwa mukono wako; onyesha mapendo yako kwa wanadamu, murehemu; pokea Mzazi-Mungu aliyekuzaa, aliyepatanisha juu yetu, na okoa, ee Mwokozi wetu, taifa isiyotumainia.

Kisha tunaimba hii wimbo:

Sauti ya saba.

Bumbwazi iliwashika wale walimuona Muumba wa inchi na wa mbingu kuvua nguo sababu ya kubatizwa moto kwa mkono wa mtumishi kusudi ya kufanya wokovu wetu akitenda kama huyu mwenye kutumikia; Malaika wote waliogopa na kufurahiwa mbinguni. Pamoja nao tunasujudu mbele yako: Utuokoe, ee Bwana Mungu wetu.

Mara ingine hii, bila shairi.

Shairi: Nitakumbuka wewe toka inchi ya Yordani na ya Hermoni.

Sauti ya mbili.

Wakati Bwana wa utukufu alikuja kwake, alipomuona, Mtangulizi akapaza sauti: Tazama anakuja Mwokozi mwenye kuondoa dunia toka uharibifu; tazama anatumkomboa toka sikitiko; huyu mwenye kutuondolea zambi zetu, tazama, kwa kutaka kwake amekuja duniani anazaliwa kwa Bikira Mtakatifu kamili; sisi tulikuwa watumwa anatumfanya kuwa wana wa Mungu; anaondoa wanadamu toka giza sababu ya kuwangazia kwa maji ya Ubatizo yake takatifu. Kujeni sisi wote tumutukuze pamoja na Baba na Roho Mtakatifu.

Shairi: Maji yalikuona, ee Mungu; maji yakakuona, yakaogopa; vilindi vilevile vikatetemeka. (*Mara ingine tunaimba hii ya yulu*)

Utukufu kwa Baba. . . Sauti ya tano.

Hii wimbo musomaji ataisoma kati ya Kanisa na kisha kundi ya waimbaji wataimba pamoja ku fasi yao.

Ee Mbatizaji, mkono ambayo iligusa kichwa cha Bwana na ilituonyesha Mwokozi, (*mara tatu*).

Kwa ajili yetu, uinyoshe kwake sababu ya matumaini unayokwake, kwani kwa ushuhuda wake wewe ni mkubwa wa Manabii wote. Macho uliona nayo Roho Mtakatifu akishuka kama njiwa, ee Mbatizaji, umutazame nayo kusudi atuonyeshe mema yake.

Utuonyeshe ushirika wako, utuonyeshe ushirika wako, utuonyeshe ushirika wako, ukisimamia hii siku kuu na nyimbo zetu kwa heshima yake.

Prokimenon Sauti ya tatu.

Bwana ni mwangaza yangu na Mwokozi yangu.

Shairi: Bwana ni mulinzi ya uzima yangu.

Unabii ya Nabii Isaya tutasoma. (49, 8-15).

Bwana anasema hivi: Kwa wakati uliokubaliwa nilikusikia, na kwa siku ya wokovu nilikusaidia; nami nitakuchunga, na kukutoa uwe mapatano ya watu, kusimamisha inchi, na kuritisha uriti uliokuwa wa kuharibika; kuwaambia wafungwa, tokeni; na wale walio pa juu watapata malisho. Hawataona njaa, wala kiu, , wala hari, wala jua halitawapiga; maana yeye anayewarhemu atawapeleka, naye atawaongoza karibu na visima vya maji. Nami nitafanya milima yangu kuwa njia, na njia zangu kubwa zitatumizwa zote. Tazama, hawa watakuja kutoka mbali; na tazama, hawa kutoka kaskazini, na kutoka manganizi; na hawa kutoka inchi ya Sinimu. Imbeni, ee mbingu; furahi, ee dunia; Pazeni sauti ya kuimba, ee milima: Kwa sababu Bwana amefariji watu wake, na atarehemu watu walioteswa. Lakini Sayuni alisema: Bwana ameniacha, na Bwana amenisahau. Mwanamuke anaweza kusahau mutoto wake anayenyonya, hata asihurumie mwana wa tumbo lake? ndiyo, wanaweza kusahau, lakini mimi sitakusahau wewe.

Matendo ya Mitume

Barua ya Paulo kwa Tito tutasoma.

Mtoto wangu Tito, kwa sababu neema ya Mungu inayoleta wokovu kwa watu wote, imeonekana, ikitufundisha sisi kukataa ubaya na tamaa za dunia, na kuishi na kiasi kwa haki, na utawa, katika ulimwengu wa sasa, tukitazamia tumaini la baraka, na kuonekana kwa utukufu wa Mungu mukubwa, Mwokozi wetu Yesu Kristu: Aliyejitoka mwenyewe kwa ajili yetu atukomboe toka uovu wote, na kujisafishia watu wawe mali yake mwenyewe, wenye bidii sasa katika kazi njema. Semia maneno haya, inya, na kuhamakia kwa nguvu zote. Hata mutu mmoja asikuzarau. Ukumbushe watu kunyenyekea wenye

kutawala na mamlaka, na kutii, na kuwa tayari, kwa kila kazi njema, wasitukane mutu, wasiwe wagomvi; wawe wapole, walionyesha adabu yote kwa watu wote. Kwa sababu zamani sisi vilevile tulikuwa pasipo akili, wenye kuasi, tumedanganywa, tukitumikia tamaa na anasa za namna nyingi, tukiishi katika uovu na hasidi, tukichukiza na kuchukiana. Lakini wakati wema wa Mungu Mwokozi wetu, na mapendo yake kwa watu yalipoonekana.

Mwimbaji: Alliluia (*mara tatu*).

EVANGELIO

Hekima; Inukeni tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.

Msomaji: Na kwa roho yako.

Somo ya Evangelio Takatifu ilionandikwa na Mwevangelizaji Luka, tusikilize.

Msomaji: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

Padri:

Katika mwaka wa kumi na tano wa kutawala kwake Tiberio Kaisari, Pontio Pilato alikuwa liwali wa Yudea, na Herode mutawala wa Galilaya, na ndugu yake Filipo mutawala wa Iturea na wa inchi ya Taroniti, na Lisania mutawala wa Abilene. Ana na Kayafa walipokuwa makuhani wakubwa, neno la Mungu lilikuja kwa Yoane mwana wa Zakaria jangwani. Akafika katika inchi yote iliyo kando ya Yorodani, akihubiri ubatizo wa toba kwa kusamehe kwa zambi; kama lilivyoandikwa katika kitabu cha maneno ya nabii Isaya: Sauti ya mutu akilia jangwani, tengenezeni njia ya Bwana, nyosheni mapito yake. Kila bonde litajazwa na kila mulima na kilima kitashushwa, njia zinazokunjama zitanyoshwa, na njia zilizoparuzwa zitakuwa sawa. Halafu akawaambia makutano waliotokea wabatizwe naye: Uzao wa nyoka, nani aliyewaonya ninyi kukimbia hasira itakayokuja? Zaeni basi matunda yanayopatana na toba; wala musianze kusema ndani ya roho zenu: Tuna Abrahamu ndiye baba yetu; kwea sababu ninawaambia ninyi ya kwamba katika mawe haya Mungu anaweza kunyanyulia Abrahamu watoto. Ma sasa shoka limewekwa katika shina la miti; basi, kila muti usiozaa matunda mema utakatwa na kutupwa motoni.

Waimbaji: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

Kisha tunasoma:

Usituache mpaka mwisho, sababu ya jina lako takatifu, usiharibu agano lako, na usitenge kwa sisi rehema yako, sababu ya Abrahamu mpendwa wako, na Isaaka mtumishi wako na Israeli mtakatifu wako.

Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utukufu. . Sasa. . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

Kisha tunasoma Kontakion:

Aliposhuka leo katika maji ya Yordani Bwana akamwambia Yoane: Usiogope kunibatiza; nimekuja kuokoa Adamu Baba wa kwanza.

Kisha tunasema: Bwana hurumia, (mara makumi ine) na hii sala: Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa. . . (Ona ukurasa 5).

Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia. Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . . Uliye wadamani. . . Kwa jina la Bwana barikia, ee padri:

Padri: Mungu atufazili na kutubariki, atuangazie uso wake na kutuhurumia.

Padri atasoma hii sala ya Mtakatifu Basile Mukubwa.

Ee Rabi na Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, mpole kwa kukasirika juu ya makosa yetu, unatufikisha mpaka hii wakati ambako ulipotundikwa juu ya msalaba wenyi kuleta uzima, ukamufungulia munyanganyi mlango ya paradizo na ukavunja mauti kwa lufu. Utuhurumie pia na sisi watumishi wako wasiostahili tena waovu; maana tulitenda zambi na hatustahili kunyanyua macho kwa kutazama mbinguni. Ndiyo, tuliacha njia ya haki, tulitembea kama ilivyopenda roho yetu. Lakini tunaomba wema wako: Utusamehe, ee Bwana, kadiri ya rehema yako kubwa na utuokoe kwa ajili ya jina lako takatifu, kwani tulijivuna katika maisha yetu. Utuondoe toka mkono ya adui, zima zambi zetu, regeza mawazo yetu ya mwili; hivi, tukiondoa mutu wa zamani, tutavaa mutu mupya, na tutaishi juu Yako wewe Rabi na Muombezi wetu; halafu, kwa kanuni zako, tutafika kwa mapumziko ya milele, kwa makao ya wenye heri wote. Kwani ni Wewe heri ya kweli tena furaha ya wale wenye kukupenda, ee Kristu Mungu wetu, na tunakutolea utukufu, pamoja na Baba yako asiye na mwanzo, na Roho wako Mtakatifu kamili, mwema na mletaji-uzima, daima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Kisha tunasoma **TIPIKA:**

Umsifu Bwana, ee roho yangu, na yote yaliyo ndani yangu yasifu jina lake Takatifu. Umsifu Bwana, ee roho yangu, wala usisahau mema yake yote! Yeye anasamehe zambi zako zote, anaponyesha magonjwa yako yote. Yeye anakomboa uzima wako katika kaburi, anayekutia taji ya huruma na rehema. Yeye anashibisha mema maisha yako, na ujana wako unarudishwa upya kama wa tai. Bwana anatenda wa huruma, anawahukumu sawa wote wanaoteswa. Alimujilisha Musa njia zake, wana wa Israeli mapenzi yake. Bwana na mwenye huruma na mpole, mvumilivu, mwenye mema mingi. Haendelei daima kukaripia, wala hatavhunga hasira yake milele. Hakututendia kadiri ya zambi zetu, wala hakutulipa sawasawa na makosa yetu. Kama vile mbingu ziinuka juu ya inchi, hivyo Bwana alizidisha kwa wenye wakumwogopa. Kama mashariki ilivyo mbali na magaribi, hivyo na zambi zetu ameziweka mbali nasi. Kama vile baba anavyowahurumia watoto wake, hivyo Bwana anawahurumkia watu wanamwogopa, maana anajua tumeumbwa kwa kitu gani, anakumbuka ya kama sisi ni mavumbi. Siku za mutu ni sawa na majani, anachanua kama ua la shamba. Upepo ukiisha pita juu yake, hayupo, wala pahali pake hapaonekani tena. Lakini huruma ya Bwana inadumu tangu milele hata milele kwa wenye kumwogopa. Na haki yake kwa wana wa wana wao, kwa wale wanaoshika agano lake, wanaokumbuka amri zake wazitimize. Bwana amesimika kiti chake mbinguni, na ufalme wake unatawala vitu vyote. Msifuni Bwana, enyi Malaika wake wote, mlio na nguvu nyingi, mnaotimiza neno laki, mnaposikia sauti ya neno lake. Msifuni Bwana, enyi majeshi yake yote, watumishi wake mnaotimiza mapenzi yake.

Msifuni Bwana, enyi matendo yake yote, pahali pote pa ufalme wake. Umsifu Bwana, ee roho yangu!

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mutakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina. Umsifu, Bwana, ee roho yangu, na yote yaliyo ndani yangu yasifu jina lake takatifu. Muhimidiwe, ee Bwana.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu.

Umsifu Bwana, ee roho yangu, nitamusifu Bwana maisha yangu yote, nitamwambia Mungu wangu zaburi mimi ningali mzima. Msiwatumainie wakubwa wa dunia, wala mwanadamu asiyeweza kuokoa. Atatoa roho yake, anarudia udongo wake. Siku ile mafikili yake yote yanapotea. Heri mtu anayesaidiwa na Mungu wa Yakobo, anayemtumainia Bwana, Mungu wake. Aliyeumba mbingu na dunia, bahari na vyote vilivyomo. Anayeshika kweli wake hata milele. Anawarudishia haki waliozulumiwa, anawapa wenye njaa chakula. Bwana anawafungwa wafungwa, Bwana anafungua macho ya vipofu. Bwana anawanyanyua walioinama. Bwana anawapenda wenye haki, Bwana anachunga wageni. Anawatunza yatima na mjane, anapindua njia ya waovu. Bwana atatawala milele, Mungu wako, ee Sayuni, kizazi hata kizazi.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Uliye Mwana wa pekee tena Neno wa Mungu, ukiwa msiyekufa ukakubali kwa ajili ya wokovu wetu kupata mwili kwa Maria Mzazi-Mungu, tena Bikira daima, ukawa mtu bila kujigeuza; hata kusulubiwa, ewe Kristu Mungu, na kukikanyanga kifo kwa kifo; ukiwa mumoja na Utatu Mtakatifu, na kutukuzwa pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, utuokoe.

HERI

Katika ufalme wako, utukumbuke, ee Bwana, utakapokuja katika ufalme wako. Heri walio masikini wa roho, maana Ufalme wa mbinguni ni wao.

Heri wenye huzuni: maana wao watafarijiwa.

Heri wenye upole: maana wao watariti inchi.

Heri wenye njaa na kiu haki: maana wao watashibishwa.

Heri wenye rehema: maana wao watapata rehema.

Heri wenye moyo safi: maana wao wataona MUnngu.

Heri wenye kufanya salama: maana wataitwa wana wa Mungu.

Heri walioteswa kwa sababu ya haki: maana ufalme wa mbinguni ni wao.

Heri ninyi, wakati wanapowatukana ninyi na kuwatesa ninyi nakuwasemea ninyi kila neno baya kwa uwongo, kwa sababu yangu.

Furahini, shangilieni; kwa sababu zawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyotesa manabii waliokuwa mbele yenu.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mutakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Utukumbuke, ee Bwana, wakati utakapokuja katika ufalme wako.

Utukumbuke, ee Rabi, wakati utakapokuja katika ufalme wako.

Utukumbuke, ee Mtakatifu, wakati utakapokuja katika ufalme wako.

Kundi la waimbaji wa mbinguni wanakuambia na wanasema: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Savaothi, mbingu na dunia zimejaa na utukufu wako.

Njongeni kwake, na mutaangaziwa na uso wetu usipate haya.

Kundi la waimbaji wa mbinguni wanakuimbia na wanasema: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Savaothi, mbingu na dunia zimejaa na utukufu wako.

Utukufu kwa Baba. . .

Kundi la malaika na malaika Wakuu, pamoja na majeshi ya mbinguni wanakuimbia na waanasema: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Savaothi, mbingu na dunia zimejaa utukufu wako.

Sasa na siku zote. . .

Tunasoma Simvolo ya Imani: Nasadiki Mungu moja. . .

Kisha tunasoma:

Zima, ashilia, hurumia, ee Mungu, makosa yetu ya kutaka na yisiyokutaka, iliyofanyika kwa matendo na maneno, ya kujuwa na ya kutokujuwa ya usiku ao ya mchana, ndani ya akili na ya ufahamu; yote utuhurumie, sawa mwema na mpenda wanadamu.

Baba yetu uliye mbinguni. . .

Kontakion:

Aliposhuka leo katika maji ya Yordani Bwana akamwambia Yoane: Usiogope kunibatiza; nimekuja kuokoa Adamu Baba wa kwanza.

Kisha tunasema Bwana hurumia (mara kumi na mbili).

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Bwana hurumia (*mara tatu*), Rabi mtakatifu barikia.

Padri:

Kristu Mungu wetu ukweli, kwa maombezi ya Mama wake Mtakatifu asiye na doa wala si lawama kamili; ya Mitume Watakatifu watukufu, wasifiwa kamili na ya watakatifu wote, atuhurumie na atuokoe, kwani ni Mwema na mpenda-wanadamu.

Kwa maombezi ya wapadri watakatifu wetu, ee Bwana Yesu Kristu, Mungu wetu, utuhurumie. Amina.

SALA YA SAA MAKUBWA YA MUKAZI TANO TAKATIFU NA KUBWA

SAA WA KWANZA

Padri: Abarikiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote hata milele na milele.

Msomaji: Amina. Mungu Mtakatifu, Mweza Mtakatifu, Musiye kufa Mtakatifu, utuhurumie. (*mara tatu*). Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasana siku zote, hata milele na milele. Amina.

Utatu Mtakatifu Kamili utuhurumie, Bwana utusamehe zambi zetu, Rabi utuondolee makosa yetu, mtakatifu utukaribie na uponye magonjwa yetu. Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama mbinguni, utupe sisi leo chakula chetu cha kila siku, utusamehe ndeni zetu kama sisi vilevile tunawasamehe walio na ndeni zetu, tena usitutie katika majaribu, lakini utuokoe na yule Mwovu

Padri: Kwa kuwa Ufalme, na uwezo, na utukufu ni kwako, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hasa milele na milele.

Msomaji: Amina. Bwana hurumia (mara kumi na mbili)

Njooi tumwinamie na tumsujudu Mungu na Mfalme wetu.

Njooi tumwinamie na tumsujudu Kristu Mfalme wetu.

Njooi tumwinamie na tumsujudu Yeye Kristu aliye Mfalme wetu.

Zaburi 5(6)

Sikiliza maneno yangu, ee Bwana, uangalie mafikili yangu. Usikie sauti ya kilio changu, Mfalme wangu, na Mungu wangu: Kwa maana ninaomba kwako. Ee Bwana, asubui utasikia sauti yangu; Asubui nitatengeneza maombi yangu kwako, na kuangalia sana. Kwa maana wewe si Mungu anayependezwa na uovu. Mwovu hatakaa kwako. Wenye majivuno hawatasimama mbele ya macho yako; utachukia watenda wote wa uovu. Utaharibu wale wanaosema uwongo; Bwana anachukia mwaaji na mwenye hila. Lakini mimi, kwa wingi wa wema wako nitaingia nyumbani mwako; Katika kukuogopa wewe nitaabudu kwa upande wa hekalu lako takatifu. Uniongoze, ee Bwana, kwa haki yako kwa sababu ya adui zangu; unifanyie njia yako wazi mbele ya uso wangu. Kwa maana hapana uaminifu kinywani mwao; mutima wao ni shimo tupu; koo lao ni kaburi wazi; Wanabembeleza na ulimi wao. Uwahasabie zambi zao, ee Mungu; Waanguke kwa

mashauri yao wenyewe; uwatoe inje katika wingi wa makosa yao, kwa maana wamekuasi wewe. Lakini wote wanaokuwekea tumaini lao wafurahi, wapige kelele daima kwa furaha kwa sababu unawasimamia; wao vilevile wanaopenda jina lako wafurahi ndani yako. Kwa maana utabariki mwenye haki; ee Bwana, utamuzungusha na mapendeleo kama ngabo.

Zaburi 2

Kwa nini mataifa wanafanya ukali, na makabila wanafikili ubatili? Wafalme wa dunia wanajipanga, Na watawala wanafanya shauri pamoja Juu ya Bwana, na juu ya mupakaliwa wake, wakisema: Tuvunje vifungo vyao na kutupa mbali nasi kamba zao. Yeye anayeketi mbinguni atacheka; Bwana atawafanyia zihaka. Kisha atawaambia katika hasira yake, na kuwafazaisha katika uchungu wake; nami nimeweka mufalme wangu Juu ya Sayuni mulima wangu mutakatifu. Nitahubiri amri; Bwana aliniambia: Wewe ni mwana wangu; leo nimekuzaa. Uniombe, na nitakupa mataifa kuwa uriti wako, na miisho ya dunia kuwa miliki yako. Utawaponda kwa fimbo ya chuma, utawavunja vipande vipande kama chombo cha mufinyanzi. Na sasa ninyi wafalme, fanyeni akili; na mufundishiwe, ninyi waamuzi wa dunia. Tumikieni Bwana kwa woga, na furahini pamoja na kutetemeka. Busuni mwana asikasirike, nanyi munapotea njiani, kwa kuwa hasira yake itawaka upesi. Heri wote wanaomukimbilia.

Zaburi 21 (22).

Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini umeniacha? Kwa nini wewe ni mbali na kumsalida, na kwa maneno ya kuugua kwangu? Ee Mungu wangu, ninalia muchana, lakini hujibu; na wakati wa usiku, wala sinyamazi. Lakini wewe ni mutakatifu, ee wewe unayeketi juu ya sifa za Israeli. Baba zetu walikuwekea tumaini lao, walitumaini, nawe uliwaponyesha. Wakalia kwako, na waliponyesha, walikuwekea wewe tumaini lao, wala hawakupata haya. Lakini mimi ni mududu wala si mutu; Laumu ya watu, na mwenye kuzarauliwa na watu. Wote wanaoniona wananicheka sana; wanatoa mudomo, wanatikisa vichwa vyao, wakisema: Ametegemea Bwana; yeye amuponyeshe; Amuponyeshe maana anapendezwa naye. Lakini wewe ndiwe uliyenitoa tumboni, Ulinitumainisha katika maziwa ya mama yangu. Nilitupwa kwako tangu tumboni; Wewe ni Mungu wangu toka tumboni mwa mama yangu. Usiwe mbali nami; maana taabu ni karibu, Maana hakuna musaidia. Ngombe ndume wengi wamenizunguka, Ngombe ndume wenye nguvu za Basani wamenisonga. Wamenifumbua vinywa, Kama simba mwenye njaa na mwenye kunguruma. Nimemwangika kama maji, na mifupa yangu yote imeteguka, moyo wangu ni kama nta; Umeyeyuka ndani ya matumbo yangu. Nguvu zangu zimekauka kama kipande cha chungu, Na ulimi wangu unaambatana na kinywa changu; Umenileta katika mavumbi ya mauti. Kwa maana imbwa wamenizunguka; kusanyiko la waovu wamenisonga; Wametoboa mikono yangu na miguu yangu. Ninaweza kuhesabu mifupa yangu yote; Wananitazama na kunikazia macho; Wanagawa nguo zangu katikati yao, Na vazi langu wanalipigia kura. Lakini wewe usiwe mbali, ee Bwana, Ee wewe musaidia wangu, fanya haraka kunisaidia. Ponyesha nafsi yangu na upanga; Mupenzi wangu na nguvu ya imbwa. Uniokoe toka kinwa cha simba; Ndiyo, toka pembe za ngombe ndume za mwitu umenijibu. Nitahubiri jina lako kwa ndugu zangu; Katikati ya kusanyiko nitakusifu. Ninyi munaogopa Bwana, mumusifu; Ninyi

wote mulio wazao wa Yakobo, mumutukuze; na mumwogope sana, ninyi wote wazao wa Israeli. Maana hakuzarau wala kuchukia mateso yake aliyeteswa; wala hakumufichia uso wake; Lakini wakati alipolia kwake, alisikia. Kwako zinatoka sifa zangu katika kusanyiko kubwa; Nitatimiza naziri zangu mbele yao wanaomwogopa. Wapole watakula na kushiba; Wanaofuata Bwana watamusifu; mioyo yenu iishi kwa milele. Miisho yote ya dunia itakumbuka na kugeuka kwa Bwana; na jamaa zote za mataifa wataabudu mbele yako. Kwa sababu ufalme ni wa Bwana; naye ndiye anayetawala mataifa. Wenye mafuta wote wa dunia watakula na kuabudu; wote wanaoshuka hata mavumbi watainama mbele yake, hata yeye asiyeweza kuchunga hai nafsi yake mwenyewe. Wazao watamutumikia; Habari za Bwana zitasimuliwa kwa kizazi kitakachokuja. Wao watakuja na kuhubiri haki yake kwa watu watakozaliwa, ya kwamba ndiye aliyefanya.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Allilulia, allilulia, allilulia, utukufu kwako, ee Mungu. (*mara tatu*), Bwana hurumia (*mara tatu*).

Kisha tunasoma hii mwimbo:

Utukufu kwa Baba. . .

Ee Kristu, ulipopanda msalabani, uliharibu uzulumu na nguvu ya Adui; apana Malaika wala mutu, lakini ni Mungu mwenyewe mwenye kutuokoa; ee Bwana, utukufu kwako.

Sasa na siku zote. . . Theotokion.

Namuna gani tutakuita ewe Mujaliwa neema? Kwa sababu ulileta duniani jua ya haki. Paradizo? Kwa sababu uliotesha ua isiyo harabika. Kwa sababu ulibaki Bikira bila uharibifu. Mama kamili? Kwa sababu ulichukua katika kifua chako takatifu Mtoto, aliye Mungu wawote. Umuombe yeye aokoe mioyo yetu.

Kisha tunaimba hii wimbo na muziki ya kuachana (Idiomela).

Sauti ya mnane.

Leo pazia ya Hekalu imepasuka katika vipande mbili sababu ya kunyamazisha makafiri, jua limeficha miangaza yake pakuona Bwana msalabani.

Tunaimba hii mara injine, bila shairi.

Kisha waimbaji wa kwanza wanaimba wimbo ingine na hii shairi:

Sababu gani hii makelele kati ya mataifa, sababu gani hii manunguniko kati ya watu?

Sauti ya mnane.

Ee Kristu Mfalme wetu, ulipelekwa kama kondoo mwenye kuchinjwa; ee Mwana-kondoo asiye na doa, ulisulubiwa msalabani kwa makafiri, ee Bwana mpenda-wanadamu, sababu ya kuzima zambi zetu.

Shairi: Wakubwa wa mataifa wanakusanyika sababu ya kufanya shauri juu ya Bwana na Kristu wao. (*Mara ingine hii wimbo ya yulu*).

Utukufu kwa Baba. . . Sauti ya mnane.

Ee Bwana, uliwaambia makafiri waliokubamba: Mumepiga mchungaji, na mumesambaza kondoo; pahali pa Mitume yangu kumi na mbili niliweza kuomba majeshi ya Malaika sababu ya kunisaidia, lakini navumilia nikiteswa kusudi yatimie mafumbo Manabii yangu waliwatangazia ninyi. Ee Bwana, utukufu kwako.

Sasa na siku zote. . . (*Mara ingine hii wimbo*)

Prokimenon. Sauti ya Ine.

Anaenda, polepole inje, anasema juu yangu.

Shairi: Heri yeye mwenye kuwaza maskini na muzaiifu, siku ya mateso Bwana atamuokoa.

Unabii ya Nabii Zakaria tutasoma. (11, 10-13)

Hivi anasema Bwana; Ninachukua gongo langu uzuri, nikalikata vipande viwili, nipate kuvunja agano nililolifanya na mataifa yote. Likavunjwa siku ile; na hivi masikini za kundi walionisikia walijua ya kama lilikuwa neno la Bwana. Nikawaambia: Kama mukipendezwa, munipe mushahara wangu; sivyo acheni. Basi walipima vipande vya feza makumi tatu kwa mushahara wangu; Bwana akaniambia: Unitupe kwa mufinyanzi, bei nzuri niliyohesabiwa nao. Ninachukua vipande makumi tatu vya feza, nikamutupia mufinyanzi ndani ya nyumba ya Bwana.

Matendo ya Mitume.

Barua ya Mtume Paulo kwa wa Galatia tutasoma.

Wa Ndugu, lakini mimi, nisijisifu hata kidogo juu ya kitu ila musalaba wa Bwana wetu Yesu Kristu; kwa yeye dunia hii imesulibiwa kwangu, na mimi kwa dunia. Kwa sababu kutahiriwa si kitu, wala kutokutahiriwa, lakini kiumbe kipya. Na wote wanaofuata amri hii, salama kwao na rehema, na kwa Israeli wa Mungu. Tangu sasa mutu asinisumbushe, kwa maana ninachukua katika mwili wangu chapa zake Yesu. Ndugu zangu, neema ya Bwana wetu Yesu Kristu iwe pamoja na roho zenu. Amina.

EVANGELIO

Hekima; Inukeni tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.

Msomaji: Na kwa roho yako.

Somo ya Evangelio Takatifu ilionandikwa na Mwevangelizaji Matayo, (27, 1-56) tusikilize.

Msomaji: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

Padri:

Na wakati ilipokuwa asubui, wakubwa wote wa makuhani na wazee wa watu wakafanya shauri juu ya Yesu kumwua; wakamufunga, wakamuchukua na kumupeleka kwa Pilato aliyekuwa liwali. Kisha Yuda aliyemutoa, wakati alipoona ya kuwa amekwisha kuhukumiwa, akatubu, akarudishia wakubwa wa makuhani na wazee vipande makumi tatu vya veza, akisema: Nimekosa wakati nilipotoa damu isiyo na kosa. Lakini wale

wakasema: Hili ni nini kwetu? Uliangalie wewe mwenyewe. Akatupa vipande vya feza katika pahali patakatifu, akaondoka; akatoka inje akajitundika mwenyewe. Wakubwa wa makuhani wakatwa vipande vile vya feza, wakasema: Si halali kuviweka katika sanduku ya hazina, kwa sababu ni bei ya damu. Wakafanya shauri, wakanunua navyo shamba la mufinyazi liwe pahali pa kuzika wageni. Kwa hivi shamba lile lilitwa shamba la damu hata leo. Halafu likatimia neno lililosemwa na Yereimia nabii, akisema: Wakatwa vipande makumi tatu vya feza, bei yake aliyesabiwa kwa bei, wana wa Israeli waliyemuhesabu kwa bei; wakavitoa kwa shamba la mufinyanzi kama Bwana alivyoniagiza. Basi Yesu akasimama mbele ya liwali; liwali akamwuliza akisema: Wewe ni Mufalme wa Wayuda? Yesu akamwambia: Wewe unasema. Na wakati wakubwa wa makuhani na wazee walipomushitaki, hakujibu neno. Halafu Pilato akamwambia: Husikii maneno mengi wanayokushuhudia? Naye hakumujibu hata neno moja; hata liwali akashangaa sana. Basi kwa wakati wa siku kubwa liwali kwa desturi alifungulia makutano mufungwa mumoja walivemutaka. Basi palikuwa na mufungwa wa kujulikana, aliyeitwa Baraba. Basi wakati walipokusanyika, Pilato akawaambia: Munataka niwafungulie ninyi nani? Baraba, ao Yesu anayeitwa Kristo? Kwa sababu alijua ya kuwa walimutoa kwa uwivu. Na wakati alipokuwa akiketi juu ya kiti cha hukumu, muke wake akatuma kwake akisema: Usiwe na neno na yule mutu mwenye haki; kwa sababu nimeteswa maneno mengi leo katika ndoto kwa ajili yake. Basi wakubwa wa makuhani na wazee wakashawishi makutano ili waombe kwa Baraba na kuharibu Yesu. Lakini liwali akajibu, akawaambia: Ni nani katika hawa wawili munayetaka niwafungulie ninyi? Wakasema: Baraba. Pilato akawaambia: Basi, nitafanya nini na Yesu anayeitwa Kristo? Wakasema wote: Asulibiwe. Akasema: Kwa nini? Ametenda ubaya gani? Lakini wakazidi sana kupiga kelele, wakisema: Asulibiwe. Basi wakati Pilato alipoona ya kuwa hakuweza kufanya neno, lakini ya kama kelele lilizidi, akatwaa maji, akanawa mikono yake mbele ya makutano, akisema: Mimi sina kosa katika damu ya mutu huyu mwenye haki; ninyi mwangalie maneno haya ninyi wenyewe. Watu wote wakajibu, wakasema: Damu yake iwe juu yetu na juu ya watoto wetu. Halafu akawafungulia Baraba, lakini akapiga Yesu mijeledi, na kututoa asulibiwe. Halafu askari za liwali wakachukua Yesu ndani ya Praitorio, wakakusanya kwake kikosi kizima. Wakamwondolea mavazi yake, wakamuvika nguo nyekundu. Wakasokota taji ya miiba, na kuiweka juu ya kichwa chake na tete mukononi mwake mwa kuume; wakapiga magoti mbele yake, wakamuzihaki wakisema: Salamu, Mufalme wa Wayuda! Wakamutemea mate, wakatwa lile tete na kumupiga kichwani. Na wakati walipomuzihaki, wakamwondolea nguo ile, wakamuvika mavazi yake mwenyewe, wakamuchukua inje kumusulidisha. Na wakati walipotoka, wakaona mutu wa Kurene, jina lake Simoni; huyu walimushurutisha ili abebe musalaba wake. Na wakati walipofika pahali palipoitwa Golgota, maana yake Mufupa wa kichwa, wakamupa mvinyo iliyochanganyika na nyongo; na wakati alipoionja hakutaka kunwa. Na wakati walipokwisha kumusulibisha, waligawa mavazi yake katikati yao wakipiga kura; wakaketi na kumulinda pale. Wakaweka juu ya kichwa chake mashitaki yake yaliyoandikwa: Huyu ni Yesu Mufalme wa Wayuda. Wakati huu wanyanganyi wawili walisulibiwa pamoja naye, mumoja kwa mukono wake wa kuume, na mumoja kwa kushoto. Nao waliopita njiani wakamutukana wakitikisisha vichwa vyao wakisema: Wewe mwenye kuvunja hekalu na kulijenga tena katika siku tatu, ujiokoe mwenyewe; kama ukiwa Mwana wa Mungu, shuka musalabani. Vile wakubwa wa makuhani wakimuzihaki pamoja na waandishi na wazee wakasema: Aliokoa wengine; hawezi kujiokoa yeye mwenyewe. Yeye ni Mufalme wa Israeli; ashuke sasa musalabani na

tutamwamini. Anaamini Mungu; amwokoe sasa kama anamutaka; kwa sababu alisema: Mimi ni Mwana wa Mungu. Wanyanganyi walisulubiwa pamoja naye walimutukana hivi vilevile. Basi toka saa sita giza lilikuwa juu ya inchi hata saa tisa. Na karibu na saa tisa Yesu alipaza sauti akisema: Eloi, Eloi, lama sabaktani; maana yake: Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini umeniacha? Na wengine wao waliosimama pale, wakati waliposikia, wakasema: Mutu huyu anaita Elia. Na mara moja mumoja wao akakimbia, akatwaa sifongo na kuijaza siki, akaitia juu ya muti, akamukunywesha. Wale wengine wakasema: Acha; tuone kama Elia anakuja kumwoko. Yesu akatoa sauti kubwa tena, akatoa roho yake. Na tazama, pazia la hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini; inchi ikatetemeka; miamba ikapasuka, makaburi yakafunguliwa, na miili mingi ya watakatifu waliokwisha kulala ilifufuliwa; na wakitoka katika makaburi nyuma ya ufufuko wake, wakaingia katika muji mutakatifu na kutokea kwa watu wengu. Basi akida, nao waliokuwa pamoja naye wakilinda Yesu, wakati walipoona tetemeko la inchi, na maneno yaliyofanyika wakaogopa sana, wakisema: Kweli huyu alikuwa Mwana wa Mungu. Na wanawake wengi walikuwa pale wakitazama kwa mbali, wao waliofuata Yesu toka Galilaya wakimutumikia; katikati yao alikuwa Maria Magdalene, na Maria mama ya yakobo na Yose, na mama ya wana wa Zebedayo.

Kisha Msomaji atasoma:

Ongoza mwendo wangu katika neno lako: Wala uovu wowote usinitawale. Unikomboe na maneno ya mutu: Hivi nitachunga mafundisho yako yote.

Uangazie Mutumishi wako na uso wako; na unifundishe amri yako.

Kinyuwa changu kinajazwa na sifa yako Bwana, kama ninavyotukuza ziku zote uzuri wako.

Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

Kisha tunasoma Kontakion:

Sauti ya mnane

Kujeni wote tumwinamie huyu aliyesulubiwa kwa ajili yetu; Mzazi-Mungu alipomuona msalabani akanwambia: Wewe mwenye kuteswa na hii lufu, ndiwe kweli Mwana wangu na Mungu wangu.

Kisha tunasema: Bwana hurumia, (mara makumi ine) na hii sala: Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa. . .(Ona ukurasa 5).

Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia. Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . . Uliye wathamani. . . Kwa jina la Bwana barikia, ee padri:

Mungu atufazili na kutubariki, atuangazie uso wake na kutuhurumia.

Padri anasoma hii sala:

Kristu, nuru ya kweli, aliyeangaza na kutakasa kila mutu, anayekuja duniani, na imeonekana kwetu nuru ya uso wako, ulitunyeshwa nuru ya uso wako isio zimika na ongoza mwendo wetu katika kazi ya amri yako. Kwa maombi ya Mama wako Mtakatifu na ya watakatifu wote. Amina.

SAA WA TATU

Msomaji mara moja anasoma:

Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . . Bwana hurumia (*mara kumi na mbili*), Njoooni tumwinamia. . .

Kisha anasoma:

Zaburi: 34 (35).

Ushindane, ee Bwana, na wanaoshindana nami; Upigane nao wanaopigana nami. Ushike ngabo na kigabo, na simama kwa kunisaidia. Utoe mukuki vilevile na kuzuiza wale wanaonifuata; Uiambie nafsi yangu; Mimi ni wokovu wako. Wapate haya na kupungukiwa heshima wanaotafuta nafsi yangu; Warudishwe nyuma na wafazaishwe wanaofanya shauri kwa kuniu miza. Wawe kama makanda mbele ya upepo. Malaika ya Bwana akiwafuata. Njia yao iwe na giza na utelezi, na malaika ya Bwana akiwafuata. Kwa sababu walinifichia wavu wao shimoni pasipo sababu, Pasipo sababu walichimba shimo kwa nafsi yangu. Uharibifu umupate kwa kumushutusha; na wavu wake alioficha umukamate yeye mwenyewe; aanguke ndani yake kwa uharibifu. Na nafsi yangu itafurahi ndani ya Bwana; Itashangilia wokovu wake. Mifupa yangu yote itasema: Bwana, nani aliye kama wewe, Unayeponyesha masikini na mutu aliye na nguvu kwa kumushinda, ndiyo, masikini na mwenye hitaji naye anayemuteka? Washuhuda wa uzalimu wanasimama; wananiuliza juu ya maneno nisiyojua. Wananilipa mabaya kwa mema, kwa kuacha nafsi yangu ukiwa. Lakini mimi, wakati wa ugonjwa wao nguo yangu ilikuwa gunia; nilitesa nafsi yangu kwa kufunga chakula; na maombi yangu yalirudi kifua ni mwangu mwenyewe. Nilifanya ya kama ni rafiki yangu ao ndugu yangu; Niliinama nikiomboleza, kama mutu anavyolilia mama yake. Lakini wakati mimi nilipojikwaa walifurahi, wakajikusanya; watu ovyo nisiojua walijikusanya juu yangu; Walinipasua wala hawakuacha; Kama watu wa ulimwengu wanaozihaki karamuni, Walinisagia meno. Bwana, hata wakati gani utatazama? Uponyeshe nafsi yangu na maharibifu yao, na mupenzi wangu na simba. Nitakushukuru katika kusanyiko kubwa; Nitakusifu katikati ya watu wengi. Usiache wao walio adui zangu pasipo haki kufurahi juu yangu; wala usiache wao wanaokonyeza macho kunichukia bule. Maana hawasemi maneno ya salama; lakini wanawaza maneno ya hila juu ya watulivu wa inchi. Ndiyo, walifungua kinywa chao wazi juu yangu; wakasema: Ewe! Ewe! jicho letu limeona. Umeona, ee Bwana; usinyamaze; ee Bwana, usiwe mbali nami. Ujishutushe, uamke, ili kunipatia hukumu, kwa maneno yangu, Mungu wangu na Bwana wangu. Unihukumu, Ee Bwana, Mungu wangu, kwa haki yako; Wala wasifurahi juu yangu. Wasiseme moyoni mwao; Ewe, tunataka hivi; Wasiseme: Tumemumeza. Wapate haya na kufazaika pamoja, wanaofurahia kuumizwa kwangu; Wavalishwe na haya na zarau wanaojikuza juu yangu. Washangilie na kufurahi wanaopendezwa na maneno yangu ya haki; Waseme daima: Bwana atukuzwe, anayependezwa na heri ya mutumishi wake. Na ulimi wangu utasema juu ya haki yako, na juu ya sifa yako muchana kutwa.

Zaburi 108 (109).

Usinyamaze, ee Bwana wa sifa yangu; kwa maana wamefungua juu yangu kinywa cha waovu na kinywa cha hila: Wamesema nami kwa ulimi wa uwongo. Wamenizungusha vilevile kwa maneno ya machukio, wakapigana nami pasipo sababu. Kwa kadiri ya mapendo yangu wao ni watesi wangu: Lakini mimi ninajitoa mwenyewe kwa maombi. Wamenilipa mabaya kwa mema, na chukio kwa mapendo yangu. Uweke mwovu juu yake: Na mutesi asimame kwa mukono wake wa kuume. Wakati anapohukumiwa, aonekane hana haki; maombi yake yageuzwe kuwa zambi. Siku zake ziwe chache; na mwingine atwae kazi yake. Wana wake wawe yatima, na muke wake mujane. Wana wake wawe wahuni na wenye kuomba matabisi; na wajitafutie chakula mbali na pahali pao pa ukiwa. Mutoza feza atege vyote alivyo navyo; na wageni wateke mapato ya kazi yake. Asiwe mutu wa kumurehemu; wala asiwe mutu wa kuhurumia wana wake wa yatima. Wazao wake wakatiliwe mbali; jina lao lizimishwe katika kizazi cha pili. Uovu wa baba zake ukumbushwe na Bwana; wala zambi ya mama yake isizilishwe. Ziwe mbele ya Bwana daima, ili aondoe ukumbuko wao duniani, kwa sababu hakukumbuka kuonyesha rehema, lakini alitesa masikini na mwenye hitaji, na mwenye moyo wa kuvunjika, ili awaue. Ndiyo alipenda kutukana, na kulimupata; Hakufurahi kwa baraka, na ilikuwa mbali naye, akajivika matukano kama vazi lake, na yaliingia moyoni mwake kama maji, na kama mafuta ndani ya mifupa yake. Yawe kwake kama nguo anayojifunika nayo, na kwa mushipi anajivika nao daima. Hii ni zawabu ya watesi wangu toka kwa Bwana, na ya wale wanaosema mabaya juu ya nafsi yangu. Lakini wewe unitendee kwa ajili ya jina lako, ee Mungu Bwana: Kwa kuwa rehema yako ni njema, uniponyeshe, kwa maana mimi ni masikini na mwenye hitaji, na moyo wangu umeumia ndani yangu. Ninapita kama kivuli wakati kinaposhuka: Ninapeperushwa kama nzige. Magoti yangu ni zaifu kwa sababu ya kufunga chakula; na mwili wangu umekonda kwa mafuta. Nami nilikuwa laumu kwao: Wakati wanaponiona wanatikiza vichwa vyao. Unisaidie, ee Bwana Mungu wangu; Uniokoe sawasawa na rehema yako: Ili wajue huu ni mukono maneno haya. Walaani, lakini wewe ubariki: Wakati wanaposimama watapata haya, lakini mutumishi wako atafurahi. Watesi wangu wavikwe zarau, na wajifunike kwa haya yao wenyewe kama kwa joho. Nitashukuru Bwana sana kwa kinywa changu; ndiyo, nitamusifu katikati ya makutano. Maana ayasimama kwa mukono wa kuume wa mwenye hitaji, kumwokoza nao wanaohukumu nafsi yake.

Kisha Zaburi 50(51):

Unirehemu, ee Mungu, sawasawa na wema wako, sawasawa na wingi wa rehema zako uzime makosa yangu. Unioshe kabisa na uovu wangu, na kunisafisha na zambi yangu. Maana ninajua makosa yangu, na zambi yangu ni mbele yangu daima. Nimekukosea wewe peke yako, na kufanya yaliyo mabaya machoni mwako, ili ujulikane kuwa mwenye haki wakati unaposema, na kuwa safi wakati unapotoa hukumu. Tazama, niliumbwa katika hali ya uovu, na katika makosa mama yangu alinichukua mimba. Tazama, wewe unataka kweli moyoni, na kwa siri utanijulisha hekima. Unisafishe kwa hisopo na nitakuwa safi, unioshe, na nitakuwa mweupe kupita theluji. Unifanye kusikia furaha na shangwe, ili mifupa uliyovunja ifurahi. Ufiche uso wako usitazame zambi zangu, na uzima maovu yangu yote. Umba moyo safi ndani yangu, ee Mungu, na ufanye upya roho nzuri ndani yangu. Usinitenge na uso wako, wala usiondolee Roho yako mutakatifu. Unirudishie furaha ya wokovu wako, unitegemeze kwa roho ya tayari. Halafu nitafundisha wenye makosa njia zako, na wenye zambi watarudi kwako. Uniponyeshe na

damu ya watu, ee Mungu, wewe Mungu wa wokovu wangu, ulimi wangu utaimba na sauti haki yako. Ee Bwana, ufungue midomo yangu, na kinywa changu kitaonyesha sifa zako. Maana hupendezwi na zabihu, ao ningeitoa, hufurahi kwa sadaka ya kuteketezwa. Zabihu za Mungu ni roho ya kuvunjika, moyo uliovunjika na wa toba hutauzarau, ee Mungu. Utendee Sayuni mema kwa mapenzi yako, ujenge kuta za Yerusalema. Halafu utafurahi kwa zabihu za haki, kwa sadaka ya kuteketezwa, na sadaka nzima ya kuteketezwa, halafu watatoa ngombe ndume juu ya mazababu yako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Allilulia, allilulia, allilulia, utukufu kwako, ee Mungu. (*mara tatu*), Bwana hurumia (*mara tatu*).

Kisha tunasoma hii mwimbo:

Utukufu kwa Baba. . . Sauti ya sita.

Ee Bwana, wana wa Israeli walikuhukumu uuawe wewe uliye uzima wa ulimwengu wote; wao waliyovuka bahari Nyekunda na msaada wa bakora ya Musa, walikupigilia msalabani; wao waliyonyonya sali ya mwamba, pahali pa chakula walikupa nyongo; lakini uliteswa kwa kutaka kwako kusudi tuokolewe toka utumwa wa Adui. Utukufu kwako, ee Kristu Mungu wetu.

Sasa na siku zote. . . Theotokion.

Ee Mzazi-Mungu, ndiwe mzabibu wa kweli wenyi kuzidisha tunda la uzima. Tunakuomba: Utuombee, ee Malkia, pamoja na Mitume na Watakatifu wote, ili roho zetu zipate rehema.

Kisha tunaimba hii wimbo (Idiomela):

Sauti ya mnane.

Alipoogopa wa Yuda, Petro msaidizi na rafiki yako alikukana, wewe Bwana na kwa machozi akakulamikia: Usiache kukauka chemchem ya machozi yangu, kwani nilikuahidi kukuamini, lakini sikushika hii niliahidi. Ee Bwana, utupe na sisi toba ileile na utuhurumie.

Mara ingine hii wimbo, bila shairi.

Shairi: Ee Bwana, tega sikio kwa maneno yangu, sikiliza kulia kwangu.

Sauti ya mnane.

Ee Bwana, ma askari walicuhekelea mbele ya Msalaba wako heshimiwa, lakini majeshi ya mbinguni walishangaa; kwa maana ulizarauliwa wewe mwenye kupamba inchi kwa maua, na kwa zihaka ukavikwa nguo nyekundu, wewe mwenye kuvika mbingu kwa mawingu; lakini kwa tendo la wokovu, unafunua rehema yako; ee Bwana, utukufu kwako.

Shairi: Sikiliza sauti ya mwito wangu, ee Mfalme na Mungu wangu.

(*Mara ingine hii wimbo ya yulu*).

Utukufu kwa Baba. . . Sauti ya tano.

Ee Bwana, wakati wa Yuda walikusulubisha msalabani, ni kwa tendo langu gani munataka kunisulubisha msalabani? Ni sababu ya kuponyesha wagonjwa wetu wenye

kupooza, ao sababu ya kufufua wafu? Ni kwa nini munataka kuniua? Tazameni huyu mutachoma mkuki!

Sasa na siku zote. . . (*mara ingine hii wimbo*).

Prokimenon. Sauti ya mnane.

Kwa maana mimi ni karibu na kusita, , , na huzuni yangu ni mbele yangu daima.

Shairi: Ee Bwana, usinihamakie katika gazabu yako.

Unabii ya Nabii Isaya tutasoma. (50, 4-11).

Bwana Mungu amenipa ulimi wa wale wanaofundishwa, nipate kujua namna ninavyoweza kumusaidia kwa maneno yangu yule aliyechoka. Anania- msha asubui nyuma ya asubui, anaamsha sikio langu kusikia kama watu wanaofundishwa. Bwana Mungu amefungua sikio langu, na sikukataa wala sikurudi nyuma. Niliwatolea mugongo wangu wale wenye kupiga, na mashavu yangu wale wanaongoa ndevu; sikuficha uso wangu usipate haya na kutemewa mate. Lakini Bwana Mungu atanisaidia: kwa sababu hii sitapata haya; kwa sababu hii nimekaza uso wangu kamajiwe gumu, nami ninajua ya kuwa sitaona haya. Yeye anayenihesabu kuwa na haki ni karibu; ni nani atakayeshindana nami? Tusimame pamoja; ni nani aliye adui yangu? anikaribie. Tazama, Bwana Mungu atanisaidia; ni nani atakayenihukumu kuwa mukosaji? Tazama, wale wote watachakaa kama vazi; nondo atawakula. Ni nani katikati yenu anayeogopa Bwana, anayetii sauti ya mutumishi wake? anayetembea katika giza, wala hana nuru, aamini jina la Bwana, na ategemeo Mungu wako. Tazama, ninyi wote munaogonga moto, munaojifunga pande zote na mienge: mutembea katika nuru ya moto wenu, na katikati ya mlenge muliyowasha. Mutapata maneno haya kwa mukono wangu: mutalala kwa huzuli.

Matendo ya Mitume

Barua ya Mutume Paulo kwa wa Roma tutasoma.

Wa ndugu, kwa maana tungali tulipokuwa pasipo nguvu, kwa wakati wa kutimia, Kristu alikufa kwa ajili yao wasioogopa Mungu. Kwa maana ni ugumu kwa mutu kufa kwa ajili ya mutu wa haki; lakini inawezekana mutu kusubutu kufa kwa ajili ya mutu mwema. Lakini Mungu anaonyesha mapendo yake kwetu, wakati tulipokuwa tungali wenye zambi, Kristu alikufa kwa ajili yetu. Basi zaidi sana tukihesabiwa haki sasa kwa damu yake, tutaokolewa katika gazabu kwa yeye. Kwa maana, kama wakati tulipokuwa adui, tulipatanishwa na Mungu kwa kufa kwa Mwana wake; zaidi sana, nyuma ya kupatanishwa, tutaokolewa katika uzima wake.

EVANGELIO

Hekima; Inukeni tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.

Msomaji: Na kwa roho yako.

Somo ya Evangelio Takatifu ilionandikwa na Mwevangelizaji Marko, tusikilize.

Msomaji: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

Padri:

Katika Mwevangelizaji Marko. (15, 16-32)

Nao askari walimuchukua ndani ya kiwanja ndiyo Praitorio, wakakusanya pamoja kikosi kizima. Wakamuvika vazi jekundu, wakasokota taji ya miiba, wakamutia kichwani. Wakaanza kumusalimu: Salamu, Mufalme wa Wayuda! Wakamupiga kichwani kwa muti, wakamutemea mate, wakapiga magoti, wakamwabudu. Hata walipokwisha kumuchekea, wakamwondolea nguo nyekundu, wakamuvika mavazi yake mwenyewe, wakamuchukua inje ili wamusulibishe. Walishurutisha mutu aliyepita akitoka mashamba, Simoni Mukurene, baba ya Alesandro na Rufu, ili achukue musalaba wake. Wakamuleta hata pahali palipoitwa Golgota, maana yake: Mufupa wa kichwa. Wakamupa mvinyo iliyotiwa manemane, lakini yeye hakuipokea. Wakamusulibisha, wakagawa mavazi yake, wakiyapigia kura, kila mutu atwae nini. Ilikuwa saa tatu, nao walimusulibisha. Maandiko ya mashitaki yake yaliandikwa juu: Mufalme wa Wayuda. Pamoja naye wakasulibisha wanyanganyi wawili, mumoja mukono mwake wa kuume, na mumoja mukono wake wa kushoto. (Basi andiko likatimizwa linalosema: Alihesabiwa pamoja na wenye kuasi). Nao waliopita walimutukana wakitikisisha vichwa vya wakisema: Ha! wewe mwenye kuvunja hekalu na kulijenga katika siku tatu! Ujiokoe wewe mwenyewe, ushuke musalabani! Vile wakubwa wa makuhani wakamuzihaki wao kwa wao pamoja na waandishi, wakasema: Aliokoa wengine, hawezi kujiokoa yeye mwenyewe. Kristo, mufalme wa Israeli, ashuke sasa musalabani, tupate kuona na kuamini. Hata wale waliosulibiwa pamoja naye wakamutukana. Ilipokuwa saa sita, giza lilikuwa juu ya inchi yote hata saa tisa. Na saa tisa Yesu alipaza sauti kubwa: Eloi, Eloi, lama sabaktani: maana yake: Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini umeniacha? ao waliosimama pale wali-sema: Tazama anaita Elia. Na mumoja alikwenda mbio, akajaza sifongo siki, akaitia juu ya muti, akamunywesha, akisema: Acheni, tuone kama Elia atakuja kumushusha. Yesu akatoa sauti kubwa, akatoa roho. Pazia la hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini. Yule akida aliyesimama mbele yake, wakati alipoona alikata roho namna hii, akasema: Hakika mutu huyu alikuwa Mwana wa Mungu. Wanawake walikuwa pale vilevile wakitazama kwa mbali; katika hawa walikuwa Maria Magdalene, na Maria mama ya Yakobo mudogo, na Yose na Salome. Hawa ndio waliomufuata na kumutumikia wakati alipokuwa katika Galilaya; na wengine wengi waliokwenda pamoja naye hata Yerusalema.

Kisha msomaji anasoma:

Ahimidiwe Bwana wetu, ahimidiwe Bwana siku kwa siku. Mungu huyu anatuletea wokovu. Mungu wetu ni Mungu mwenye kuokoa.

Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utukufu. . . Sasa. . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

Kisha tunasoma Kontakion:

Sauti ya mnane

Kujeni wote tumwinamie huyu aliyesulubiwa kwa ajili yetu; Mzazi-Mungu alipomuona msalabani akamwambia: Wewe mwenye kuteswa na hii lufu, ndiwe kweli Mwana wangu na Mungu wangu.

Kisha tunasema: Bwana hurumia, (mara makumi ine) na hii sala: Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa. . .(Ona ukurasa 5).

Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia. Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . . Uliye wathamani. . . Kwa jina la Bwana barikia, ee padri:

Mungu atufazili na kutubariki, atuangazie uso wake na kutuhurumia.

Padri anasoma hii sala:

Mungu, Rabi, Baba Mwenyezi; Mwokozi, Mwana wa pekee, Yesu Kristu na Roho Mtakatifu, umungu moja, nguvu moja, unihurumie; wakati wa mwisho uniokoe mimi mukoosifu wako, kwani unabarikiwa milele na milele. Amina.

SAA WA SITA

Musomaji anasoma mara moja:

Njooi tumwinamie na tumsujudu Mungu na Mfalme wetu.

Njooi tumwinamie na tumsujudu Kristu Mfalme wetu.

Njooi tumwinamie na tumsujudu Yeye Kristu aliye Mfalme wetu.

Zaburi 53 (54).

Uniokoe, ee Mungu, kwa jina lako, na unihukumu kwa uwezo wako. Sikia maombi yangu, ee Mungu, usikilize maneno ya kinywa changu. Kwa maana wageni wamesimama juu yangu, na watu wakali wametafuta nafsi yangu, hawakuweka Mungu mbele yao. 4 Tazama, Mungu ni musaidia wangu; Bwana ni kati yao wanaotegemeza nafsi yangu. Atarudishia adui zangu ubaya wao, uwaharibu kwa kweli yako. Nitakutolea sadaka ya moyo, nitashukuru jina lako, ee Bwana, maana ni jema. Kwa kuwa ameniokoa toka taabu zote, na jicho langu limeona mapenzi yangu juu ya adui zangu.

Zaburi 139 (140).

Uniokoe, ee Bwana, na mutu mubaya; Unichunge na mutu wa Jeuri: Wanaowaza mabaya moyoni mwao; Kila siku wanakusanyika kwa vita. Wametia ulimi wao mukali kama nyoka; Sumu ya fira ni chini ya midomo yao. Unilinde, ee Bwana, na mikono ya mwovu; Unichunge na mutu wa jeuri: Walioshauri kugeuza hatua zangu. Wenye kiburi wamenifichia mutego na kamba; Wametandika wavu kando ya njia; Wameniwekea matanzi. Nimemwambia Bwana: Wewe ni Mungu wangu; Usikie sauti ya kusihi kwangu, ee Bwana. Ee Mungu Bwana, nguvu ya wokoyu wangu, umefunika kichwa changu katika silu ya vita. Usimupe mwovu tamaa zake, Ee Bwana; Usiendeleze shauri lake baya: wasijikuze. Lakini kwa maneno ya kichwa chao wanaonizungusha, hasara ya midomo yao wenyewe iwafunike. Makaa ya moto yawaangukie: Watupwe katika moto; Katika mashimo wasipate kusimama tena. Musingizaji hatawekwa imara katika inchi: Uovu utawinda mutu wa jeuri na kumwanganlza. Ninajua ya kuwa Bwana atategemeza wale wanaoteswa, na kuwapa wenye hitaji haki yao. Hakika wenye haki watashukuru jina lako: Wenye adili watakaa mbele ya uso wako.

Zaburi 90 (91).

Yeye anayekaa kwa pahali pa maficho yake aliye juu atakaa chini ya kivuli cha Mwenyezi. Nitasema juu ya Bwana, yeye ni pahali pangu pa kukimbilia na boma la nguvu langu, Mungu wangu ninayemwamini. Kwa maana atakuokoa toka mutego wa muwindaji ndege, na kwa tauni ya uharibifu. Na manyoya yake atakufunika. Na chini ya mabawa yake utakimbilia, kweli yake ni ngabo na kigabo. Hutaogopa kwa woga wa usiku, wala kwa mushale unaoruka muchana; kwa tauni inayotembea katika giza, wala kwa kuharibu kunakoharibu azuhuri, elfu moja wataanguka kando yako, na elfu kumi kwa mukono wako wa kuume; lakini hakutafika karibu nawe. Na macho yako tu utatazama, na kuona zawabu ya waovu. Maana wewe, ee Bwana, ni pahali pangu pa kukimbilia! Umefanya aliye juu kao lako; mabaya hayatakupata wewe wala tauni haitafika na hema yako. Maana ataagiza malaika yake juu yako, wakuchunge katika njia zako zote. Watakuchukua juu mikononi mwao, usivunje muguu wako kwa jiwe. Utakanyaga simba na nyoka mudogo mwenye sumu, utakanyaga mwana-simba na joka. Kwa sababu ametia mapendo yake juu yangu, kwa hivi nitamuponyesha. Nitamuweka juu kwa sababu amejua jina langu. Ataniita na nitamujibu; nitakuwa pamoja naye katika taabu; nitamuponyesha na kumuheshimu. Kwa maisha ndefu nitamushibisha, na kumwonyesha wokovu wangu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Allilulia, allilulia, allilulia, utukufu kwako, ee Mungu. (*mara tatu*), Bwana hurumia (*mara tatu*).

Kisha tunasoma hii mwimbo:

Utukufu kwa Baba. . . Sauti ya sita.

Ee Bwana, wana wa Israeli walikuhukumu uuawe wewe uliye uzima wa ulimwengu wote; wao waliyovuka bahari Nyekunda na msaada wa bakora ya Musa, walikupigilia msalabani; wao waliyonyonya sali ya mwamba, pahali pa chakula walikupa nyongo; lakini uliteswa kwa kutaka kwako kusudi tuokolewe toka utumwa wa Adui. Utukufu kwako, ee Kristu Mungu wetu.

Sasa na siku zote. . . Theotokion.

Kwani hatuna matumaini hata moja sababu ya zambi zetu nyingi, umwombe huyu aliyezaliwa kwako, ee Bikira Mzazi-Mungu. Maana ni la nguvu, ombi la Mama kwa kupata neema ya Rabi. Usizarau maombi ya wenye zambi, ewe Mtukufu kamili, kwa kuwa yeye ni mwenye rehema na Mweza kwa kuokoa, huyu aliyekubali kuteswa mwilini kwa ajili yetu.

Kisha tunaimba hii wimbo:

Sauti ya mnane.

Bwana anasema: Ee taifa langu, nimekutendea nini? Kwa nini nimekusikitisha? Niliponyesha vipofu wako, nilitakasa wagonjwa wako wenye ukoma, niliamusha mwenye pupooza kitandani mwake; ee taifa langu, nimekutendea nini? Unanirudisha nini? Pahali pa mkate umenipa nyongo, pahali pa maji ya mwamba umenipa siki, sababu ya mapendo yangu umenisulubisha msalabani; hata mara moja hautakuwa taifa langu teule, nitaita mataifa watanitukuza pamoja na Baba na Roho Mtakatifu na nitawapa uzima wa milele.

Shairi: Pahali pa chakula walinipa nyongo, kwa kiu yangu walininywisha siki. (*Mara ingine hii ya yulu*).

Sauti ya mnane.

Mitume wanawaambia waalimu wa Sheria: Enyi Waandishi na wa Farisayo, oneni Hekalu muliobomoa; oneni Mwana-kondoo wa Mungu mulisulubisha msalabani, mulimuweka kaburini lakini kwa uwezo wake alifufuka! Ni yeye aliyewaokoa ninyi katika Bahari Nyekundu, ni Yeye aliwalisha ninyi katika jangwa, ni yeye mwenye kuleta uzima, nuru na amani duniani.

Shairi: Uniokoe, ee Mungu, kwani maji yameingia mpaka rohoni.

(mara ingine hii ya yulu).

Utukufu kwa Baba. . . Sauti ya tano.

Kujeni, enyi wa Kristu, oneni fitina ya mtoaji Yudasia pamoja na makuhani makafiri juu ya Kristu Mwokozi wetu: Leo wamemua Neno msiyekufa wakati walimutoa kwa Pilato kusudi asulubiwe; na kule Kalvario aliteswa Mwokozi wetu alisema: Ee Baba, uwasamehe hii kosa kusudi mataifa yote wajue ufufuo wangu katika wafu.

Prokimenon. Sauti ya Ine.

Ee Bwana, Mungu wetu, jina lako ni kubwa duniani kote.

Shairi: Kwa maana utukufu wako inapanda yote.

Unabii ya Nabii Isaya tutasoma. (52, 13-54, 1)

Tazama, mutumishi wangu atafanya kwa akili; atatukuzwa na kunya-nyuliwa juu, naye atakuwa juu sana. Kama vile wengi walishangaa juu yako, (uso wake ulikuwa umeharibiwa sana zaidi ya mutu ye yote, na sura yake zaidi ya watoto wa watu), ndivyo atashitusha mataifa mengi; wafalme watamufungia vinywa vyao; maana maneno wasiyoambiwa watayaona, na maneno wasiyoyasikia watafahamu.. Ni nani aliyeamini habari zetu? Na mukono wa Bwana amefunuliwa nani? Maana atakua mbele yake kama chipuko, na kama shina katika inchi kavu; Yeye hana sura wala uzuri, na wakati tunapomwona hana uzuri hata tumutamani. Amezarauliwa na kukataliwa na watu; mutu wa huzuni, na mwenye kujua taabu: Na kama mutu watu wanayemufichia nyuso zao, alizarauliwa, na hatukumuhesabu kuwa kitu. Kweli amechukua taabu zetu, na amebeba huzuni zetu; lakini tulimwona akipigwa, Akiteswa na Mungu, na kuhuzunishwa. Lakini aliumizwa kwa makosa yetu, alichubuka kwa maovu yetu, azabu ya salama yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo tumepeotea; tumegeuka kila mumoja kwa njia yake mwenyewe na Bwana ameweka juu yake Maovu yetu sisi sote. Alionewa na aliteswa, lakini hakufungua kinywa chake; kama mwana-kondoo anayepelekwa kuchinjwa, na kama kondoo anavyonyamaza mbele yao wanaokata manyoya yake; Hakufungua kinywa chake. Aliondolewa kwa kuonewa na kuhukumikiwa, na kwa kizazi chake, nani aliyewaza ya kuwa Amekatiliwa mbali na inchi ya walio hai; alipigwa kwa sababu ya makosa ya watu wangu. Wakamufanyia kaburi pamoja na waovu; na pamoja na matajiri katika kufa kwake; hata yeye hakuranya jeuri, wala hila haikuonekana kinywani mwake, Hata hivi ilipendeza Bwana kumuchubua; amemuhuzunisha. Wakati utakapotolea nafsi yake kuwa zabihu kwa zambi, ataona uzao wake, atazidisha siku zake, na mapenzi ya Bwana yatasitawi katika mukono wake. Ataona ya taabu ya nafsi yake, naye atatulia: Kwa maarifa yake mutumishi wangu mwenye haki atawafanya wengi kuwa wenye haki: Naye

atachukua maovu yao. Kwa sababu hii nitamugawia sehemu pamoja na wakubwa, naye atagawa nyara pamoja na wahodari, kwa sababu alimwanga nafsi yake hata kufa. Akahesabiwa pamoja na wale wenye kukosa. Na alichukua zambi za watu wengi, na kuombea wenye kukosa. Imba, wewe uliye tasa, wewe usiyezaa; paza sauti yako kwa kuimba, piga kelele kwa furaha, wewe usiye kuwa na uchungu wa kuzaa; maana watoto wāke aliyeachwa ni wengi kuliko watoto wake aliye na mume, Bwana anasema.

Matendo ya Mitume

Barua ya Mtume Paulo kwa wa Ebrania tutasoma.

Wa Ndugu, maana mwenye kutakasa, nao wenye kutakaswa wote pia wanataka kwa mumoja. Kwa sababu hii haoni haya kuwaita ndugu zake, akisema: Nitahubiri jina lako kwa ndugu zangu; katikati ya kanisa nitakuambia sifa. Na tena: Nitaweka imani yangu ndani yake. Na tena: Tazama, mimi pamoja na watoto niliopewa na Mungu. Basi, kwa sababu watoto wameshiriki damu na mwili, yeye mwenyewe vivyo hivyo alishiriki kama wao, hata kwa njia ya kufa apate kuharibu yeye aliyekuwa na nguvu za kufa, ndiye Shetani, na kuwafungua wale wote waliokuwa maisha yao yote katika hali ya utumwa, kwa woga wa mauti. Maana ni hakika, hatwai asili ya malaika, lakini anatwaa asili ya mazao ya Abrahamu. Kwa hivyo ilimupasa kufananishwa na ndugu zake katika maneno yote, apate kuwa kuhani mukubwa mwenye rehema na mwaminifu katika mambo ya Mungu kusudi afanye upatanisho kwa zambi za watu. Na kwa kuwa yeye mwenyewe aliteswa wakati alipojaribiwa, anaweza kusaidia wale wanaojaribiwa.

EVANGELION

Hekima; Inukeni tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.

Msomaji: Na kwa roho yako.

Somo ya Evangelio Takatifu ilionandikwa na Mwevangelizaji Luka, tusikilize.

Msomaji: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

Padri:

Katika Mwevangelizaji Luka (23, 32-49)

Na wawili wengine, watenda mabaya, walipelekwa pamoja naye kuuawa. Wakati walipofika pahali palipoitwa Mufupa wa Kichwa, kule walimusulibisha, na wale watenda mabaya, mumoja kwa mukono wa kuume, na mumoja kwa mukono wa kushoto. Yesu akasema: Baba, uwasamehe, kwa sababu hawajui neno wanalolifanya. Wakigawanya nguo zake, wakapiga kura. Watu wakasimama wakitazama. Lakini wakubwa wakamuzihaki, wakisema: Alikoa wengine, ajiokoe yeye mwenyewe kama yeye ni Kristo wa Mungu, Muchaguliwa. Askari vilevile wakamuzihaki, wakakuja kwake wakimupa siki, na kusema: Kama wewe ni mufalme wa Wayuda ujiokoe wewe mwenyewe. Na maandiko yaliandikwa juu yake kwa maandiko ya Kiyunani na Kiroma na ya Kiebrania, Huyu ni Mufalme wa Wayuda. Mumoja wa wale watenda mabaya waliotundikwa pamoja naye akamutukana, akisema: Si wewe uliye Kristo? Ujiokoe mwenyewe pamoja nasi. Lakini wa pili akamuhamakia, akisema: Huogopi hata Mungu, maana wewe ni katika hukumu ile ile? Na sisi kwa kweli, sababu tunapokea malipo yanayostahili kwa matendo yetu, lakini mutu huyu hakufanya neno lisilofaa.

Akamwambia Yesu: Bwana, unikumbuke wakati unapokuja katika ufalme wako. Yesu akamwambia: Kweli ninakuambia, leo utakuwa pamoja nami katika Paradiso. Ilikuwa karibu na saa sita azuhuri, na giza lilikuwa juu ya inchi yote hata saa tisa; jua lilipunguka; pazia la hekalu likapasuka katikati. Yesu alipolia kwa sauti kubwa, akasema: Baba, katika mikono yako ninaweka roho yangu; na alipokwisha kusema maneno haya akatoa roho. Mukubwa wa askari, alipoona maneno haya, akatukuza Mungu akisema: Kweli mutu huyu alikuwa mwenye haki. Na makutano yote waliokusanyika kuangalia maneno haya, walipotazama maneno yaliyofanyika, wakarudi wakipigapiga vifua vyao. Rafiki zake zote na wanawake waliofuatana naye toka Galilaya, wakasimama mbali, wakiangalia maneno haya.

Kisha msomaji anasoma:

Huruma yako itufikie upesi, kwani tumetaabika sana. Utusaidie, ee Mungu Mwokozi wetu, kwa ajili ya utukufu wa jina lako. Utuokoe, utusamehe zambi zetu kwa ajili ya jina lako.

Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utukufu. . . Sasa. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

Kisha tunasoma Kontakion:

Sauti ya mnane

Kujeni wote tumwinamie huyu aliyesulubiwa kwa ajili yetu; Mzazi-Mungu alipomuona msalabani akamwambia: Wewe mwenye kuteswa na hii lufu, ndiwe kweli Mwana wangu na Mungu wangu.

Kisha tunasema: Bwana hurumia, (mara makumi ine) na hii sala: Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa. .. (Ona ukurasa 5).

Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia. Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . . Uliye wathamani. . . Kwa jina la Bwana barikia, ee padri:

Mungu atufazili na kutubariki, atuangazie uso wake na kutuhurumia.

Padri atasoma hii sala ya Mtakatifu Basile Mukubwa.

Ee Mungu na Bwana wa majeshi, fundi wa kiumbe yote, kwa mapendo ya rehema yako isiyoweza kufananishwa, ulimtuma Mwana wako wa pekee, Bwana wetu Yesu Kristu, kwa ajili ya wokovu wa wanadamu. Ulizima ile barua ya deni zetu, kwa msalaba wake tukufu na ulishinda, katika hii, ufalme na nguvu za giza. Wewe mwenyewe, ee Rabi, mpenda-wanadamu, utupokee sisi wenye zambi; pokea shukrani zetu na maombi yetu. Utuopoe ku kosa yote yenye kuzuru na ya giza na kwa wale wote wenyi kutafuta kutuzuru, maadui wenye kuonekana na wasioonekana. Toboa mwili wetu na woga wako, usiinamisha mioyo yetu ku maneno wala ku mawazo mabaya, lakini umiza mioyo yetu ku mapendo yako ili wakati wote macho yenye kukaza kwako, na tukiongozwa na nuru isiyokaribika na ya milele, na kukutolea utukufu na shukrani, Baba wasipo mwanzo, pamoja na Mwana wako wa pekee na Roho wako Mtakatifu kamili, mwema na mletaji uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SAA WA TISA

Msomaji mara moja anasoma: Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . . Bwana hurumia (*mara kumi na mbili*), Njoooni tumwinamia. .

Kisha anasoma:

Zaburi 68 (69)

Uniokoe, ee Mungu; Maana maji yamefika katika nafsi yangu. Ninazama katika matope mengi pahal, i pasipo wezekana kusimama; Nimefika katika maji ya vilindi, pahali maji yanaponigarikisha. Ninachoka kwa kulia kwangu; shingo langu limekauka; Macho yangu hayaoni ningali ninangojea Mungu wangu. Wao wanaonichukia pasipo sababu ni wengi kuliko nyole za kichwa changu; wao wanaotaka kunikatia mbali, wakiwa adui zangu pasipo hakl ni wenye uwezo; halafu nilipaswa kurudisha vitu nisivyovichukua. Ee Mungu, anajua upumbafu wangu; na zambi zangu hazifichwi mbele yako. Usiache wao wanaokungojea kupata haya kwa ajili yangu, ee Bwana Mungu wa majeshi; usiache wale wanaokutafuta kuzarauliwa kwa ajili yangu, ee Mungu wa Israeli. Maana kwa ajili yako nimevumilia laumu; haya imefunika uso wangu. Nimekuwa mugeni kwa ndugu zangu, nisiyepatana na watoto wa mama yangu. Maana wivu wa nyumba yako umenkula; Na laumu zao wanaonilaumu zimeniangukia, wakati nilipotoa machozi na kuazibu roho yangu kwa kufunga, Ilikuwa laumu juu yangu. Wakati nilipovaa gunia, nilikuwa mufano kwao, wao wanaoketi langoni wanasomezana juu yangu; nami ni wimbo wa walevi. Lakini mimi, maombi yangu ni kwako, ee Bwana, kwa wakati unaokubaliwa; ee Mungu, kwa wingi wa rehema yako, unijibu katika kweli ya wokovu wako. Uniponyeshe kwa kunitoa toka matope, wala usiache kuzama; uniokoe nao wanaonichukia, na katika vilindi vya maji. Usiache maji kunigarikisha, wala kilindi kunimeza; wala shimo lisifunge kinywa chake juu yangu. Unijibu, ee Bwana; maana uzuri wako ni wema; kwa kadiri ya wingi wa rehema zako ugeuke kwangu. Wala usifiche uso wako kwa mutumlshl wako; Kwa sababu mimi ni katika taabu; unijibu mbio. Ukaribie nafsi yangu, na kuikomboa; Unikomboa kwa sababu ya adui zangu. Wewe unajua laumu yangu, na haya yangu, na kuzarauliwa kwangu; watesi wangu ni wote mbele yako. Laumu imenivunja moyo; nami ninaugua sana; Nikatafuta mwenye kunihurumia, lakini hakuna mutu; na kwa wenye kunifariji, lakini sikipata. Wakanipa nyongo vilevile, kuwa chakula changu; Na kwa kiu yangu wakanikunyweshia siki. Meza yao mbele yao iwe mutego; na wakiwa na salama, iwe shabaki. Macho yao yatiwe giza, wasione; na viuno vyao uvitetemeshe daima. Mwanga gazabu yako juu yao, na ukali wa kasirani yako uwapate. Kao lao liwe ukiwa; pasipo na mutu kukaa hemani mwao. Maana wanatesa mutu wewe uliyemupiga; Na wanapasha huzuni yao uliowaumiza. Ongeza uovu juu ya uovu wao; wala wasiingie katika haki yako. Waondolewe katika kitabu cha uzima, wasiandikwe pamoja na wenye haki. Lakini mimi ni masikini na mwenye huzuni; wokovu wako, ee Mungu, uninyanyue. Nitasifu jina la Mungu kwa wimbo, na kumutukuza na kushukuru. Na itapendeza Bwana kuliko ngombe ndume, ao ndama mwenye pembe na kwato. Wapole waliona na wanafurahi; ninyi munaotafuta Mungu, moyo wenu uishi. Kwa kuwa Bwana anasikia

wenye hitaji, wala hazarau mufungwa wake. Mbingu na inchi zimusifu, Bahari na kila kitu kinachotembea ndani yake. Maana Mungu ataokoa Sayuni na kujenga miji ya Yuda; nao watakaa pale na kuiriti. Wazao wa watumishi wake watairiti vilevile; nao wanaopenda jina lake watakaa ndani yake.

Zaburi 69 (70).

Ee Mungu, uniokoe; Unisaidie mbio, ee Bwana. Wapate haya na kufazaishwa Wanaotafuta nafsi yangu; Warudishwe nyuma na kuzarauliwa Wanaofurahi kwa kumia kwangu. Warudishwe nyuma kwa ajili ya haya yao Wanaosema: Ewe, ewe. Wote wanaokutafuta washangilie na kukufurahia; Nao wanaopenda wokovu wako waseme daima: Mungu atukuzwe. Lakini mimi ni masikini na mwenye hitaji; Unisaidie mbio, ee Mungu; Wewe ni musaidia wangu na mwokozi wangu; Ee Bwana, usikawie.

Zaburi 85 (86).

Uiname sikio lako, ee Bwana, unijibu; Maana mimi ni masikini na mwenye hitaji. Chunga nafsi yangu maana mimi ni mwema; Ee wewe Mungu wangu, ponyesha mutumishi wako anayekutumainia. Unirehemu, ee Bwana; Maana kwako ninalia muchana kutwa. Furahisha nafsi ya mutumishi wako; Maana kwako, ee Bwana, ninanyanyua nafsi yangu. Kwani wewe, Bwana, ni mwema, na tayari kusamehe, ukijaa rehema kwa wote wanaokuomba. Sikia, ee Bwana, maombi yangu; Na sikiliza sauti ya kuomba kwangu. Kwa siku ya taabu yangu nitaomba kwako, kwani utanjibu: Hakuna mwingine katika miungu kama wewe, ee Bwana, Wala hakuna kazi kama kazi zako. Mataifa yote uliyofanya watakuja na kuabudu mbele yako, ee Bwana; na watatukuza jina lako. Kwa kuwa wewe ni mukubwa, na unafanya maajabu; wewe pekee ni Mungu. Unifundishe njia yako, ee Bwana; nitatembea katika kweli yako; Ufunganishe moyo wangu kuogopa jina lako. Nitakusifu, ee Bwana Mungu wangu, na moyo wangu wote, na nitatukuza jina lako kwa milele. Maana rehema yako ni kubwa kwangu, Na umeponyesha nafsi yangu toka Hadeze ya chini kabisa. Ee Mungu, wenye majivuno wamesimama juu yangu, na makutano ya wenye jeuri wametafuta nafsi yangu, wala hawakukuweka wewe mbele yao. Lakini wewe, ee Bwana, ni Mungu anayejaa huruma na neema, Muvumilivu, mwenye rehema na kweli nyingi. Ugeuke kwangu na kunirehemu; umupe mutumishi wako nguvu yako, na kuponyesha mwana wa kijakazi chako. Unionyeshe alama kwa wema; hata wao wanaonichukia wapate kuiona na kuhayarishwa, kwa kuwa wewe, Bwana, umenisaidia, na kunifariji.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Allilulia, allilulia, allilulia, utukufu kwako, ee Mungu. (*mara tatu*), Bwana hurumia (*mara tatu*).

Kisha tunasoma hii mwimbo:

Utukufu kwa Baba. . . Sauti wa mnane.

Alipoona Mfalme wa uzima ametundikwa msalabani, Munyanganyi akapaza sauti kwa imani. Kama huyu anasulubiwa pamoja na sisi hakuna Mungu aliyejifanya mutu, jua halingalificha nuru yake wala inchi kutetemeka kwa woga; na wewe mwenye kuvumilia hii yote, unikumbuke, ee Bwana, katika ufalme wako.

Sasa na siku zote. . . Theotokion.

Wewe uliyezaliwa kwa Bikira kwa ajili yetu, na uliyevumilia usulubisho, ee Mwema, uliyenyaganya mauti kwa lufu, na uliyeonyesha usimamao sawasawa na Mungu, usikengue walioubwa kwa mukono wako; onyesha mapendo yako kwa wanadamu, murehemu; pokea Mzazi-Mungu aliyekuzaa, aliyepatanisha juu yetu, na okoa, ee Mwokozi wetu, taifa isiyotumainia.

Kisha tunaimba hii wimbo:

Sauti ya saba.

Wakati yaliona Muumba wao ametundikwa msalabani, mbingu na dunia: Jua lilificha nuru yake na giza ikawa, wafu walifufuka kaburini. Pamoja na viumbe vyote tunasujudu mbele yako: Ee Bwana, utuokoe.

Shairi: Waligawanya mavazi yangu, walipigia kura kanzu yangu.

(mara ingine hii)

Sauti wa mbili.

Ee Bwana, wakati makafiri walikusulubisha msalabani, ukawaambia: Kwa nini niliwasikitisha ili musirike? Nani kupita mimi aliwaokoa ninyi toka mateso? Sasa nini munanirudishia? Ubaya kwa uzuri; pahali pa nguzo ya moto munanipingilia msalabani; pahali pa wingu munachimba kaburi yangu; pahali pa mkate munanipa nyongo; na pahalii pa maji wa mwamba munaninywisha siki! Tangu leo nitaita mataifa kusudi wanitukuze pamoja na Baba na Roho Mtakatifu.

Shairi: Pahali pa chakula walinipa nyongo, kwa kiu yangu wameninywisha siki. *(mara ingine hii)*.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Sauti wa sita.

Hii wimbo musomaji ataisoma kati ya Kanisa na kisha kundi ya waimbaji wataimba pamoja ku fasi yao.

Leo ametundikwa msalabani huyu aliyetundika inchi juu ya maji. *(mara tatu)*.

Mfalme wa malaika anavikwa taji ya miiba,

anavikwa kanzu ya zihaka yeye aliyevika mbingu kwa mawingu;

Huyu aliyekomboa Adamu katika Yordani anaitika mapigo na makofi;

Bwana wa Eklezya anatobolewa misumari;

Mwana wa Bikira anachomwa mkuki.

Ee Kristu, tunaabudu Mateso yako. *(mara tatu)*.

Utuonyeshe Ufufuo wako takatifu.

Prokimenon. Sauti wa sita.

Mupumbafu amesema moyoni mwake: hakuna Mungu.

Shairi: Hakuna mumoja anayetenda mema.

Unabii ya Nabii Yeremia tutasoma.

Tena Bwana akanijulisha maneno haya, nami ninakajua; halafu ulinionyesha matendo yao. Lakini mimi nilikuwa kama mwana-kondoo mupole anayechukuliwa kwenda kuchinjwa; wala sikujua ya kuwa wamefanya mashauri juu yangu, wakisema: Tuharibu muti pamoja na matunda yake, na tumukatilie mbali atoke katika inchi ya walio hai, ili jina lake lisikumbukwe tena. Lakini, ee Bwana wa majeshi, unayehukumu haki, unayejaribu viuno na moyo, nione malipizo yako juu yao; kwa maana nimekufunulia wewe neno langu. Basi ndivyo anavyosema Bwana juu ya watu wa Anatoti, wanaotafuta uhal wako, wakisema: Usifanye unabii kwa jina la Bwana, usife kwa mukono wetu, kwa sababu hii Bwana wa majeshi anasema hivi: Tazama, nitawaazibu watu hawa; vijana watakufa kwa upanga; wana wao na binti zao watakufa kwa njaa; wala hapatakuwa na mutu atakayebaki kwao; maana nitaleta mabaya juu ya watu wa Anatoti, mwaka wa kuangaliwa kwao. Wewe ni mwenye haki, ee Bwana, wakati ninapoulizana nawe, lakini nitasema nawe katika habari za haki. Kwa nini njia ya wabaya inasitawi? Kwa nini wote wanaotenda hila wanakaa salama? Umewapanda, hata wametia mizizi. wanasitawi, mupaka wanazaa matunda; katika vinywa vyao wewe ni karibu, lakini katika mioyo yao wewe ni mbali. Lakini wewe, Bwana, unanijua mimi; umeniona, umejaribu moyo wangu, namna unavyokutegemea; uwakokote kama kondoo wanaokwenda kuchinjwa, uwaweke tayari kwa siku ya kuchinjwa. Hata wakati gani inchi itaomboleza, na majani ya inchi yote kukauka? Kwa ajili ya mabaya yao wanaokaa ndani yake, nyama wameangamia na ndege pia; kwa sababu walisema: Hataona mwisho wetu. Kama ikiwa umepiga mbio pamoja nao wanaokwenda kwa miguu, nao wamekuchokeza, basi unaweza namna gani kushindana na farasi? Na hata katika inchi ya utulivu wewe una salama, utafanya nini hapa katika mafuriko ya Yorodani? Uriti wangu umekuwa kwangu kama ndege, mwenye madoadoa, ndege wakali wanamuzunguka pande zote; kwendeni, kusayeni pamoja nyama zote za poli, munalete ile wale. Wachungaji wengi wameharibu shamba langu la mizabibu, wakakanyaga fungu langu chini ya miguu yao, wamefanya fungu langu zuri kuwa jangwa la ukiwa. Wamelifanya kuwa ukiwa, na kwa kuwa ni ukiwa linanililia; inchi yote imefanywa kuwa ukiwa, kwa sababu hapana mutu aliyeweka maneno haya moyoni mwake. Bwana anasema hivi juu ya jirani zangu walio wabaya, wanaogusa uriti wangu nilioritisha watu wangu Israeli. Tazama, nitawangoa katika inchi yao, nami nitangoa nyumba ya Yuda isiwe kati yao. Tena itakuwa, nyuma ya kuwangoa, nitarudi na kuwahurumia; nami nitawaleta tena, kila mutu aingie katika uriti wake, na kila mutu aingiea katika inchi yake.

Matendo ya Mitume.

Barua ya Mtume Paulo kwa wa Ebrania tutasoma.

Basi, ndugu kwa sababu tuna uhodari wa kungia pahali Patakatifu kwa damu ya Yesu, njia ile aliyoanza kwa ajili yetu, mpya na hai, katika pazia, ndio mwili wake; na tukiwa na kuhani mukubwa juu ya nyumba ya Mungu; tukaribie kwa moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, mioyo yetu ikikwisha kunyunyiziwa kwa kuacha zamiri mbaya, na miili yetu kuoshwa kwa maji safi. Tushike sana kukiri kwa tumaini letu, kusudi lisigeuke; maana

yeye aliyeahidi ni mwaminifu; na tuangaliane kwa njia ya kusukumana katika mapendo na kazi nzuri; tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; lakini tukionyana, zaidi sana munavyoona siku ile inakaribia. Maana kama tukifanya zambi kusudi nyuma ya kupokea kujua kwa kweli, haibaki tena zabibu kwa ajili ya zambi; lakini kutazamia hukumu kwa woga, na ukali wa moto ulio tayari kula adui. Mutu aliyezarau sheria ya Musa alikufa pasipo huruma kwa neno la washuhuda wawili ao watatu. Munazania nini? Haikupasa azabu kubwa zaidi kwa mutu yule aliyekanyaga Mwana wa Mungu, na kuhesabu damu ya agano aliyotakaswa nayo kuwa kitu kichafu, na kutukana Roho ya neema? Maana tunamujua yeye aliyesema: Malipizi kisasi ni juu yangu, mimi nitalipa. Na tena: Bwana atahukumu watu wake. Ni neno la kuogopa kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai.

EVANGELION

Hekima; Inukeni tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.

Msomaji: Na kwa roho yako.

Somo ya Evangelio Takatifu ilionandikwa na Mwevangelizaji Yoane, tusikilize.

Msomaji: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

Padri:

Basi askari, wakati waliposulibisha Yesu, wakatwaa mavazi yake, wakayatenga sahemu ine, kwa askari sahemu moja; na kanzu yake vilevile; na kanzu ile haikushonwa, imesukwa pia toka juu hata chini. Basi wakasemezana: Tusiipasue, lakini tuipigia kura, itakuwa ya nani; andiko litimizwe linalosema: Waligawanya nguo zangu katikati yao na vazi langu walilipigia kura. Basi maneno haya waliyofanya askari. Lakini karibu na musalaba wa Yesu alisimama mama yake, na ndugu muke ya mama yake, Maria mwanamuke wa Kleopa, na Maria Magdalene. Basi wakati Yesu alipoona mama yake, na yule mwanafunzi mupendwa akisimama karibu, akamwambia mama yake: Mwanamuke, tazama mwana wako! Halafu akamwambia yule mwanafunzi: Tazama, mama yako. Na kutoka saa ile mwanafunzi yule alimupeleka kwake. Nyuma ya maneno haya, Yesu akijua ua kama maneno yote yamekwisha kumalizwa, ili andiko litimizwe, akasema: Nini kiu. Palikuwa kule chombo kimejaa siki; wakajaza sifongo na siki, wakatia juu ya hisopo, wakatia kwa kinwa chake. Basi wakati Yesu alipopokea siki, akasema: Imekwisha; akainama kichwa chake, akatoa roho yake. Basi Wayuda, kwa sababu ilikuwa Maandalio, miili isikae juu ya musalaba siku ya sabato (kwa sababu siku ya sabato ile ilikuwa siku kubwa), wakaomba Pilato, miguu yao ivunjwe, na waondolewe. Basi askari walikuja, wakamuvunja miguu wa kwanza, na wa pili, aliyesulibiwa pamoja naye; lakini wakati walipofika kwa Yesu, wakaona ya kama amekwisha kufa, hawakuvunja miguu yake; lakini mumoja wa askari alimuchoma mbavu yake kwa mukuki, na mara moja ilitoka damu na maji. Naye aliyeona alishuhudia, na ushuhuda wake ni kweli: na yeye anajua ya kwamba anasema kweli, ninyi mupate kuamini. Kwa maana maneno haya yalifanyika, ili andiko litimie: Hapana mufupa wake utakaovunjwa. Na tena andiko lingine linasema: Watamutazama yeye waliyemuchoma.

Kisha msomaji anasoma:

Usituache mpaka mwisho, sababu ya jina lako takatifu, usiharibu agano lako, na usitenge kwa sisi rehema yako, sababu ya Abrahamu mpendwa wako, na Isaaka mtumishi wako na Israeli mtakatifu wako.

Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

Kisha tunasoma Kontakion:

Kujeni wote tumwinamie huyu aliyesulubiwa kwa ajili yetu; Mzazi-Mungu alipomuona msalabani akamwambia: Wewe mwenye kuteswa na hii lufu, ndiwe kweli Mwana wangu na Mungu wangu.

Kisha tunasema: Bwana hurumia, (mara makumi ine) na hii sala: Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa. . . (Ona ukurasa 5).

Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia. Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . . Uliye wathamani. . . Kwa jina la Bwana barikia, ee padri:

Mungu atufazili na kutubariki, atuangazie uso wake na kutuhurumia.

Padri atasoma hii sala ya Mtakatifu Basile Mukubwa.

Ee Rabi na Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, mpole kwa kukasirika juu ya makosa yetu, unatufikisha mpaka hii wakati ambako ulipotundikwa juu ya msalaba wenyi kuleta uzima, ukamufungulia munyanganyi mlango ya paradizo na ukavunja mauti kwa lufu. Utuhurumie pia na sisi watumishi wako wasiostahili tena waovu; maana tulitenda zambi na hatustahili kunyanyua macho kwa kutazama mbinguni. Ndiyo, tuliacha njia ya haki, tulitembea kama ilivyopenda roho yetu. Lakini tunaomba wema wako: Utusamehe, ee Bwana, kadiri ya rehema yako kubwa na utuokoe kwa ajili ya jina lako takatifu, kwani tulijivuna katika maisha yetu. Utuondoe toka mkono ya adui, zima zambi zetu, regeza mawazo yetu ya mwili; hivi, tukiondoa mutu wa zamani, tutavaa mutu mupya, na tutaishi juu Yako wewe Rabi na Muombezi wetu; halafu, kwa kanuni zako, tutafika kwa mapumziko ya milele, kwa makao ya wenye heri wote. Kwani ni Wewe heri ya kweli tena furaha ya wale wenye kukupenda, ee Kristu Mungu wetu, na tunakutolea utukufu, pamoja na Baba yako asiye na mwanzo, na Roho wako Mtakatifu kamili, mwema na mletaji-uzima, daima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

HERI

Katika ufalme wako, utukumbuke, ee Bwana, utakapokuja katika ufalme wako. Heri walio masikini wa roho, maana Ufalme wa mbinguni ni wao.

Heri wenye huzuni: maana wao watafarijiwa.

Heri wenye upole: maana wao watariti inchi.

Heri wenye njaa na kiu haki: maana wao watashibishwa.

Heri wenye rehema: maana wao watapata rehema.

Heri wenye moyo safi: maana wao wataona MUnngu.

Heri wenye kufanya salama: maana wataitwa wana wa Mungu.

Heri walioteswa kwa sababu ya haki: maana ufalme wa mbinguni ni wao.

Heri ninyi, wakati wanapowatukana ninyi na kuwatesa ninyi nakuwasemea ninyi kila neno baya kwa uwongo, kwa sababu yangu.

Furahini, shangilieni; kwa sababu zawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyotesa manabii waliokuwa mbele yenu.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mutakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Utukumbuke, ee Bwana, wakati utakapokuja katika ufalme wako.

Utukumbuke, ee Rabi, wakati utakapokuja katika ufalme wako.

Utukumbuke, ee Mtakatifu, wakati utakapokuja katika ufalme wako.

Kundi la waimbaji wa mbinguni wanakuimbia na wanasema: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Savaothi, mbingu na dunia zimejaa na utukufu wako.

Njongeni kwake, na mutaangaziwa na uso wetu usipate haya.

Kundi la waimbaji wa mbinguni wanakuimbia na wanasema: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Savaothi, mbingu na dunia zimejaa na utukufu wako.

Utukufu kwa Baba. . .

Kundi la malaika na malaika Wakuu, pamoja na majeshi ya mbinguni wanakuimbia na waanasema: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Savaothi, mbingu na dunia zimejaa utukufu wako.

Sasa na siku zote. . .

Tunasoma Simbolo ya Imani: Nasadiki Mungu moja. . .

Kisha tunasoma:

Zima, ashilia, hurumia, ee Mungu, makosa yetu ya kutaka na yisiyokutaka, iliyofanyika kwa matendo na maneno, ya kujuwa na ya kutokujuwa ya usiku ao ya mchana, ndani ya akili na ya ufahamu; yote utuhurumie, sawa mwema na mpenda wanadamu.

Baba yetu uliye mbinguni. . .

Kontakion:

Kujeni wote tumwinamie huyu aliyesulubiwa kwa ajili yetu; Mzazi-Mungu alipomuona msalabani akamwambia: Wewe mwenye kuteswa na hii lufu, ndiwe kweli Mwana wangu na Mungu wangu.

Kisha tunasema: Bwana hurumia, (mara kumi na mbili).

Jina la Bwana lihimidiwe tangu sasa, na mupaka milele (*mara tatu*). Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Tunasoma zaburi hii:

Zaburi 34

Nitabariki Bwana wakati wote; sifa yake itakuwa kinywani mwangu daima. Nafsi yangu itajisifu katika Bwana; Wapole watasikia na watafurahi. Musifu Bwana pamoja nami, na tutukuze jina lake pamoja. Nilitafuta Bwana, naye alinjibu, na kuniponyesha toka woga zangu zote. Wakamutazama, na walitiwa nuru; Na nyuso zao hazitaona haya milele. Masikini huyu akalia, Bwana akamusikia, akamwokoza toka taabu zake zote. Malaika ya

Bwana anapiga kambi kuzunguka wale wanaomwogopa, na anawaokoa. Onjeni mwone ya kuwa Bwana ni Mwema; Heri mutu anayemuwekea tumaini lake. Ogopeni Bwana, ninyi watakatifu wake; Kwa sababu wale wanaomwogopa hawahitaji kitu. Wana-simba wanahitaji, wanaona njaa; Lakini wao wanaotafuta Bwana hawatakosa kitu cho chote kilicho chema. Njoooni, ninyi watoto, munisikilize; nitawafundisha ninyi woga wa Bwana. Ni nani mutu yule anayetaka uzima, na anayependa siku nyingi ili apate kuona mema? Uzuize ulimi wako na ubaya, na midomo yako na kusema hila. Uache mabaya ukatende mema; Tafuta salama, na kuifuata. Macho ya Bwana yanatazama wenye haki, na masikio yake ni wazi kwa kusikia kilio chao. Uso wa Bwana ni juu yao wanaotenda mabaya, aondoshe ukumbusho wao duniani. Wenye haki walilia, na Bwana alisikia, na kuwaponyesha toka taabu zao zote. Bwana ni karibu na wenye moyo wa kuvunjika, na anaokoa wenye roho ya toba. Mateso ya mwenye haki ni mengi; Lakini Bwana anamuponyesha nayo yote. Anachunga mifupa yake yote; haukuvunjika hata mumoja. Uovu utawa mwovu; nao wanaochukia wenye haki watahukumiwa. Bwana anakomboa nafsi ya watumishi wake; wala hawatahukumiwa wote wanaomuwekea yeye kimbilio lao.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Bwana hurumia (*mara tatu*), Rabi mtakatifu barikia.

Padri:

Kristu Mungu wetu ukweli, kwa maombezi ya Mama wake Mtakatifu asiye na doa wala si lawama kamili; ya Mitume Watakatifu watukufu, wasifiwa kamili na ya watakatifu wote, atuhurumie na atuokoe, kwani ni Mwema na mupenda-wanadamu.

Kwa maombezi ya wapadri watakatifu wetu, ee Bwana Yesu kristu, Mungu wetu, utuhurumie. Amina.

**UTUKUFU KWA UTATU MUTAKATIFU
MONASTERI YA MUTAKATIFU GRIGORIOS
KILIMA TAKATIFU
GREKIA
1999**

